# NAFASI YA MSHIKAMANO KATIKA KUKUZA MAUDHUI KATIKA INSHA ZA WANAFUNZI WA KIDATO CHA NNE KATIKA KAUNTI YA MURANG'A

**NA**

**MARGARET MORAA OGATO**

**C50/23537/2013**

**TASNIFU INAYOWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**APRILI, 2018**

# IKIRARI/UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kwa madhumuni ya kutuzwa shahada yoyote.

Sahihi ____________________ Tarehe 26|4|2018

Margaret Moraa Ogato C50/23537/2013

Tasnifu hii limetolewa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi ____________________ Tarehe 26/04/2018

DKT. Leonard Mwita Chacha

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

Sahihi ____________________ Tarehe 26.04.2018

DKT. Jacktone Okello Onyango

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

# TABARUKU

Kwa mamangu mzazi Florence Mosinya, mume wangu Tom, watoto wangu: Eddy, Adrian, Eliud, na Audley na Marehemu ndugu yangu John Kebaso, kwa kuichochea ari yangu ya uandishi na kwa kunipa muda rahisi nilipoiandika kazi hii. Ahsante kwa upendo wenu mkuu.

## SHUKRANI

Shukrani za dhati zimwendee Mungu Mwenyezi kwa afya aliyotukirimu mimi na wasimamizi wangu hadi tukakamilisha kazi hii.

Aidha, nawashukuru wasimamizi wangu Daktari Leonard Chacha na Daktari Jacktone Onyango. Mlijitolea na kujinyima ili kuisoma na kunielekeza kila nilipowahitaji. Mungu awatunze siku zote.

Shukrani pia zimwendee mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili Dkt. Wafula kwa kuhakikisha kuwa mipango na mawasiliano yote yaliyohusu kazi hii yanaenda sawa.

Sitawasahau wahadhiri wengine katika idara kama  Dkt. Mwihaki, Dkt.Ngugi, Dkt. Masinde, Dkt. Osore na Dkt. Arege kwa kunipa msingi katika kazi hii.

Wanafunzi niliokuwa nao darasani mathalani Wamalwa, Mary, Stephen, Margy, Sophy, Makau na Evans nawaombea Mola awaongoze kwa yote na ahsante sana kwa himizo mlilonipa.

Hatimaye, shukrani za dhati ziwaendee walimu na wanafunzi wa shule za Murang’a, Mugoiri, Njiiri, Kahuhia, Mahutia na Pioneer kwa kukubali kushirikishwa katika utafiti na hatimaye kuufanikisha.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MAALUMU

| | | |
|---|---|---|
| Kanuni | : | Sifa bia zinazotawala mifumo ya lugha zote za binadamu kwa mujibu wa sarufi zalishi. |
| Maudhui | : | Mambo muhimu |
| Mshikamano | : | Hali ambapo uelewa wa sehemu moja hutegemea uelewa wa sehemu iliyotangulia. |
| Umilisi | : | Ni uwezo wa msemaji wa lugha kutunga na kuelewa tungo za lugha yake. |
| Utendaji | : | Ni usemaji wa lugha fulani au utumiaji wa lugha; ni utumiaji wa ule uwezo wa kiisimu katika muktadha halisi. |
| Sarufi zalishi | : | Mtindo wa sarufi ambao unasisitiza ujuzi wa kanuni ubongoni mwa msemaji wa lugha unaomwezesha kuunda na kufasiri sentensi. |
| Semantiki | : | Taaluma ya Isimu inayochunguza maana. |
| Sintaksia | : | Ni jinsi kategoria za maneno huungana ili kuunda virai hadi sentensi. |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Al. | : | Alama |
| Bad | : | Ubadilishaji |
| KBC | : | Kenya Broadcasting Corporation |
| KCPE | : | Kenya Certificate of Primary Education |
| KCSE | : | Kenya Certificate of Secondary Education |
| KNEC | : | Kenya National Examinations Council |
| Lik | : | Kimilikishi |
| Lek | : | Leksia |
| Ling | : | Kilinganuzi |
| N | : | Nafsi |
| Ndel | : | Kiendelezo |
| Rej | : | Urejeshi |
| Rud | : | Urudiaji |
| S | : | Sentensi |
| SAM | : | Sarufi Amilifu Mfumo |
| Sh | : | Kiashiria |
| Taz. | : | Tazama |
| U | : | Kiunganishi |
| Uk. | : | Ukurasa |
| ___ | : | Kuashiria udondoshaji |

# IKISIRI

Utafiti huu ulitekelezwa kwa madhumuni ya kuchunguza nafasi ya mshikamano katika kukuza maudhui katika insha za wanafunzi wa shule za upili. Mtafiti alichunguza matatizo yanayohusiana na mshikamano pekee katika insha za wanafunzi wa shule za viwango mbalimbali; wilaya, kaunti na taifa. Wanafunzi lengwa ni wa kidato cha nne wa kaunti ya Murang'a. Kusudi la kuchunguza matatizo yanayohusiana na mshikamano lilikuwa kubainisha chanzo cha matatizo hayo kwa madhumuni ya kupendekeza mbinu mwafaka zinazoweza kutumiwa na walimu pamoja na wanafunzi ili kuimarisha ufunzaji na uandishi wa insha. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni nadharia za Sarufi Zalishi na Sarufi Amilifu Mfumo. Nadharia ya Sarufi Zalishi ilisaidia katika kutathmini ung'amuzi na matumizi ya vipengele vya mshikamano katika insha za wanafunzi. Nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo ilisaidia katika kudondoa na kuchanganua maudhui. Utafiti ulifanyiwa nyanjani pamoja na maktabani. Uteuzi wa sampuli kimakusudi ulitumiwa na shule sita zikachaguliwa. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuainisha mada tofauti tofauti kulingana na malengo ya utafiti kisha kuwekwa kwenye majedwali na vielelezo. Uchanganuzi ulitumia mihimili ya umilisi na utendaji ya Sarufi Zalishi na ya maana tambuzi, maana husishi na maana matinishi ya nadharia ya SAM. Mahitimisho yalionyesha kuwa matatizo ya mshikamano huathiri ubora wa insha za wanafunzi. Utafiti huu unanuia kuwafaidi wanafunzi, walimu watafiti na watahini.

## ABSTRACT

This research explored the place of cohesion in enhancing themes in students' compositions at secondary school level. The research explored the mistakes associated with cohesion only in students' compositions at different school levels; district, county and national levels. The aim of this was to analyse the causes of the mistakes so as solution can be sought to make learnig and teaching successful. The students involved are form four students from Murang'a County. The theories used in this research were Generative Grammar and Systematic Functional Grammar. The theory of Generative Grammar was used to analyse the different levels of cohesion in students' compositions; the students' ability to effectively use different aspects of cohesion in their proses. The theory of Systematic Functional Grammar helped in identifying and analysing themes in their proses. The research was carried out in the library and field and Purposeful sampling was done whereby six schools were selected. The data has been presented in form of charts and diagrams and later analysed as per the research objectives and questions. It was evident that improper usage of cohesive devices lower the undertstanding of themes in students' compositions. It is therefore necessary that teachers and students need to embrace and insist on proper usage of the same. This research is meant to benefit the following classes of people; teachers, students, researchers and examiners.

# YALIYOMO

MADA UKURASA

Ikirari/Ungamo......................................................................................................ii

Tabaruku………………………………………………………………………iii

Shukrani……………………………………………………………………. iv

Ufafanuzi wa Istilahi Maalumu…………………………………………….. v

Orodha ya Vifupisho……………………………………………………….. vi

Ikisiri …………………………………………………………………………vii

Abstract……………………………………………………………………… viii

Yaliyomo………………………………………………………………………ix

Orodha ya Majedwali, Chati na Vielelezo……………………………………xvi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..............................................................1

1.0 Usuli wa Mada ..............................................................................................1

1.1 Swala la Utafiti ..............................................................................................3

1.2 Maswali ya Utafiti...........................................................................................4

1.3 Malengo ya Utafiti ..........................................................................................4

1.4 Sababu za Kuchagua Mada....5
1.5 Upeo na Mipaka....6
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada....7
1.6.1 Kumudu Utunzi....7
1.6.2 Tafiti Kuhusu Insha....8
1.6.3 Maandishi Jumlifu Kuhusu Mshikamano....10
1.6.4 Tafiti Kuhusu Mshikamano....10
1.7.0 Misingi ya Nadharia....14
1.7.1 Nadharia ya Sarufi Zalishi....14
1.7.2 Nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo....17
1.8.0 Mbinu za Utafiti....20
1.8.1 Muundo wa Utafiti....20
1.8.2 Mahali pa Utafiti....20
1.8.3 Mbinu za Usampulishaji Data....21
1.8.4 Vifaa vya Kukusanya Data....22
1.8.4.1 Insha....22
1.8.4.2 Zoezi....22
1.8.4.3 Hojaji....22
1.8.4.4 Ukaguzi wa Madaftari....23

1.8.5 Maadili ya Utafiti ....................................................................................23

1.8.6 Uchanganuzi wa Data......................................................................................23

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo ...............................................................................24

SURA YA PILI: UKUZAJI WA VIPENGELE VYA MSHIKAMANO............25

2.0 Utangulizi ..........................................................................................................25

2.1 Maana ya Mshikamano ...................................................................................25

2.2 Urejeshi.............................................................................................................27

2.2.1 Urejeshi Sabiki ..............................................................................................28

2.2.2 Urejeshi Dokezi .............................................................................................29

2.2.3 Urejeshi Nje.....................................................................................................31

2.2.4 Urejeshi Nafsi..................................................................................................34

2.2.5 Urejeshi wa Kuashiria.....................................................................................36

2.2.6 Urejeshi Linganuzi...........................................................................................40

2.3 Mshikamano wa Kuunganisha..........................................................................42

2.4 Mshikamano wa Kileksia ..................................................................................47

2.4.1 Kategoria za Leksimu ......................................................................................48

2.4.2 Nomino za Kawaida.........................................................................................48

2.4.3 Urudiaji ............................................................................................................49

2.4.3.1 Sinonimu ........................................................................................................50

2.4.3.2 Homonimu ..................................................................... 52

2.4.3.3 Antonimu ..................................................................... 53

2.4.3.4 Hiponimu ..................................................................... 55

2.4.3.5 Meronimu ..................................................................... 55

2.4.3.6 Uhusiano-leksika ..................................................................... 55

2.4.4 Ruwaza za Mshikamano wa Kileksia ..................................................... 56

2.5 Mshikamano wa Ubadilishaji ..................................................................... 60

2.6 Mshikamano wa Udondoshaji ..................................................................... 63

2.7 Mshikamano na Kiimbo ..................................................................... 66

2.7.1 Mkondo wa Panda-Shuka ..................................................................... 67

2.7.2 Mkondo - Shuka ..................................................................... 67

2.8 Hitimisho ..................................................................... 68

SURA YA TATU: MATUMIZI POTOSHI YA MSHIKAMANO KATIKA INSHA ZA WANAFUNZI ..................................................................... 69

3.0 Utangulizi ..................................................................... 69

3.1 Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi ..................................................................... 70

3.2 Makosa ya Kileksia ..................................................................... 72

3.3 Makosa ya Viunganishi ..................................................................... 74

3.4 Makosa ya Tafsiri Isiyofaa ..................................................................... 76

3.5 Makosa ya Urudiaji ........................................................................78
3.6 Makosa ya Urejeshi ........................................................................80
3.7 Makosa ya Viashiria ........................................................................81
3.8 Makosa ya Vilinganuzi ........................................................................82
3.9 Makosa ya Vimilikishi ........................................................................83
3.10 Makosa ya Nafsi ........................................................................84
3.11 Makosa ya Mshikamano katika Sentensi ........................................................................84
3.12 Makosa ya Udondoshaji ........................................................................85
3.13 Makosa ya Mshikamano katika Tungo ........................................................................86
3.14 Hitimisho ........................................................................91
SURA YA NNE: CHANZO CHA MAKOSA YA MSHIKAMANO NA NAMNA YA KUUBORESHA ........................................................................92
4.0 Utangulizi ........................................................................92
4.1 Mbinu za Kufunzia ........................................................................93
4.1.1 Mbinu za Kufunzia Insha ........................................................................93
4.1.2 Mbinu za Kufunzia Viunganishi ........................................................................94
4.1.3 Mbinu za Kufunzia Msamiati ........................................................................95
4.1.4 Mbinu ya Idadi ya Masomo ya Insha na Kusahihisha ........................................................................95
4.2 Mbinu Zinazohusu Mwanafunzi ........................................................................97

4.3 Ukaguzi wa Madaftari ya Insha za Wanafunzi ............................................98
4.4 Namna ya Kuboresha Mshikamano ..........................................................106
4.5 Hitimisho ................................................................................................111
SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................112
5.0 Utangulizi ...............................................................................................112
5.1 Muhtasari................................................................................................112
5.1.1 Lengo la Kwanza ....................................................................................113
5.1.2 Lengo la Pili ...........................................................................................113
5.1.3 Lengo la Tatu..........................................................................................113
5.1.4 Lengo La Nne .........................................................................................114
5.2 Matokeo ya Utafiti ..................................................................................114
5.3 Changamoto Wakati wa Utafiti ................................................................118
5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti huu.....................................................119
5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ..................................................................121
5.6 Hitimisho .................................................................................................121
MAREJELEO................................................................................................122
VIAMBATISHO ...........................................................................................130
Kiambatisho (i): Insha kwa Wanafunzi ........................................................130
Kiambatisho (ii): Zoezi kwa Wanafunzi.......................................................137

Kiambatisho (iii): Hojaji kwa Walimu ........................................................139

Kiambatisho (iv): Kibali cha Utafiti............................................................143

Kiambatisho (v): Mwongozo wa KNEC wa Kusahihisha Insha.....................144

## ORODHA YA MAJEDWALI, CHATI NA VIELELEZO

Jedwali 2.1: Mrejeo Sabiki…………………………………………………………28

Jedwali 2.1: Mrejeo Dokezi……………………………………………………...30

Jedwali 2.3: Mrejeo Nje……………………………………………………….33

Jedwali 2.4: Virejeshi vya Nafsi na Vimilikishi.................................................35

Jedwali 2.5: Nafsi na Vimilikishi………………………………………………...35

Jedwali 2.6: Jedwali la Viashiria………………………………………………...37

Jedwali 2.7: Jedwali la Vibainishi……………………………………………….38

Jedwali 2.8: Viashiria na Vishamirishi…………………………………………..39

Jedwali 2.9: Vilinganuzi…………………………………………………………41

Jedwali 2.10: Viunganishi………………………………………………………..46

Jedwali 2.11: Mshikamano wa Kileksia…………………………………………57

Jedwali 2.12: Mshikamano wa Ubadilishaji……………………………………..60

Jedwali 2.13: Mshikamano wa Udondoshaji…………………………………….63

Jedwali 3.1: Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi………………………………...70

Jedwali 3.2: Makosa ya Kileksia……………………………………………...72

Jedwali 3.3: Makosa ya Viunganishi……………………………………………74

Jedwali 3.4: Tafsiri Isiyofaa…………………………………………………...77

Jedwali 3.5: Makosa ya Urudiaji……………………………………………...78

Jedwali 3.6: Makosa ya Urejeshi……………………………………………...80

Jedwali 3.7: Jedwali la Makosa ya Viashiria…………………………………….81

Jedwali 3.8: Muhtasari wa Makosa……………………………………………90

Chati 2.1: Ukuzaji wa Mshikamano wa Kuunganisha…………………………...47

Chati 4.1: Chati ya Usahihishaji wa Vitabu…………………………………….100

Kielelezo 1.1: Viwango vya Umilisi na Utendaji………………………………..16

Kielezo 1.2: Viathiri vya Umilisi na Utendaji…………………………………...16

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Lugha huwa na jukumu kubwa mno kwani kupitia kwayo mawasiliano hufanikiwa. Aidha, huwa ndiyo nguvu za kuunganisha wanajamii kwa kuwafanya kutangamana na kwa njia hii huleta uelewano na umoja. Hata hivyo, mawasiliano yayo hayo yanaweza kukwazwa. Kwa mfano, kupitia kwa maneno yaliyotolewa kwa njia isiyo wazi na kutoelewa ujumbe vyema miongoni mwa mengine. Hali hii inaweza kuletwa miongoni mwa mengine, na mshikamano.

Suala la mshikamano ni muhimu mno katika tungo na linajikita katika eneo pana la kiusomi la Isimu-matini. Isimu-matini hushughulikia uchambuzi wa matini nzima na utendakazi wa vipengele hivyo katika matini husika. Taaluma hii huchukulia matini inayochambuliwa kama tukio la mawasiliano (Taz. Dressler na Beaugrande 1981). Hii ndiyo sababu wataalamu mbalimbali wamelishughulikia suala hili zima; wa Kimagharibi na wa Kiafrika. Kwa mfano, Hope na Write (1996) wanasema kuwa mshikamano huleta uendelezaji wa maudhui, usababishi wa visa na kadhalika.  Habwe na Karanja (1999) nao wanasema kuwa mshikamano husaidia katika uelewaji wa matini kwani uelewaji wa sehemu moja ya matini hutegemea uelewaji wa matini iliyotangulia.

Ukuzaji wa ujuzi wa kuhesabu, kuandika na kusoma huunda msingi wa mtaala wa shule za msingi (Kariuki, 2012). Katika shule za upili, kila wiki imetengewa

kipindi cha kusoma na kuandika. Hann (1984), kwa mfano, huonyesha kuwa kuandika na kusoma ni vipengele muhimu katika kupitisha mawazo. Umuhimu huu umesisitizwa kupitia kwa sera ya elimu na shule mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umejaribu kuchunguza kiwango cha ubunifu wa kushikamanisha wazo kwa kutumia vipengele mbalimbali vya mshikamano hadi liweze kuleta maana iliyokusudiwa. Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya mshikamano na muwala; ili mshikamano uwepo, lazima kuwe na muwala lakini muwala hauhitaji mshikamano ili kufanikisha uelewa. Nchini Kenya, wanafunzi hutahiniwa kwa somo la Kiswahili. Hata hivyo, wao hutatizika mno na kujenga mshikamano katika tungo zao (Thiga, 1997).

Aidha, tafiti zaidi zinaonyesha kuwepo kwa makosa ya urejeshi wa kulinganisha (Nyarige, 2002). Saddimbah (2012) naye alibaini ukosefu wa matumizi ya mshikamano wa ubadilishaji na udondoshaji katika mahubiri ya Dholuo. Kwa mujibu wa ripoti za KNEC za 2009-2013, ukosefu wa mshikamano umesemekana kuwa na mchango mkubwa kwa matokeo mabaya katika insha za wanafunzi katika kiwango cha kitaifa (Taz. Ripoti ya KNEC, mwaka wa 2012, uk.5). Jedwali lifuatalo linadhihirisha haya kuhusu Kiswahili karatasi ya 102/1 (insha);

**Jedwali 1.1: Ripoti ya KNEC ya Karatasi ya 102/1 ya Mwaka 2009 -2013**

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2009 | 102/1 | 335,377 | 40 | 15.40 | 6.93 |
| 2010 | 102/1 | 354,738 | 40 | 14.32 | 6.53 |
| 2011 | 102/1 | 410,807 | 40 | 16.43 | 5.61 |
| 2012 | 102/1 | 433,886 | 40 | 10.43 | 3.63 |
| 2013 | 102/1 | 455,555 | 40 | 18.46 | 5.44 |

Asili: Ripoti ya KNEC ya Mwaka 2012, Uk.5

Kama inavyojitokeza katika jedwali hili, alama wastani katika miaka mitano mfululizo (2009-2013) haijafika nusu ya upeo (20).

Baadhi ya wataalamu hushikilia kuwa uwezo wa kuandika husaidia kukuza mawazo ya watoto na jinsi wanavyojieleza (Kroll, 1990). Hata hivyo, baadhi ya wataalamu hushikilia kuwa uwezo wa kuandika ni mgumu na hutegemea vigezo vya kijamii, vya akili na kiisimu (Vygotsky,1986, Edelsky,1986, na Hedge, 1988). Utafiti huu umechunguza kiwango cha mshikamano katika tungo za insha za wanafunzi wa kidato cha nne.

## 1.1 Swala la Utafiti

Baraza la Mitihani nchini Kenya linatoa ripoti za mitihani kipindi kwa kipindi. Katika ripoti zake za mwaka 2004 hadi 2007, Baraza lilitambua kuwa wanafunzi wa shule za upili walifanya vibaya katika somo la insha. Sababu kuu za matokeo mabaya ni miundo mibaya ya sentensi, upatanisho wa kisarufi usiofaa na mwambatano usiofaa wa nafsi na virejeshi. Swala la kutoambatanisha virejeshi ni swala la mshikamano. Ripoti za hivi karibuni za mwaka 2011 hadi 2013 bado

zinaonyesha kuwa wanafunzi wanakosa kuoanisha mada ipasavyo na kwa hivyo insha zao zinakosa mshikamano. Ni kwa sababu hii ndipo utafiti huu unakusudia kuangalia nafasi ya mshikamano katika kukuza maudhui katika insha za wanafunzi wa shule za upili hasa wa kidato cha nne. Baadhi ya tafiti zilizoshughulikia mshikamano ni kama Nyarige (2002) na Saddimbah (2011). Hawa waliangazia mshikamano wa kurejelea na mahubiri ya Dholuo mtawalia. Utafiti huu umeziba pengo kwa kuangazia vipengele vyote vya mshikamano katika insha za wanafunzi.

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo;

i) Mshikamano umekuzwaje katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne?

ii) Mshikamano umelemazwaje katika insha husika?

iii) Chanzo cha matatizo ya mshikamano ni kipi?

iv) Mshikamano katika insha za wanafunzi unaweza kuboreshwaje?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo;

i) Kuonyesha jinsi mshikamano ulivyokuzwa katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne.

ii) Kubainisha vile mshikamano umelemazwa katika insha husika.

iii) Kuonyesha chanzo cha matatizo ya mshikamano.

iv) Kuonyesha namna mshikamano katika insha za wanafunzi unaweza kuboreshwa.

**1.4 Sababu za Kuchagua Mada**

Matini nyingi huwa katika mtindo wa insha. Kwa mfano, matini ya vitabu, vyombo vya habari, mtandao na majarida. Aidha, wanafunzi wanapoandika mitihani yao, huifanya kiinsha. Uelewa wa matini husika hutegemea ni kwa kiwango kipi maneno na sentensi zimeshikamana. Kulingana na Kitsao (1995), insha ina mchango mkubwa katika ufunzaji wa matumizi ya lugha na kukuza stadi za uandishi kwa jumla. Naye Candlin (1952), katika kusisitiza mawazo hayo anasema kwamba kupitia kwa insha mwandishi hueleza maoni, athari na tajriba zake binafsi. Ni kwa sababu ya umuhimu huu ndipo utafiti huu umefanywa. Kukiwa na mshikamano katika tungo mbalimbali, basi kile kinachowasilishwa hueleweka bila tatizo.

Pili, kuna haja ya utafiti huu kwa sababu ya matokeo mabaya ya karatasi ya kwanza (karatasi 102/1: Insha) katika mitihani ya kitaifa. Utafiti huu umenuia kuwafaa wanafunzi waweze kuandika tungo zilizo na mshikamano. Matumaini ni kuwa walimu na watahini pia watatumia maarifa haya kuwafunza wanafunzi namna ya kuandika tungo nzuri; ambazo hazitatizi uelewa.

Isitoshe, utafiti huu una thamani ya kuongeza maarifa kuhusu mada. Mshikamano umeangaziwa na watafiti wengine lakini si katika maswala yanayoangaziwa na utafiti huu.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umejikita katika Kaunti ya Murang'a kwa sababu matokeo ya somo la Kiswahili katika kaunti hii miaka ya 2012 na 2013 hayakuwa bora; ilichukua nafasi ya 33 na 32 mtawalia kwa jumla ya kaunti 47.

Wanafunzi husika ni wa kidato cha nne. Shule sita zilichaguliwa kwa kufuata kigezo cha aina ya shule. Kuna vipengele vingi katika uandishi wa insha kama vile; mtindo na sarufi lakini utafiti huu umeshughulikia matatizo yanayohusiana na mshikamano pekee; chanzo cha makosa hayo na suluhisho. Aidha, utafiti huu umejikita kwa mshikamano na kupuuza vipengele vingine vya matini kama vile vilivyokuzwa na Beaugrande na Dressler (1981). Hivi ni kusudi, ukubalifu, ujuzi/maarifa, muktadha, muwala na mwingiliano matini. Sababu kuu hapa ni kuwa mshikamano ndilo swala la utafiti katika utafiti huu.

Sarufi Zalishi ina mihimili mingi lakini utafiti huu utatumia mihimili ya utendaji na umilisi ili kutathmini ung'amuzi na matumizi ya vipengele vya mshikamano katika insha husika. Aidha, vitengo vya sintaksia na semantiki katika nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo ndivyo vimetumika.

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii imechunguza maandishi kuhusu kumudu kwa utunzi, tafiti kuhusu insha na tafiti na maandishi jumlifu kuhusu mshikamano.

#### 1.6.1 Kumudu Utunzi

Allen na Vallette (1972) wanasema kuwa utunzi huanza kwa kuandika kuliko rahisi na huishia mhusika anapoandika bila tatizo. Wanaojifunza uandishi wanatarajiwa kutunga mashairi, michezo na utunzi unaohusu uwanja mpana. Mazoezi mengi ya insha hutimiza wazo hili. Kuczaji (1984) anasema kuwa uwezo wa kuwasilisha ujumbe hukua hatua kwa hatua. Mawazo haya yanaendelezwa na Scinto (1986) anayesema kuwa ukomavu wa mwandishi hujitokeza pale anapokuwa na uwezo si tu wa kutunga neno moja au sentensi bali wa usemi kamilifu. Kwake, kilicho muhimu ni uwezo wa matini kutoa ujumbe kikamilifu. Hii ndiyo sababu utafiti huu umejikita katika nafasi ya mshikamano katika kukuza maudhui katika tungo husika.

Walimu wanastahili kuhimiza ubunifu wa mawazo kwa wanafunzi wao. Mhusika huwa na ubunifu anapogundua utakubalika na wengine (Digolo, 1986). Mawazo ya mwanafunzi yakikubalika na wengine, atakuwa na moyo wa kuandika zaidi na kadri atakavyoandika zaidi, ndivyo uwezo wake wa kushikamanisha matini utakavyokua.

Crystal (1988) naye anasema kuwa uandishi ni mtindo wa mawasiliano ambao ni mgumu na kwa hivyo huhitaji mhusika kujifunza, kuvumilia na kutumia muda wa

kutosha kuufanya. Anaongeza kuwa ujuzi huu si muhimu tu vyuoni bali pia katika maisha ya kila siku. Insha za wanafunzi zitachanganuliwa na mtafiti ili kubaini mawasiliano yao kupitia maudhui.

Kinneavy na Warriner (1993) wanasema kwamba waandishi huandika kwa sababu mbalimbali. Baadhi yao huandika kuonyesha mitazamo yao, ubunifu, kusihi au kufahamisha. Haya yanaweza kufanikiwa kupitia kwa uandishi wa insha.Tumechunguza insha za wanafunzi ili kutathmini haya.

### 1.6.2 Tafiti Kuhusu Insha

Okwara (1989) alichunguza visababishi vya matokeo ya insha za Kiingereza katika shule za upili. Baadhi yavyo, kulingana na utafiti wake, ni ukosefu wa vifaa vya kutumia, aina ya shule, matokeo ya watangulizi, maarifa, miongoni mwa vingine. Utafiti wake ni muhimu kwa huu lakini ni tofauti kwa sababu ulichunguza visababishi vya matokeo mabaya katika insha kwa jumla.

Tahajia ni suala muhimu katika uandishi wa insha. Hii ndiyo sababu Nyamasyo (1994) aliangalia makosa ya tahajia katika insha za wanafunzi wa viwango viwili vya mwisho kabla waingie chuoni. Aligundua kuwa makosa ya tahajia yakiwa mengi huathiri uelewa wa insha husika.

Swala la athari ya lugha ya kwanza kwa uandishi wa insha za Kiswahili pia limeshughulikiwa na Were (1996). Alitumia wanafunzi Wabukusu 120 wa kidato cha tatu. Aligundua kuwa lugha ya kwanza ina athari kubwa kwani makosa ya kisarufi yalichukua asilimia 29, ya maendelezo 61.4 na ya msamiati 56.3 ya

makosa yote kwa jumla.  Aidha, wanafunzi walikosa vitabu vya Kiswahili na walipokosa ung'amuzi wa msamiati katika lugha ya Kiswahili, walikopa kutoka lugha ya kwanza. Utafiti wake unahusu wanafunzi wa kidato cha tatu pekee, tofauti na huu unaohusisha kidato cha nne.

Mutugu (2001) naye aliangazia makosa ya kileksia katika insha na chanzo chake. Aligundua kuwa wanafunzi wa kidato cha pili hufanya makosa mengi ya kileksia katika insha zao. Makosa hayo yalitokana na athari ya lugha yao ya kwanza na mbinu za walimu za kufunzia. Aidha, alibaini kuwa takribani asilimia tisini na nane ya wanafunzi walioshiriki walifanya makosa ya tahajia. Utafiti wake utakuwa na umuhimu kwa huu japo huu ni tofauti.

Ombati (2009) alichunguza tofauti kati ya insha za maelezo za wanafunzi walio na matatizo ya kuona na vinginevyo. Aligundua kuwa kwa wanafunzi wasioona, insha ya aina hii huwatatiza sana kuliko wenzao wasio na tatizo la kuona. Utafiti wake, tofauti na huu, unachunguza insha za maelezo.

Makosa ya kisintaksia katika uandishi wa insha za wanafunzi wa shule za upili huathiri ubora wa insha kwa kiwango kikubwa. Hili nalo limeshughulikiwa na Kariuki (2012). Alitambua kuwa makosa ya ufungami, utegemezi muundo, ufasiri kamili, ya kileksia na uarifu hutokea katika insha zao. Hata hivyo, makosa ya ufungami na utegemezi muundo yalibainika kuwa sugu. Alivumbua vyanzo vya makosa hayo na suluhisho. Utafiti huu, tofauti na wake, umehusisha semantiki.

### 1.6.3 Maandishi Jumlifu Kuhusu Mshikamano

Halliday na Hasan (1976) wanasema kuwa mshikamano unaletwa na urejeshi, udondoshaji, ubadilishanaji, uunganishaji na matumizi ya vipengele vya kileksia. Wanachukulia mshikamano kama kiungo muhimu cha matini na maana hupatikana kupitia mshikamano huo. Utafiti huu  umetumia vipengele hivyo katika kutathmini kiwango cha mshikamano katika insha husika.

Yde na Spoelders (1985) wanasema kuwa makosa ya mshikamano yanayohusiana na urudiaji yanaweza kuhusishwa na ufinyu wa uwezo wa kiakili wa watoto husika. Hata hivyo, Scinto (1986) anasema kuwa uwezo wa matumizi ya lugha ya mtu hujitokeza katika uwezo wa mhusika wa kutunga matini; iliyo na maana fupi au ndefu. Kwa mujibu wake, kipengele kimoja cha mshikamano huitwa kifungo.

Mbaabu (1995) anaonyesha kuwa watu wa viwango mbalimbali katika jamii hufanya makosa ya kisintaksia wanapozungumza na kuandika.  Hii ndiyo sababu Njoroge (2006) anasisitiza kuwa wanafunzi wanahitaji kuzoeshwa miundo sahihi ya sentensi katika usemi na uandishi. Utafiti huu unakubaliana na wazo hili ndiposa umejaribu kuonyesha umuhimu wa mshikamano.

### 1.6.4 Tafiti Kuhusu Mshikamano

Tafiti nyingi zilizorejelewa hapa ni zile zilizofanywa katika lugha ya Kiingereza. Witte na Falgley (1981) walichunguza uhusiano kati ya mshikamano na ufaafu wa kilichoandikwa. Waligundua kuwepo kwa uhusiano wa karibu kati ya vipengele

hivi viwili. Utafiti huu umeangazia uhusiano lakini kati ya mshikamano na maudhui husika.

Fitzgerald na Spiegel (1981) waliangalia mshikamano na muwala kati ya watoto wa gredi ya sita na saba. Waligundua kuwepo kwa uhusiano kati ya muwala na mshikamano. Utafiti huu ni tofauti na wao kwani unashughulikia wanafunzi wa shule ya upili.

Mshikamano kati ya watoto wa gredi ya tatu na sita pia umeshughulikiwa na Yde na Spoelders (1985). Waligundua kuwa watoto wakiwa wakubwa, kiwango chao cha mshikamano huwa juu. Aidha, makosa fulani huhusishwa na viwango mbalimbali vya kujifunza na kuandika. Utafiti huu umetofautiana na wao kwa sababu utahusisha wanafunzi wa kidato cha nne.

Jafarpur (1991) aliangalia mshikamano katika wanafunzi walio na uwezo tofauti. Katika kufanya hivi, alijikita sana katika kipengele cha mshikamano cha urejeshi. Utafiti wake unahusiana na huu kwa ambavyo unahusu mshikamano. Tofauti kati ya utafiti wake na huu ni kuwa alisisitiza kipengele cha urejeshi. Utafiti huu umehusisha vipengele vyote vya mshikamano.

Karanja (1993) aliangalia jinsi mshikamano, muwala na uelewa vinavyojitokeza katika matangazo ya Kituo cha Utangazaji cha Kenya (KBC). Utafiti wake ulichunguza matangazo lakini huu ulichunguza insha za wanafunzi. Aidha, Yousif (1995) naye aliangazia mshikamano katika usemi zungumzi miongoni mwa Waarabu wa viwango mbalimbali. Alitumia kielelezo cha Halliday na Hasan

(1976). Utafiti wake unachangia huu lakini data na nadharia yake ni tofauti na zilizotumika katika utafiti huu.

Thiga (1997) aliangazia mshikamano katika insha za wanafunzi wa darasa la nne na nane katika shule za mjini nchini Kenya. Alibaini kuwa wanafunzi walitatizwa na mbinu za kujenga ushikamano katika uandishi wa insha. Alibaini kwamba mshikamano wa kurejelea ulitumiwa zaidi huku wanafunzi wa darasa la nne wakiwa na shida kuutumia. Mshikamano wa udondoshaji na ubadilishaji haukutumiwa kabisa na viwango hivyo viwili. Utafiti wake ulichangia utafiti huu lakini u tofauti. Utafiti wake ulilenga wanafunzi wa miaka minne hadi kumi tena wa mjini. Vile vile, alitaka kubaini uwezo wa wanafunzi wa kuandika kwa kutumia lugha ngeni na alitumia nadharia tofauti na zilizotumiwa katika utafiti huu na wanafunzi lengwa katika utafiti huu ni wa shule za upili; wa mjini na mashinani.

Onguko (1999) aliangalia mshikamano katika makala ya kiusomi na magazeti. Aligawa vipengele vya mshikamano katika makundi mawili; visivyobadilika na ambavyo hubadilika. Utafiti huu haukufanya mgao huo na data yake ni insha za wanafunzi, tofauti na ya Onguko ambayo ni makala ya kiusomi na magazeti.

Mpangilio wa maudhui na mshikamano wa kurejelea umeshughulikiwa na Nyarige (2002) katika tungo za wanafunzi wa kidato cha tatu. Alitathmini kielelezo cha Halliday na Hassan katika kuhakiki insha husika. Hakuangalia mshikamano katika kishazi kizima kwa sababu alijishughulisha zaidi na

uthematiki. Aligundua kuwa makosa ya urejeshi wa nafsi ya kwanza hayakuwa mengi kama ya urejeshi wa kulinganisha. Utafiti wake, tofauti na huu, unahusisha wanafunzi wa kidato cha tatu pekee na aliangazia mshikamano wa kurejelea pekee. Huu umejikita katika vipengele vyote vye mshikamano na utalenga kidato cha nne. Aidha, wake ulijihusisha zaidi na sintaksia. Huu ulihusisha sintaksia na semantiki. Utafiti huu umejumuisha kishazi kizima tofauti na wake.

Saddimbah (2011) alishughulikia mshikamano katika usemi zungumzi wa mahubiri ya wasemaji wa Dholuo. Alibaini kuwa mshikamano wa ubadilishaji na ule wa udondoshaji haukuwepo. Ule wa kileksia ulikuwa asilimia 51. Alichanganua mahubiri lakini utafiti huu umechanganua insha za wanafunzi.

Mbinu zinazotumiwa katika ufunzaji wa insha huathiri matokeo ya insha kwa kiwango kikubwa. Wazo hili linajitokeza wazi katika kazi ya Mogere (2013) ambaye alishughulikia mbinu mbalimbali zinazotumiwa katika ufunzaji wa insha. Alibainisha kwamba mazoezi waliyopewa wanafunzi hayakufuata mkondo mahususi na walimu hawakujiandaa vilivyo kwa somo hilo kwani walichokitegemea sana ni mbinu ya maswali na majibu; mbinu ambayo ilimpendelea mwalimu zaidi kuliko mwanafunzi. Aidha, kulikuwa na matumizi mabaya ya vifaa vya kufunzia. Licha ya utafiti wake kufanyiwa wanafunzi wa shule za msingi, ni muhimu sana kwa utafiti huu. Sababu mojawapo ni kuwa bila mkondo muhimu na maandalizi ya kutosha kuhusu somo la insha, wanafunzi katu

hawataweza kuimarisha mshikamano katika insha zao. Mbinu mwafaka za kufunzia ni muhimu katika kukuza mshikamano katika tungo.

### 1.7.0 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Sarufi Zalishi na nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo. Nadharia ya Sarufi Zalishi ilisaidia katika kutathmini kiwango na uwezo wa mwanafunzi wa kutumia vipengele mbalimbali vya mshikamano kwa njia ifaayo. Nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo ilitumiwa kudondoa na kuchanganua maudhui katika insha husika.

### 1.7.1 Nadharia ya Sarufi Zalishi

Nadharia hii iliasisiwa na Noam Chomsky miaka ya sitini. Anashikilia kuwa kila binadamu ana uwezo wa kupata na kujifunza lugha. Aliangalia lugha kama mfumo wa ujuzi uliojiwakilisha kwa njia moja au nyingine akilini mwa msemaji. Onyango (2006) anaonyesha maendeleo ya nadharia hii kama ifuatavyo; Sarufi Bia 1965, sheria na vigezo 1967, Utawala na Ufungami 1981, Fonolojia Arudhi 1981, Fonolojia Leksia 1984, Fonolojia Vipande Sauti 1986, Fonolojia Mizanishi 1990, Fonolojia Umbo Upeo 1993 na Sintaksia Finyizi 1995 inayosisitiza kanuni na ndio sahili zaidi. Kanuni hizi ni kanuni ya ufungami, utawala, uarifu, tegemezi muundo, leksia miongoni mwa zingine. Mihimili yake ni kama ifuatayo;

1. Umilisi na utendaji. Umilisi ni ule uwezo wa kiisimu; ni ule ujuzi wa mzungumzaji asilia wa lugha. Chomsky (1965) anaueleza kama ule uwezo wa

mzungumzaji asilia wa lugha wa kumudu lugha yake. Utendaji ni yale matumizi ya lugha katika muktadha halisi.

Utafiti huu ulitumia mihimili hii miwili. Umilisi ulitumiwa kutathmini uwezo wa mwanafunzi wa kumudu vipengele mbalimbali vya mshikamano kama vile viunganishi, vipengele vya kileksia, urejeshi, ubadilishaji na udondoshaji. Mhimili wa utendaji nao ulitumiwa kutathmini matumizi halisi ya vipengele hivyo katika insha za wanafunzi.


Hata hivyo, si kila wakati utendaji utatumiwa kupima umilisi. Kulingana na Hymes (1965), mazungumzo ya kawaida huonyesha mianzo ya uongo mwingi, ukiukaji wa sheria na kubadilisha nia katikati ya mazungumzo. Kwa hivyo, utendaji wa kiisimu ni kama ghushi wa umilisi kamili. Utafiti huu unakubaliana na wazo hili kwamba kuna miktadha ambayo husababisha tofauti kati ya umilisi na utendaji wa mhusika. Utendaji unaweza kuathiriwa na mambo yafuatayo; usahaulifu, uoga, umri, kosa dogo katika kusema, uchovu, kutomakinika, hasira na hali.

Aidha, utendaji unaweza kuyumbayumba huku umilisi ukibaki pale pale. Umilisi utabaki katika asilimia sawa kwa muda ikiwa mhusika hajajiongezea maarifa yoyote.

Kawaida, umilisi huwa juu kuliko utendaji lakini kuna muktadha ambapo utendaji unaweza kuwa juu kuliko umilisi. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kutumia


njia zisizofaa ili kupita mtihani. Utafiti huu uljaribu kupunguza miktadha ambayo inaweza kuathiri matokeo. Vifuatavyo ni vielelezo vinavyoonyesha viwango vya umilisi na utendaji na vilevile viathiri vyavyo;

**Kielelezo 1.1: Viwango vya Umilisi na Utendaji**




Asili: Ukadiriaji wa Mtafiti

**Kielelezo 1.2: Viathiri vya umilisi na utendaji**




Asili: Ukadiriaji wa mtafiti

2. Mhimili mwingine ni kuwa Sarufi Zalishi haielezei tu tungo ambazo tayari zimezuliwa au kutungwa lakini inaweza kuzua kwa kubashiri tungo zote ambazo

kuna uwezekano wa kuzitoa katika lugha husika au pengine hazijawahi hata kutolewa.

3. Sarufi Zalishi hueleza sentensi ambazo ni sahihi na zile ambazo si sahihi katika lugha husika.

4. Sarufi Zalishi inajieleza kinaganaga na kwa uwazi hivi kwamba msomaji wa sarufi hii hapaswi kutumia makisio yoyote au ujuzi wowote kubaini yanayoelezwa.

Onyango (2006) pia anaonyesha mihimili minne; umilisi na utendaji, sarufi ya lugha kuwa kielelezo cha umilisi wa mzungumzaji, isimu hujishughulisha na utazamaji wa sifa bainifu na sarufi iwe na sheria na muundo bainifu za tungo.

### 1.7.2 Nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo

Utafiti huu uliongozwa pia na nadharia msingi ya Isimu Amilifu. Nadharia ya Isimu Amilifu ilichipuka mnamo miaka ya 1960. Wanaisimu wa wakati huo kama vile Halliday walisisitiza uamilifu wa utambuzi na uamuzi ambao watu hufanya ili kujenga mawasiliano baina yao. Nadharia hii imeendelelezwa kama ifuatavyo; Halliday (1985), Halliday (1997), Halliday (1999), Halliday na Mathiessen (2004) na Mathiessen (2013). Isimu Amilifu inafidia upungufu wa falsafa na mtazamo wa Sarufi Zalishi kwa kutambua kuwa lugha ni mali ya jamii, wala siyo umilisi wa mtu binafsi. Kwa mujibu wa Halliday (1994), nadharia hii husisitiza muundo wa ndani wa lugha. Kwa mujibu wake, kipengele kimoja katika matini huwa na maudhui na kinapoungana na sehemu ya kishazi inayosalia,

ujumbe hupatikana. Pia, nadharia hii husisitiza matumizi ya lugha kulingana na muktadha wa kijamii na hutambua msingi wa semantiki tofauti na Sarufi Zalishi iliyojikita katika sintaksia. Lugha huchukuliwa kama mfumo wa maana unaowakilishwa kwa matini za kisarufi na hukua ili kukidhi mahitaji ya binadamu. Katika nadharia hii, kuna uhusiano kati ya matini za kisarufi na maana, kwa hivyo katika muktadha huu, sarufi ya lugha si dhahania. Utafiti huu uliangalia uhusiano huu wa maana katika maudhui yaliyojitokeza katika insha za wanafunzi.

Nadharia ya Isimu Amilifu hutambua kuwa kila lugha ulimwenguni imejengwa kwa maana mbili za kimsingi: maana tambuzi au dhahania na maana husishi. Kwa pamoja, maana hizi hushirikisha kanuni bia za matumizi ya lugha. Kanuni hizi ni kudhibiti mazingira yetu maishani na kutumia akili zetu. Maana tambuzi inasimamia dhati ya ujumbe na maudhui, ilhali maana husishi inatazama kaida za vikwazo jumulifu vya kimawasiliano na kijamii. Hata hivyo, mfumo huu pia unatambua na kudhihirisha aina ya tatu ya maana ambayo ni maana matinishi. Maana matinishi ndiyo huweka maana tambuzi na maana husishi katika muktadha wa lugha na mawasiliano (Sichangi, 2008). Hii ina maana kwamba maana husishi na tambuzi hupata uhalisia kupitia maana matinishi. Kwa ujumla, majukumu msingi ya lugha ni mawili; kujenga mahusiano ya kijamii na kupasha ujumbe.

Mtazamo bayana wa nadharia ya Isimu Amilifu uliotumika katika utafiti huu ni Sarufi Amilifu Mfumo (SAM). SAM ni mtazamo uliojengwa na Halliday iIi

kuchanganua matini za kisarufi. Kwa mujibu wa SAM, kishazi ndicho kipashio msingi cha kisarufi ambacho kinatumika katika kuchanganua matini za kisarufi. Kipashio cha kishazi kimelinganishwa na sentensi sahili. Katika muktadha huu, kishazi hubeba na kuakisi maana zote zinazotambuliwa na SAM. Sarufi Amilifu Mfumo imetambua na kufuma tanzu tatu za sarufi. Tanzu hizi ni sintaksia, semantiki na pragmatiki. Sintaksia inazingatia uhusiano wa maumbo yenyewe; hubainisha mitazamo na hali ya maumbo kama yanavyodhihirika katika matini. Katika sintaksia, aina tatu za kiima zimetambuliwa na kubainishwa; nomino, kivumishi na kihusishi. Kila aina ya kiima husawiri maana tofauti inayosimbwa katika kishazi. Pragmatiki hushughulikia umuhimu wa miingizo ya kiarifa kwa kuzingatia muktadha mpana wa lugha na mawasiliano yaani huchunguza lugha kwa kutegemea maoni ya mtumiaji. Utanzu huu huchunguza hasa vikwazo vya kijamii katika matumizi ya lugha, utambuzi na uchaguzi wa miundo ya maneno anaoufanya mtumiaji na athari za kijamii za matumizi ya lugha.

Kwa upande mwingine, semantiki inashughulikia dhana ya maudhui. Utanzu huu wa semantiki ndio hubainisha maana zinavyofumwa katika kishazi. Maana hizi ni tambuzi, husishi na matinishi. Maana tambuzi huwakilisha uwezo wa msemaji kung'amua mambo. Kitengo hiki cha maana hubeba maudhui na ujumbe katika lugha. Kupitia maana tambuzi, lugha husimba tajriba za kitamaduni na kijamii naye msemaji akisimba tajriba zake binafsi. Mhimili huu ulitumiwa na mtafiti katika kutathmini ung’amuzi wa wanafunzi wa vipengele vya mshikamano na matumizi yavyo katika insha. Kwa hiyo, maana tambuzi humilikiwa kama nyenzo

ya kuelewa na kueleza ujuzi na tajriba kwa jumla. Maana husishi huwakilisha dhima ya lugha ya kuwatangamanisha wanajamii. Pia, humilikiwa na watumiaji wa lugha kama nyenzo ya kufasili na kufasiri wajibu na dhima ya kijamii. Insha za wanafunzi zilifasiriwa kwa msingi huu wa maana husishi.

Aina nyingine ya maana ni matinishi. Maana matinishi inarejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa mawasiliano ya lugha. Hii humilikiwa na msemaji kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha wa lugha. Aidha, insha za wanafunzi zilipimwa kwa kutumia kigezo hiki cha usarufi ili kutathmini jinsi vipengele vya mshikamano vilivyokuza au kulemaza uelewa wa maudhui. Kutokana na maelezo ambayo tayari yametolewa, nadharia hii ilifaa sana utafiti huu.

### 1.8.0 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti zimezingatiwa katika muktadha wa vipengele vifuatavyo; muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, usampulishaji wa data, mbinu za kukusanya data, mbinu za kuchanganua data na mbinu za kuwasilisha data.

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu umechukua muundo wa maelezo na takwimu. Maelezo yalitumiwa katika ufafanuzi wa data kulingana na malengo ya utafiti nao wa takwimu ulitumika katika kutathmini idadi ya wanafunzi wanaokuza na kulemaza mshikamano katika insha zao.

### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Mikondo miwili imetumiwa ambayo ni utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulizingatia usomaji wa vitabu, majarida na makala ya mtandao. Taarifa zilizopatikana kutoka maktabani ni taarifa kuhusu aina mbalimbali za mshikamano na utumikizi wa nadharia za Sarufi Zalishi na Sarufi Amilifu Mfumo. Utafiti wa nyanjani ulihusu utayarishaji wa mbinu za kukusanya data, majaribio ya mbinu husika na ukusanyaji wa data halisi. Data za utafiti zilikuwa insha za wanafunzi wa kidato cha nne kutoka kaunti ya Murang'a.

### 1.8.3 Mbinu za Usampulishaji Data

Utafiti huu umefanyika shuleni. Sampuli husika ilihusu shule na madarasa. Utafiti ulitumia sampuli iliyotokana na makundi mawili kimsingi; sampuli ya kimaeneo na sampuli ya watafitiwa. Shule sita zilichaguliwa kimakusudi kwa kutumia mbinu ya aina ya shule, idadi ya wanafunzi, uchangamano wao na jinsia. Sababu kuu hapa ni kuwa shule husika zina wanafunzi wa viwango tofauti na hili lilisaidia katika kubaini hali ambayo ilijirudia katika insha za wanafunzi licha ya viwango vyao vya ung'amuzi. Shule hizi ni shule za upili za Murang'a, Pioneer, Mugoiri, Njiiri, Kahuhia na Mahutia.

Insha ishirini zilichaguliwa kinasibu kutoka kila kidato cha nne; tano za kiwango cha chini, kumi za kiwango cha katikati na tano za wanafunzi wa kiwango cha juu. Insha hizi zilifaa kwa sababu ziliwakilisha zaidi ya thuluthi moja ya wanafunzi wa kila kidato (Orodho, 2004). Tofauti katika insha hizo zilisaidia

katika kuonyesha viwango vya mshikamano katika viwango vyote. Sampuli yote ilihusisha wanafunzi mia moja na ishirini. Unasibu wa aina hii hutoa nafasi sawa, majibu hupatikana kwa muda mfupi na hupunguza gharama ya usafiri (Orodho, 2004).

### 1.8.4 Vifaa vya Kukusanya Data

Mbinu za kukusanya data zilihusu yafuatayo; uandishi wa insha, hojaji kwa walimu, zoezi wazi, na ukaguzi wa insha zilizotuzwa na walimu. Mbinu zaidi ya moja zikitumika, matokeo ya utafiti huwa bora tofauti na mtafiti anapotumia mbinu moja tu chambilecho Wiersma (1986).

#### 1.8.4.1 Insha

Wanafunzi waliulizwa waandike insha kuhusu mada iliyoamuliwa na mtafiti. Hii insha ilikuwa kamili (maneno mia nne) na iliyoandikwa kwa muda uliopendekezwa na KNEC; insha mbili kwa muda wa saa 1¾. Mtafiti alitathmini uwezo wa wanafunzi wa kutumia vipengele vya mshikamano katika insha zao.

#### 1.8.4.2 Zoezi

Zoezi wazi kuhusu virejeshi, viunganishi, vipengele vya kileksia, udondoshaji na ubadilishaji lilitahiniwa. Wanafunzi waliandaliwa mapema na maagizo ya mtihani

kutolewa kulingana na malengo ya mtafiti. Uandalizi wa aina hii ulisaidia katika kupunguza miktadha itakayoweza kuathiri umilisi wao kwa njia hasi.

#### 1.8.4.3 Hojaji

Mtafiti vile vile alitumia hojaji kwa walimu ili kuchunguza maoni yao kuhusu chanzo cha ukosefu wa mshikamano na jinsi ya kuuboresha katika insha wanazoziandika wanafunzi. (Taz. Kiambatisho iii)

#### 1.8.4.4 Ukaguzi wa Madaftari

Aidha, mtafiti alichunguza insha zilizotuzwa na walimu ili kutathmini ikiwa zilituzwa kulingana na mwongozo wa kudumu wa KNEC na hili lilisaidia katika kubaini uandalizi wa wanafunzi kuhusu tuzo la hatimaye katika mtihani wa kitaifa na kutathmini mazoea yao ya kutumia vipengele vya mshikamano katika insha zao. Hili lilifaa kutimiza lengo la kwanza na la pili katika utafiti huu.

### 1.8.5 Maadili ya Utafiti

Kabla ya utafiti kufanywa, walimu na wanafunzi walielezwa nia na umuhimu wa utafiti. Waliombwa kuhusika kwa hiari. Aidha, walihakikishiwa kuwa data iliyotokana na majibu yao itatumika kwa ajili ya utafiti tu wala si mengineyo. Vilevile, majina ya shule na wahusika yaliwekwa siri. Kuhusiana na maswali yaliyohitaji kujibiwa nao, umakinifu ulifanywa kuhakikisha kwamba maswali husika hayawadhalilishi wahusika. Hatimaye, matokeo ya utafiti yaliwasilishiwa shule mbalimbali zilizohusika.

### 1.8.6 Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi ya mshikamano katika kukuza maudhui katika insha za wanafunzi. Vipengele vya mshikamano vinavyokuza au kulemaza mshikamano vilipangwa katika makundi mbalimbali; urejeshi, udondoshaji, ubadilishaji, uunganishaji na leksia na kisha vikatumiwa katika kupima mshikamano katika insha husika. Mpangilio huu ulifaa kwani kila kipengele kilijitawala na hivyo kuzua utaratibu bora wa uchanganuzi. Katika kufanya hivi, hali inayofanana au kutofautiana katika viwango vyote vya utafiti ilijitokeza wazi.

Data iliyotokana na hojaji pia ilichanganuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Hojaji kwa walimu ilitoa maelezo kuhusu maoni yao kuhusu ubora wa insha za wanafunzi, chanzo cha ukosefu wa mshikamano na njia mwafaka za kuboresha hali hiyo. Majibu yao yalisaidia katika kufanikisha lengo la tatu na nne. Asilimia ya wanafunzi waliokuza au kulemaza mshikamano iliafikiwa kwa njia ifuatayo;

$$X/M$$

X – Idadi ya waliokuza au kulemaza mshikamano

M – Idadi ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti.

### 1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Data zimewasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalifanikiwa kwa kutumia majedwali na takwimu hasa akisami ili kuwasilisha data ya kutegemewa. Majedwali haya yamekuwa ya manufaa katika kuonyesha vipengele mbalimbali

vya mshikamano na vilevile kuonyesha mshabaha na tofauti kati ya viwango husika. Taarifa zifuatazo zilihusishwa mtawalia; Utangulizi, maelezo ya kijumla ya vipengele vya mshikamano, jinsi mshikamano ulivyokuzwa na kulemazwa, chanzo cha ukosefu wa mshikamano, jinsi ya kuboresha hali hiyo na hitimisho. Kutokana na haya basi, ni wazi kwamba utafiti huu kwa kiasi kikubwa ni elezi na ndiposa matokeo yaliwasilishwa kwa maelezo.

# SURA YA PILI

# UKUZAJI WA VIPENGELE VYA MSHIKAMANO

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia kwa ufupi vipengele mbalimbali vya mshikamano na namna vilivyokuzwa katika insha za wanafunzi. Vipengele hivi ni urejeshi, uunganishaji, udondoshaji, ubadilishaji na leksia. Ukuzaji wa vipengele husika katika insha za wanafunzi vilichanganuliwa kwa kutumia mihimili ya utendaji na umilisi ya Sarufi Zalishi na ule wa maana tambuzi wa Sarufi Amilifu Mfumo. Aidha, baadhi ya vipengele kama viunganishi, viashiria na vimilikishi vimeainishwa katika kategoria zao za maneno kwa kutumia nadharia ya Sarufi Zalishi.

## 2.1 Maana ya Mshikamano

Wataalamu wengi wana mawazo tofauti tofauti kuhusu mshikamano. Kwa mujibu wa Labov (1972), mshikamano ni dhima ya kinachosemwa na uhusiano wake na vitendo. Halliday na Hasan (1976) na Beagrande na Dressler (1981)

wanakubaliana kwamba mshikamano hurejelea mahusiano ya maana yaliyopo katika usemi au matini na kuwa ni miongoni mwa vipengele vya sifa za usemi. Hata hivyo, Halliday na Hasan wanasisitiza kuwa mshikamano hutokea wakati ufasiri wa kipashio fulani kwenye usemi unategemea ule wa kingine na huelezwa kupitia sarufi na msamiati. Wataalamu hawa wanauona kama mahusiano ya kimaana ambayo huyapa matini muundo. Kwa upande mwingine, Beagrande na Dressler wanaonyesha kuwa lazima sifa au vipengele vya usemi viwepo ili maandishi yasemekane kuwa usemi. Mbali na mshikamano, kuna uarifu, muwala, ukubalifu, kusudi, hali na mwingiliano matini .

Kwake Tanen (1993), mshikamano ni vijenzi vinavyotumia pamoja mikakati ya kimuundo. Hili linaungwa mkono na Redeker (2000) anaposema kuwa mikakati ya kimuundo hutegemea mawazo yetu ya kiitikadi kuhusu ni nini maana ya matini na kupitia kwa njia gani inaweza kusemekana kuwa na maana. Linalojitokeza ni kuwa, mshikamano huwa kama gundi katika usemi.

Kuna aina mbili kuu za mshikamano; mshikamano wa kisarufi na mshikamano wa kileksia (Njogu, Mwihaki na Buliba, 2006). Mshikamano wa kisarufi unarejelea yaliyomo kisarufi, nao wa kileksia unarejelea lugha iliyotumika katika usemi.

Mshikamano unaweza kujitokeza ama katika sentensi moja au kati ya sentensi mbili tofauti. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya;

*Sentensi 1a)* : John amekula?

*b)* : Ndiyo, amekula.

Sentensi hizi mbili zinazungumzia mhusika mmoja ambaye ni John. Kwa hivyo, zinaonyesha mshikamano kati ya sentensi mbili.

*Sentensi c):* John amekula lakini *yeye* huwa mlafi. Neno 'yeye' linamrejelea John anayezungumziwa katika sehemu ya kwanza. Katika muktadha huu, mshikamano umetokea katika sentensi moja.

*Sentensi d): Mimi* ni mwalimu. *Ni*nafanya juhudi kubwa kuhakikisha *ni*mewaelekeza wanafunzi vilivyo.

Katika mfano wa sentensi ya 1 (d), *ni* katika 'ninafanya' na *mimi v*inarejeleana katika kuonyesha mtenda. Mifano hiyo minne ni ishara kuwa viungo mbalimbali hutumika kama gundi ya kushikilia matini au usemi.

Kuna kategoria tano za vipengele vinavyoleta mshikamano katika tungo (Halliday na Hasan, 1976);

i) Urejeshi/urejeo

ii) Udondoshaji

iii) Ubadilishaji

iv) Uunganishaji

v) Leksia

**2.2 Urejeshi**

Hii ni hali ambapo kipashio kimoja cha kiisimu hupata kueleweka kupitia kipashio kingine kilichotangulia. Kwa hivyo, huu ni uhusiano wa kimaana.

Lyons (1968) anasema kwamba uhusiano kati ya maneno na vitu, unatambulika kama urejeshi. Mzungumzaji ndiye hutumia urejeshi kwa kutumia maneno au misemo inayofaa. Vipengele vinavyoweza kufasirika hivi ni virejeshi vya nafsi, viashiria na vilinganuzi (Halliday na Hasan, 1976). Wanasisitiza kuwa mshikamano katika muktadha huu, huwa pale ambapo kuna mwendelezo wa urejeshi; kuwa kile kinachozungumziwa huingizwa katika usemi kwa mara ya pili. Tanned na Hamilton (2001) wanasema kuwa, uteuzi mwafaka wa urejeshi hulingana na muktadha.

Mshikamano unaweza kupatikana kupitia hali zifuatazo za urejeshi; Urejeshi sabiki/ndani, urejeshi dokezi na urejeshi nje.

### 2.2.1 Urejeshi Sabiki

Urejeshi sabiki ni hali ambapo umbo fulani hutumiwa kurejelea kilichokuwa kimezungumziwa tayari. Urejeshi sabiki hutokea ili kuepuka urudiaji usiofaa. Kwa mfano:

*Sentensi 2:* *Daktari* ni wa maana sana. *Yeye* hutibu maradhi yanayowasumbua watu.

Neno 'yeye' linamrejelea daktari anayezungumziwa katika sentensi ya kwanza. Ifuatayo ni mifano kutoka insha za wanafunzi.

**Jedwali 2.1: Mrejeo Sabiki/ Ndani**

| Sentensi | Vipengele vya mrejeo ndani |
|---|---|

| | |
|---|---|
| i) Simiyu na Somuyi *wa*lizaliwa maskini.<br>ii) Ibilisi *a*liwaangalia kwa jicho la wivu. | wa, a |
| iii) *A*litikisa kichwa *chake* na kuendelea na kazi *yake*. | a, chake na yake |
| iv) Niliamka nikiwa mchovu kama mkongwe ali*ye*lima usiku kucha. | ye |
| v) Wachezaji walijitahidi, *nao* hawakutaka kuachwa nyuma. | nao |

Katika sentensi (i), kiwalikishi ‘wa’ kinawarejelea wahusika Simiyu na Somuyi. Katika (ii), kiwakilishi ‘a’ kinamrejelea ibilisi. Viwakilishi hivyo vimetumika ili kuepuka urudiaji usiofaa wa nomino. Aidha, ‘chake’ na ‘yake’ katika (iii) ni vuvumishi vimilikishi vya nomino inayowakilishwa na kiambishi ‘a’ katika kitenzi ‘alitikisa’. Mwisho, ‘o’ katika ‘nao’ katika sentensi ya (iv), ni kiwalikilishi nafsi kinachorejelea nafsi ya tatu. Wanafunzi wote walitumia mrejeo ndani. Hii ni asilimia 100.

Mshikamano wa kurejelea katika sentensi mbalimbali katika jedwali yamekuza maudhui mbalimbali kwa usaidizi wa mhimili wa maana tambuzi wa SAM. Mhimili huu hutathmini maudhui yanayojitokeza katika kishazi husika. Kwa mfano, katika sentensi ya i), maudhui ya ni nani walizaliwa yanajitokeza (Simiyu

na Somuyi). Aidha, katika sentensi ya iii), mrejeo ndani wa viambishi *a*, *chake* na *yake* unakuza maudhui ya kutikisa kichwa na kumiliki ( kichwa na kazi).

### 2.2.2 Urejeshi Dokezi

Urejeshi dokezi ni muktadha ambapo neno au umbo linatumika kurejelea kitakachotajwa. Kwa mfano:

*Yeye ni mwandishi bingwa wa eneo hili zima. Ameandika vitabu anuai; si vya fasihi, si vya lugha, si vya insha. Leo ni mara yake ya kumi ya kutunukiwa tuzo na sifa sufufu. Aidha, hushiriki katika vikao vingi mno vya kuunda mtaala wa lugha ya Kiswahili*. Si mwingine ila Profesa Akoth.

Sehemu iliyoandikwa kwa italiki inamtambua na kumrejelea mwandishi Akoth. Wanafunzi walidhihirisha mifano ifuatayo;

**Jedwali 2.2: Mrejeo Dokezi**

| Sentensi | Kiambatisho/Mrejeo Dokezi |
|---|---|
| i) Pingu mkononi, askari wakiwafuata, Hasan na Juma walitoa milango ya korti baada ya uamuzi wa mashtaka yao kufanywa. | Kiambatisho P 6 |
| ii) Maisha yao yote waliishi kisiri. Ghafla wakaja kutuambia mipango yao…..Edith na Ali walikuwa marafiki wa dhati. | Edith na Ali wanatambuliwa baadaye |

| | |
|---|---|
| iii) Uuwii! Njooni muwaone washerati. Jibaba nzima kama hili linajaribu kuniibia mke….”mkewe Ali alikuwa alikuwa amekumbatiwa na mzee Mawewa wakijamiana. | Kiambatisho P13 |
| iv) Milango ya kanisa ilifunguliwa. Mlangoni alisimama Bi. arusi huku ameva rinda jeupe pe pe pe….Sela akifunga pingu za maisha. | Kiambatisho P 9 |
| v) Tabasamu lililomvaa Melina lilibadilika na kuwa majonzi. Kumbe Said alikuwa mbwa mwitu. Said alionekana kuwa na wasiwasi siku hiyo. (Chanzo cha hali hizo kinafichuliwa baadaye; Said kuwa na msichana mwingine). | |

Katika sentensi ya (i), wanaotiwa pingu mkononi na kufuatwa na askari wanatambulishwa baadaye kama Hasan na Juma. Katika mfano wa pili, maelezo ya Edith na Ali yanatolewa kwanza kabla ya wao kujulishwa kwetu. Washerati wanakuja kujulikana baadaye kama jibaba na mkewe Ali katika mfano wa tatu. Mwisho, taharuki ya kubadilika kwa hali ya Melina inakuja kufichuliwa mwisho kuwa Said alikuwa na msichana mwingine. Hii yote ni mirejeo dokezi. Wanafunzi 34 kati ya 120 ndio walitumia mrejeo dokezi katika insha zao. Hii ni asilimia 28.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika hapa katika kukuza maudhui ya uasherati, kuishi kisiri, kuitiwa mbaroni na majonzi katika snentensi i)-iv) mtawalio.

### 2.2.3 Urejeshi Nje

Urejeshi nje ni hali ambapo maana itapatikana tu kwa kurejelea muktadha. Urejeshi huu unapotumiwa, huonyesha hali ya kidhahania katika maandishi na kwa sababu hii, msomaji au msikilizaji hutafuta ufasiri wa nje ya matini. Hali hii hutumika sana na watoto wakiwa wanachukulia kuwa wanachorejelea kinaeleweka na kila mtu. Kwa mfano;

**Kielezo 2.1**

Mtoto : Kwa nini kile kinatumiwa hivyo?

Mlezi : Nini hicho?

Mtoto : Hicho hicho.

Mlezi : Hicho hicho nini?

Labda mtoto anaashiria chombo fulani na anatarajia mlezi wake atafasiri ujumbe katika muktadha anaourejelea.

Wanafunzi wanaweza kupewa picha za aina mbalimbali na waambiwe waandike hadithi kutokana na picha walizopewa. Picha hizi ni kama;

Picha 1 - Mwalimu akiwa ameketi sokoni.

Picha 2 - Wachuuzi wakiwa wanauza.

Picha 3 - Mwendawazimu mmoja akimnyang'anya mama mmoja tunda.

Picha 4 - Umati ukimchapa mwendawazimu.

Picha 5 - Mwendawazimu kutorokea kiingilio cha soko.

Hadithi zifuatazo zinaweza kujitokeza;

Hadithi ya kwanza: Mwalimu akiwa ameketi sokoni huku wachuuzi wakiuza, alimwona mwendawazimu akimnyang'anya mama mmoja tunda. Umati ulimchapa huyo mwendawazimu; jambo lilomfanya kutorokea kiingilio cha soko.

Hadithi ya pili: Alipokuwa akiketi sokoni huku wakichuuza, aliona akimnyang'anya mama tunda. Umati ulimchapa; jambo lililompelekea kutorokea kiingilio cha soko.

Hadithi ya kwanza inafasirika bila tatizo ilhali ya pili itafasirika tu ikiwa anayeambiwa anaelewa kuhusu picha zile tano na kwa hivyo afasiri ujumbe kwa kuzitumia. Huu ni urejeshi nje katika muktadha huu. Mfano wa wanafunzi katika Jedwali lifuatalo unadhihirisha hili;

**Jedwali 2.3: Jedwali la Mrejeo Nje**

| Sentensi | Mrejeo nje |
|---|---|

| | |
|---|---|
| Zuhura: Ngang’a, mbona umenifanya hivi?<br>Ng’ang’a: Nilikufanya nini? | ‘Umenifanya hivi’ na ‘nilikufanya nini’ |

Vishazi *umenifanya hivi* na *nilikufanya nini* ni mfano wa mrejeo nje. Hii ni kwa sababu wanaoulizana hivyo wanaelewana kutokana na maana ya wanachorejelea kulingana na muktadha wa mazungumzo yao. Ufasiri wa aina hii ulieleweka kwa kwa kutumia mhimili wa umilisi wa Sarufi Zalishi. Umilisi ni uwezo wa msemaji wa lugha kutunga na kuelewa tungo za lugha yake. Wahusika katika jedwali 2.3 wana ung’amuzi au uelewa wa ‘nini’ katika mazungumzo yao kulingana na muktadha wa mazungumzo japo si wazi kwa asiyeelewa muktadha.

Mrejeo nje haukutumiwa sana na wanafunzi kwani ni asilimia moja tu iliyoutumia. Hata hivyo, mrejeo nje uliotumiwa katika mfano wa jedwali 2.3, unakuza maudhui ya ‘nini’ kumaanisha kitendo alichofanyiwa zuhura.

Mrejeo nje unaonekana kuwa tatizo kwa wanafunzi kwa jumla jinsi walivyogundua Thiga (1997) na Nyarige (2002). Sababu ya hali hii inaweza kuwa ukosefu wa kusoma kwa mapana na aina ya insha. Kwa mfano, insha kama ya maelekezo inafaa iwe wazi na mrejeo nje usiwe au uwe mchache.

Kama ilivyodokezwa awali, urejeshi hufasirika kupitia urejeshi nafsi, viashiria na vilinganuzi. Katika kufanya hivyo, mshikamano kupitia kwa vipengele hivi hukuza maudhui ya mtendaji/ kiima, umbali wa nomino na tofauti miongoni mwa

aina za maneno. Yanayofuata ni maelezo mafupi kuvihusu vipengele hivyo na namna vilivyojitokeza katika insha za wanafunzi.

### 2.2.4 Urejeshi Nafsi

Urejeshi nafsi hurejelea nafsi tatu umoja na wingi. Halliday na Hasan (1976) wanasema kwamba nafsi hizi tatu hufanya kazi na vimilikishi. Jedwali 2.4 lifuatalo linadhihirisha hayo:

**Jedwali 2.4: Virejeshi vya nafsi na vimilikishi vyake**

| Nafsi | Neno (Umoja) | Kiambishi (Umoja) | Kimilikishi (Umoja) | Neno (Wingi) | Kiambishi (Wingi) | Kimilikishi (Wingi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mimi | Ni | -angu | sisi | tu | -etu |
| 2 | Wewe | U | -ako | ninyi | m | -enu |
| 3 | Yeye | A | -ake | wao | wa | -ao |

**Asili: Halliday na Hasan (1976) uk.38**

Tungo za wanafunzi zilikuwa na mifano ifuatayo;

**Jedwali 2.5: Nafsi na Vimilikishi**

| Nafsi | Sentensi | Vipengele-nafsi, umilikishi |
|---|---|---|
| 1 | Nakusihi u*ni*ombee *mimi* na marafiki *zangu*.” | *ni, mimi, zangu, u* |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Tuli*m*shukuru Mungu. | *m, Mungu* |
| 3 | Mama *a*liposikia vile, *a*kajaribu ku*m*pigia Abdi simu kwa kuwa *yeye* na marafiki *zake wa*likuwa huko. | *a, wa, yeye, zake, m* |

Urejeshi nafsi hurejelea nafsi tatu umoja na wingi. Urejeshi nafsi hufanya kazi na vimilikishi. Kuna uhusiano wa kurejeleana kati ya *ni, mimi* na *zangu* katika sentensi ya kwanza. Katika sentensi ya pili, kiambishi *m* kinamrejelea Mungu navyo *a, wa, yeye, zake* na *m* vina uhusiano wa kurejelea Abdi**.**

Ilibainika kutoka insha za wanafunzi kuwa nafsi ya tatu ndiyo ilichukua nafasi kubwa katika matumizi. Wanafunzi wote mia moja na ishirini walitumia nafsi ya tatu, thelathini na tisa nafsi ya pili na sitini na saba nafsi ya kwanza. Nafsi ya kwanza ilichukua asilimia 55.8, ya pili asilimia 32.5 na ya tatu asilimia 100. Hali hii huenda ilichangiwa na kidokezo walichopewa wanafunzi. Nafsi katika kidokezo ilikuwa ya tatu. Hii inamaanisha kuwa mshikamano katika muktadha wa nafsi uliimarishwa nao.

Mwanafunzi anapokosa kung'amua viwakilishi vya nafsi na viambata vinavyotumika pamoja navyo yaani 'ni', 'tu', 'u', 'm', 'a' na 'wa', mshikamano wa kurejelea mtenda, mtendwa na mtendewa huathiriwa pakubwa. Aidha, maana katika kishazi huweza kuwa na utata au potoshi.

### 2.2.5 Urejeshi wa Kuashiria

Urejeshi wa kuashiria huonyesha umbali wa kile kinachorejelewa na nomino; karibu, mbali kidogo na mbali mno. Viashiria hivi hutegemea ngeli (Mogambi, 2007). Jedwali 2.6 lifuatalo linadhihirisha hili.

**Jedwali 2.6: Jedwali la Viashiria**

| Nomino (Umoja) | Karibu | Mbali Kidogo/kati | Mbali Mno | Nomino (Wingi) | Karibu | Mbali Kidogo | Mbali Mno |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mbuzi (a) | Huyu | huyo | yule | Mbuzi wa) | hawa | hao | yule |
| Mfuko (u) | Huu | Huo | ule | Mifuko (i) | hii | hiyo | ile |
| Kitabu (ki) | Hiki | hicho | kile | Vitabu (vi) | hivi | hivyo | kile |
| Ndoo (i) | Hii | hiyo | Ile | Ndoo (zi) | Hizi | hizo | zile |
| Jibu (li) | Hili | hilo | Ile | Majibu (ya) | haya | hayo | yale |
| Ukuta (u) | Huu | huo | ule | kuta (zi) | hizi | hizo | zile |
| Maziwa (ya) | Haya | hayo | yale | Maziwa (ya) | haya | hayo | yale |
| Kucheza (ku) | Huku | huko | kule | Kucheza (ku) | huku | huko | yule |
| Pahali (PO) | Hapa | hapo | pale | Pahali (pa) | hapa | hapo | pale |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahali (KO) | Huku | huko | kule | Mahali (ku) | huku | huko | kule |
| Mahali (MO) | Humu | humo | mle | Mahali (mu) | humu | humo | mle |

Kwa mujibu wa Kariuki (2012) na Ombuna (2014), viashiria, vimilikishi na viwakilishi katika Sarufi Zalishi huainishwa katika kategoria ya vibainishi pamoja na pronomino, viswahilishi na viratibishi. Kulingana nao, vibainishi ni maneno ambayo hutumika badala ya nomino au kuelezea mahali ambapo nomino husika ipo.

Kwa jumla, maneno ambayo yalikuwa yakiainishwa kama vivumishi vya pekee, vivumishi vya idadi, vivumishi vimilikishi, vivumishi vionyeshi na viwakilishi nafsi katika Sarufi Mapokeo ndiyo yanaainishwa kama vibainishi katika Sarufi Zalishi. Jedwali lifuatalo linaonyesha aina za vibainishi.

**Jedwali 2.7: Jedwali la Vibainishi**

| Kategoria | Sifa za kategoria | Mifano |
|---|---|---|
| Vibainishi vya pronomino | Viwakilishi nafsi | Mimi, wewe na yeye- nafsi umoja.<br>Sisi, nyinyi na wao- nafsi wingi. |
| Vibainishi vimilikishi | Huonyesha umilikaji | -angu, -ako na ake |

| | | |
|---|---|---|
| | | (umoja)<br>-etu, -enu na –ao (wingi) |
| Vibainishi<br>vya Idadi | Hubainisha idadi dhahiri au isiyo dhahiri ya nomino. | -chache, -ingi, tele ( idadi isiyo dhahiri), tatu na moja, ishirini (dhahiri). |
| Vibainishi Vionyeshi | Hubainisha umbali wa nomino; karibu, mbali kidogo na mbali mno. | Hiki (karibu) kile (mbali mno) na hicho (wastani/kati) |
| Vibainishi Jumlishi | Huashiria nomino kijumla; Vivumishi vya pekee –ote na –o-o-te | lolote, chochote, kote |
| Vibainishi rejeleshi | Hudokeza dhana za -enye, -enyewe na -ingine. | Chenyewe, mwingine nyingine, chenye |

Asili: ukadiriaji wa Mtafiti

Utafiti huu umetumia vibainishi vya pronomino, vibainishi vimilikishi na vibainishi viashiria na vilijitokeza katika insha za wanafunzi kama inavyodhirika katika Jedwali 2.8;

**Jedwali 2.8: Viashiria/Vishamirishi**

| Sentensi | Kiashiria |
|---|---|
| Melina alikuwa mhusika mkuu wa siku *hiyo* (Kati) | huyo |

| | |
|---|---|
| Kidosho *huyo* aliamua kuavya mimba maana hakuwa na uwezo wa kumlea mwanawe (kati). | huyo |
| Melina alikuwa na uchungu aliposikia maneno *haya* na akakomesha usahibu wao (karibu). | haya |
| Kijana mmoja aliyempenda alimtendea unyama katika chumba *kile* (mbali mno). | kile |

Viashiria *huyo, haya na kile* ni vya mbali kidogo, karibu na mbali mno mtawalia. Viashiria hivi vya karibu, mbali kidogo na mbali mno vilitumika ifuatavyo; Wanafunzi waliotumia viashiria vya karibu walikuwa sitini na wanane ambayo ni asilima 57, vya kati themanini na watatu ambayo ni asilimia 69 na na vya mbali mno hamsini na wanane ambayo ni asilimia 48.

Viashiria vya kati au wastani vilitumika zaidi ya vya karibu na mbali mno. Hali hii ilijitokeza hasa katika wanafunzi waliokuza mshikamano kati ya maudhui waliyodhihirisha katika insha zao, na kimalizio cha insha walichopewa katika zoezi la insha.

### 2.2.6 Urejeshi Linganuzi

Urejeshi linganuzi huonyesha ulinganifu wa wizani au ubora kupitia kwa vielezi na vivumishi; huonyesha kufanana au kutofafana kwa vipengele husika. Vivumishi hufanya kazi katika kikundi nomino kuonyesha wizani au ubora.

Maneno kama *kama, tofauti na, kuliko, zaidi ya* na *–ingine* hutumika. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya;

*Sentensi 3(a):* Nilikuwa natarajia mtu *tofauti.*

*(b):* Ungependa viti *vingine?*

*(c):* Wageni hula chakula *sawa* kila siku.

*(d):* Wanafunzi walitoa majibu *sawa.*

*(e):* Sikufikiria alikuwa mkorofi *hivyo*- labda alidang'anya.

Jedwali lifuatalo linaonyesha namna wanafunzi walivyovitumia vilinganuzi katika insha zao.

**Jedwali 2.9: Vilinganuzi**

| Sentensi | Kilinganuzi |
|---|---|
| i) Bibi arusi aliingia. Alivaa nguo nyeupe *kama* theluji. | kama |
| ii) Mzee Mawewa alitangulia kutoka kitandani huku akitetemeka *mithili* ya kifaranga aliyenyeshewa. | mithili |
| iii)Tunda alifurahi na kuagiza wenzake waendelee kutoa taka katika maeneo *mengine.* | mengine |
| iii) Kuuliza si ujinga, ungewaona wanafunzi waliovalia rangi *tofauti* na sare. | tofauti |
| iv) Waliona heri kuvunjika miguu na mikono *kuliko* kuchomeka na moto huo. | kuliko |
| v) Madai mengi yalitokea kuhusu mwelekeo wa sudi kama *ilivyo* kawaida. | ilivyo |

Vilinganuzi katika matini huonyesha ulinganifu wa wizani au ubora kupitia kwa vielezi na vivumishi; kufanana au kutofanana kwa vipengele husika. Vilinganuzi vinaweza kuonyesha ama mrejeo nje au ndani katika matumizi yake. Mifano iliyotolewa inaonyesha mrejeo sabiki na nje. Mfano wa i) unalinganisha nguo na theluji, wa ii) nao unalinganisha kutetemeka kwa mzee Mawewa na kutetemeka kwa kifaranga. Mfano wa iii) unadhihirisha tofauti za sare zilizovaliwa na wanafunzi. Hii ni mifano ya mrejeo sabiki lakini mfano wa v), unaonyesha mrejeo nje kwa sababu kishazi *kama ilivyo* kitafasirika tu ikiwa anayeambiwa anaelewa hiyo *kawaida* ya mambo.

Wanafunzi 66 kati ya 120 walitumia vilinganuzi katika kazi yao. Hii ni asilimia 55 katika jumla za wanafunzi. Asilimia 34 haikuvitumia. Hata hivyo, vilivyotumika sana ni vya mzizi –ngine. Sababu hapa ni kuwa mzizi huu huwa na dhana nyingi chambilecho Mogambi (2007). Dhana hizi ni: tofauti na, kando na, mbali na, zaidi ya na baadhi ya.

## 2.3 Mshikamano wa Kuunganisha

Viunganishi ni maneno yanayounga maneno, vifungu vya maneno au sentensi (Waihiga na Wamitila, 2004). Mawazo haya yanaungwa mkono na Matei (2008). Hata hivyo, Matei anaongeza kuwa hata kiambishi kinaweza kuwa kiunganishi. Katika nadharia ya Sarufi Zalishi, viunganishi huainishwa katika kategoria ya

maneno ya vishamirishi. Kishamirishi ni kategoria inayoungana na kiima ili kukikamilisha kwa kutoa taarifa zenye uhusiano na kiarifu (Kariuki, 2012).

Vipengele vya kuunganisha havifanyi kazi ya kushikamanisha vikiwa vimetumika peke yao ila hufanya hivyo kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika kufanya hivi, huonyesha uwepo wa vipengele vingine katika usemi ( Halliday na Hasan, 1976). Katika muktadha huu, mshikamano wa kuunganisha hukuza maudhui kutegemea aina na jukumu la vipengele vilivyotumika.

Viunganishi vikitumika vizuri, husaidia katika kujenga na hatimaye kuimarisha mshikamano. Aidha, hutumiwa katika matini kama kitambulishi cha hadhi ya vishazi (Halliday, 1994).

Hata hivyo, baadhi ya viunganishi vingine huonyesha mshikamano kutegemea ni jinsi gani vilitumika. Kwa mfano, 'na' huweza kutumika ama kama kipengele cha muundo au kama kipengele cha mshikamano. Kiambishi 'na' kinapotumika kama kiunganishi cha kuongeza, hufanya kazi ya kuimarisha mshikamano katika matini lakini vinginevyo ni kama kipengele cha kimuundo. Mfano wake kama kipengele cha kimuundo ni;

A-*na*-som-a- Kiambishi/ mofimu ya wakati uliopo

Yafuatayo ni matumizi yake kuonyesha mshikamano:

“Mtoto alilia kwa sauti,” alisema mama. “*Na* alipomaliza kulia aliinua kichwa *na* kumwomba mwalimu wake msamaha.” Katika muktadha huu, mtoto alilia na kuinua kichwa ili kuomba mwalimu msamaha.

*Sentensi 4:* Baba na mama wanasoma.

‘*Na’* inaweza kutumika na matumizi yake kama kipengele cha mshikamano na kimuundo yakaribiane. Hili hutokea pale inapoonyesha kinachofuata katika mfululizo; Pia, huunganisha mkururo wa maswali yanayoelekeza kuhusu kinachofuata.

**Kielelezo 2.2**

Mtoto aliuliza, “Nyumba ni nini?”

“Sawa, nyumba ni mjengo *na* mjengo huo hujengwa kwa kutumia mawe.” Mama alieleza.

“ Lazima mawe hayo yawe mengi?”

“Naam.” Alisema mama, “Pia lazima yawe ya kupendeza.*”*

*“Na* kuna zingine zinaezekwa kwa nyasi au vigae?

“Zile za nyasi ni za kitambo *na* si nyingi *na* watu wengine pia huamua kutumia vigae. Hapa ‘*na*’ inaunganisha maswali na hoja au mawazo yanayoashiria kitu kimoja ambacho ni nyumba.”

Kuna aina tano za viunganishi (Matei, 2008);

**i) Viunganishi vya Kinyume**

Viunganishi vya kinyume hudokeza maana kinyume na matarajio. Kwa mfano, lakini, ingawa, hata hivyo, badala ya, ijapokuwa, miongoni mwa vingine.

**ii) Viunganishi vya Wakati**

Viunganishi vya wakati huunganisha mafungu ya maneno kwa kuonyesha jinsi yanavyofuatana kiwakati. Kwa mfano, halafu, kisha, muda si mrefu, mwishowe, kwanza na kadhalika.

**iii) Viunganishi vya Uteuzi**

Viunganishi vya uteuzi huonyesha hali kuwa kitendo kimoja tu ndicho kinafanywa kwa wakati mmoja; si mawili kwa wakati mmoja. Pia, huleta dhana kuwa, hakuna jambo linaloendelea kufanywa. Kwa mfano, ‘ au’ na ‘ama’ na ‘wala’.

**iv) Viunganishi Visababishi**

Viunganishi visababishi huonyesha uhusiano kati ya kitu na kingine au mtu mwingine. Kwa mfano, kwa sababu, hivyo, kutokana na, madhali, maadamu na kadhalika.

**v) Viunganishi Viongezi**

Viunganishi viongezi hudokeza ongezeko la kitu au idadi. Kwa mfano, na, tena, pia, na kadhalika.

Mbali na makundi haya makuu kuna viunganishi vingine ambavyo Halliday na Hasan (1976) wanaviita viunganishi viendelezo. Hivi huendeleza usemi. Baadhi yavyo, huonyesha uhusiano wa nje na vingine wa ndani. Kwa mfano, Sasa, sawa, vyovyote vile, kwa kweli, na kwa yote. Viunganishi vitumika namna ifuatavyo;

**Jedwali 2.10: Viunganishi**


| Viunganishi | Sentensi | Kiunganishi |
|---|---|---|
| Vya kinyume | Walijawa na furaha ya kibogoyo aliyeota meno *lakini* hawakujua yayo hayo meno yangeng'oka. | Lakini |
| Vya wakati | *Baada ya* kulia na kuumia sana, alifurahi kwa kuepuka mtego huo. | baada ya |
| Vya uteuzi | Alionekana amelewa chakari; asiyeona mbele *wala* nyuma, asijue la kufanya *au* la kutendewa. | wala, au |
| Visababishi | Melin waliokuwa wakwassi wakakubali kumpa msichana aliyetengwa na Said usaidizi kama njia ya shukrani kwa kumwokoa mwanao Melina *kutokana na* Said ambaye angemtumia vile vile. | kutokana na |
| Viongezi | Simiyu *na* Somiyu walizaliwa.<br>Walikuwa chanda *na* pete. | Na |

| | | |
|---|---|---|
| Viendelezo | *Kwa kweli*, sikujua mwanamume yule alikuwa mwalimu. | kwa kweli |

Ilibainika kutoka insha za wanafunzi kuwa asilimia 100 ilitumia viunganishi vya kuongeza, vya wakati asilimia 72.5, visababishi asilimia 55, vya uteuzi asilimia 20, vinyume asilimia 53.3 na viendelezo asilimia 39.2. Hili linaonyesha kuwa wanafunzi hawana uzoefu wa kutumia viunganishi vya uteuzi. Idadi ya waliotumia viongezi ni 120, vya kinyume 64, visababishi 59, uteuzi 28 na viendelezo wanafunzi 47.

Asilimia hizi zinaonyesha wazi kutozoea kwa wanafunzi kutumia viunganishi vya uteuzi na viendelezo. Hili ni jambo ambalo linastahili kutafutiwa suluhu hasa mbinu mwafaka kutumiwa ili kufanikisha matumizi haya miongoni mwao. Asilimia ya matumizi ya viiunganishi imedhihirishwa pia katika chati ifuatayo;

**Chati 2.1: Ukuzaji wa Mshikamano wa Kuunganisha**




## 2.4 Mshikamano wa Kileksia

Mshikamano wa kileksia huchangia muundo wa usemi. Kulingana na Martin (1992), mshikamano wa kileksia ni uhusiano wa leksimu katika usemi na kwa hivyo mshikamano wa kileksia huonyesha taarifa ya jinsi leksimu zimepangwa katika usemi. Mshikamano hutofautiana kulingana na aina ya usemi (Thompson, 1994, na Tanskanen, 2006).

Mshikamano wa kileksia hupatikana kupitia kwa nomino za kawaida, urudiaji na uhusiano-leksika (Halliday na Hasan, 1976).

### 2.4.1 Kategoria za Leksimu

Morris na Hirst (2004) na Halliday na Hasan (1976) wanakubaliana kuhusu aina kuu za leksimu ambazo ni uradidi na uhusiano leksia. Hata hivyo, Morris na Hirst (2004) wanaongeza kategoria ya mfumo maana. Haya yanadhihirishwa kama ifuatavyo;

i) Urudiaji ambao ni hali ya kurudia neno lile lile katika matini. (Hasan 1976, na Tanskanen 2006).

ii) Mfumo maana kama vile homonimu, meronomia, sinonimia, antonimia na hiponimu.

iii) Iso mfumo maana kama vile uhusiano- leksika.

### 2.4.2 Nomino za Kawaida

Hizi ni nomino zinazojumulisha nomino za mahali, binadamu na mawazo/kauli. Nomino hizi husisitiza ujumbe kwa kutokea kwa mara ya pili katika matini na kwa njia hii husaidia katika kuleta mshikamano. Kwa mfano;

*Sentensi 5 (a):* Umewahi kufika *Marekani*? Mimi mwenyewe sijafika *hapo.*

*(b):* *Kevin* alipatikana na kosa la matumizi mabaya ya mamalaka. *Mhusika* huyo jamani ataadhibiwa!

*(c):* Rais anaamini kuwa *ruwaza ya 2030 itaafikiwa* lakini baadhi ya wabunge hawakubaliani na *wazo hilo*.

Mifano 5 a) – c) inahusu nomino za kawaida; mahali, binadamu na wazo mtawalia.

Mshikamano kupitia kwa nomino za kawaida hufanikishwa kwa kutumia kiashiria kinachoakisi leksimu husika kama ilivyo katika mifano*; hapo*, *huyo* na *hilo* hapo juu.

Katika kutimiza jukumu lake la kushikamanisha, nomino za kawaida pia hutumika pamoja na hisia kuzaji; neno linalodokeza kuhusu hisia. Kwa mfano;

*Sentensi 6: John* amekuwa akionywa sana na mkubwa wake kuhusu uwajibikaji wake. *Mjinga* huyo hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Neno ‘mjinga’ hapa lina maana ya kutozingatia maonyo na linahusishwa na John.

### 2.4.3 Urudiaji

Huu ni urudiaji wa leksimu ile ile katika usemi, matumizi ya leksimu ya kijumla inayorejelea leksimu husika, matumizi ya sinonimu au leksimu kuzaji (Halliday na Hasan, 1976). Kwa mfano,

*Sentensi 7(a):* Kifo cha *Mama* Lucy Kibaki kilishtua *wengi*. *Mama* alikuwa kielelezo kwa *wengi* (urudiaji).

*(b)*: Wanaraga walipewa *kikombe* kwa ushindi wao mkuu. Walimkabidhi *rais kikombe* hicho katika ikulu ya *rais* (urudiaji).

*(c):* *Zawadi* kwa waliotia fora katika mtihani wa kidato cha nne zitatolewa hivi karibuni. *Tuzo* hizo hutolewa kila mwaka (sinonimu).

*(d)*: Bi Moraa alijenga *nyumba* nzuri ajabu. *Kasri* hilo lina vyumba ishirini na vitano (leksimu kuzaji).

#### 2.4.3.1 Sinonimu

Kulingana na Njogu, Mwihaki na Buliba (2006), sinonimu ni maneno tofauti ya kifonolojia yenye maana sawa au inayofanana sana. Hata hivyo, wanakubaliana na Ullman (1972) kuwa ni vigumu kupata sinonimu kamili; ni maneno machache sana yana usinonimia hivi kwamba yanaweza kutumika badala ya jingine katika muktadha wowote bila kubadili maana kusudiwa.

Habwe na Karanja (2004) wanasema kwamba huu ni uhusiano mwimo ambao huletwa na hali kama ukopaji wa msamiati, jinsia, dini, tofauti za kimaeneo, tofauti za kilahaja, taaluma, wakati, miongoni mwa mengine. Mifano ya sinonimu ni kama sahibu na rafiki.

Katika kufafanua uhusiano huu, Lyons (1968) anatumia fomula ya sentensi mbili S1 na S2. Sentensi hizi zinakuwa tofauti kwa neno moja ambapo X inabadilishwa na Y, kumaanisha kwamba ikiwa S1 na S2 zina usawa wa maana basi X na Y ni sinonimu katika muktadha huo. Kielelezo kifuatacho kinadhihirisha haya:

**Kielelezo 2.3: Sinonimu**

Mfano: S1 ⟶ Mama alimpa mwanawe *mawaidha*

S2 ⟶ Mama alimpa mwanawe *wosia*

Kwa mujibu wa Lyons (1968) sinonimu zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo viwili ambavyo ni ukamilifu na ujumlifu. Sinonimu kamilifu ni zile ambazo hurejelea fahiwa za kiutambuzi na kihisia. Sinonimu jumlifu hurejelea

sinonimu zilizo au zisizo kamilifu lakini zinaweza kubadilishana nafasi katika muktadha wowote.

**Sinonimu Kamilifu na Jumlifu.**

Sinonimu kamilifu na jumlifu hubadilishana nafasi katika miktadha yote na pia huzua athari sawa za kiutambuzi na kihisia wa watumiaji. Kwa mfano, mtoto na mwana.

**Sinonimu Kamilifu ziso Jumlifu**

Sinonimu hizi huzua athari zinazolingana ambazo ni za kiutambuzi na kihisia lakini haziwezi kubadilishana nafasi katika miktadha yote. Kwa mfano, kuzaa na kujifungua.

**Sinonimu Jumlifu ziso Kamilifu**

Hizi ni sinonimu ambazo hubadilishana nafasi katika miktadha yote, japo hazizui athari za kiutambuzi na kihisia zinapotamkwa. Kwa mfano, katili na mbaya.

**Sinonimu ziso Kamilifu wala Jumlifu**

Sinonimu hizi huweza kutumiwa kama vibadala katika muktadha fulani tu wala si miktadha yote na pia huzua athari za hisia za kitambuzi zinazotofautiana kwa mfano, kiongozi na mtawala.

Sinonimu huchangia katika kuleta mshikamano katika usemi pale neno linaloweza kutumika badala ya lingine, hutumika kulitilia mkazo.

### 2.4.3.2 Homonimu

Palmer (1981) anasema kwamba, homonimu ni maneno ambayo hufanana katika maumbo yake lakini yana maana tofauti. Hapa, umbo moja la neno linaweza kubainisha maana mbalimbali. Homonimu huwa ni maneno ambayo huandikwa sawa, hutamkwa sawa lakini maana ni tofauti. Uhusiano kati ya maneno husika huitwa homonomia. Habwe na Karanja (2004) wanaona homonimia kama uhusiano wa kileksia; uhusiano ambapo maneno yamefanana katika maumbo yake lakini yana maana tofauti. Kufanana huko ni kwa kisadfa tu kwani maneno haya huwa tofauti.

Homonimu ni maana mbili tofauti kabisa lakini zinawakilishwa na umbo moja (Njogu, Mwihaki na Buliba) Wanatofautisha homonimu zifuatazo;

i) Leksimu za jopo moja la kisintaksia, na zenye hijai moja kama vile

*Vua*: samaki

*Vua*: Nguo

ii) Leksimu za jopo tofauti, lakini hijai moja. Kwa mfano,

*Paa:* mnyama

*Paa:* kwenda juu.

Katika kamusi, maneno haya huingizwa kama vidahizo tofauti. Hii ina maana kuwa kila homonimu huwa ni leksia na huwa na mnyambuliko wake na kule

kufanana kwake katika maumbo ni wa kisadfa tu. Hii inamaanisha kuwa maneno haya yasipotumika vyema kutegemea muktadha, utata bila shaka utatokea na utata huu utaathiri mshikamano na uelewa kwa jumla. Utata hutokea kama neno au sentensi ina maana zaidi ya moja (Kempson, 1977).

Mshikamano kupitia kwa matumizi ya homonimu mbalimbali hutokea kutegemea muktadha wa mazungumzo. Kwa hivyo, ufasiri wa maana nje ya muktadha hulemaza uelewa wa maudhui katika usemi.

#### 2.4.3.3 Antonimu

Antonimu ni maneno ambayo maana yake ni ya kinyume. Njogu, Mwihaki na Buliba (2006) wanaainisha antonimu katika makundi yafuatayo;

**a) Antonimu za Kawaida**

Huu ni uhusiano baina ya maneno hivi kwamba kukubali hali moja ni kukataa nyingine. Kwa mfano kufa na kuishi.

**b) Antonimu za Vidato**

Huu ni uhusiano baina ya vinyume ambapo kukubali neno moja hakuna maana inayoafiki kinyume chake. Kwa mfano, *Kasi/pole*, *karibu/mbali*. Uhusiano huu hupatikana kwenye vivumishi na una sifa zake. Sifa hizi ni kama zifuatazo;

a) Uwepo kwa maneno ya kati kwa mfano vuguvugu kati ya baridi na joto.

b) Uwepo wa uhusiano wa kulinganisha kama katika –nene na –embamba.

c) Kuwepo katika jozi na neno la kimsingi zaidi kuliko jingine kwa mfano, *urefu/ufupi*. Kawaida, watu huuliza kitu kina urefu gani na si ufupi gani.

**iii) Antonimu za Vipinduzi**

Katika uhusiano huu, neno moja huelezea mwendo kuelekea upande mmoja na jingine huelezea mwendo kuelekea upande wa kinyume. Kwa mfano, *sukuma/vuta, jenga/jengua na suka/sukua.*

**iv) Antonimu za Tofauti Mkabala**

Hizi huelezea uhusiano baina ya hali zinazodokeza mikabala tofauti kwa mfano, *mwajiri/mwajiriwa.*

Antonimu kwa jumla husaidia kuleta mshikamano katika usemi zinapohusishwa na kiimbo hasa kiimbo cha panda-shuka. Katika muktadha huu, maudhui katika hali ya kiimbo cha “panda’ huwa kinyume na yale yanayojitokeza katika sehemu ya usemi ya hali ya kiimbo cha ‘shuka’.

### 2.4.3.4 Hiponimu

Hiponimu ni maneno yanayoingiza maana ya neno la kijumla kwa mfano, msichana, mvulana, mwanamke na mwanamume ni hiponimu za binadamu.

Mshikamano ni kama gundi katika usemi. Kwa hivyo, Hiponimu huwa kama gundi pale neno moja hutumiwa kusisitizia maneno mengi.

#### 2.4.3.5 Meronimu

Meronimu huonyesha uhusiano kati ya sehemu na dhana ya ‘nzima’ baina ya maneno. Njogu, Mwihaki na Buliba (2006) wanaieleza kama A ikiwa sehemu ya B na B kuwa na A. Kwa mfano, kucha, vidole, kiganja na kisigino ni meronimu ya mkono.

#### 2.4.3.6 Uhusiano-leksika

Uhusiano-leksika ni uhusiano wa kimfumo kati ya jozi za leksimu; uhusiano ambao Lyons (1968) anauita uhusiano saidizi kama ule wa unyume kama katika ‘simama’ na ‘keti’. Huwa ni uhusiano kati ya leksimu ambazo hutambulika pamoja katika maana zao za kileksimu. Sura mbalimbali hapa ni sinonimu, antonimu, majina ya kiuvuli na majina yanayotokana na ruwaza fulani. Kwa mfano;

*Sentensi 8 a):* Yeye hucheza *mpira wa vikapu*. *Mchezo* huo husifika sana shuleni (kiuvuli).

*b):* Alimpa *sarafu kumi* siku ya *Jumatatu* na *Ijumaa*, akampa *noti ya elfu moja* (Ruwaza- Jumatatu na Ijumaa, sarafu na noti). Mifano leksika.

### 2.4.4 Ruwaza za Mshikamano wa Kileksia

Ruwaza ni mpangilio maalumu wa jambo (TUKI 2004). Ruwaza za kileksia hujitokeza ama kama mkufu ama wavu. Kwa sababu leksimu hizi huhusiana katika kuleta uhusiano wa kimaana, basi huunda wavu; zile nomino ambazo hurejelea zingine katika usemi huunda mkufu wa urejeleaji. Hata hivyo, utanzu wa usemi husika ndio huamua kama ruwaza ya mshikamano wa kileksia ni ama mkufu au wavu (Berzlanovich, Egg na Redeker 2008).

Halliday (1984) anadokeza kwamba muundo wa mshikamano katika usemi huangaliwa vyema kwa kuzingatia mshikamano wa kiukufu na utendakazi wao katika usemi husika. Katika kuendeleza wazo hili, anapendekeza kuwepo kwa aina mbili za tofauti wazi kati ya aina mbili za mshikamano wa kileksia ukufu. Hizi ni; mkufu sawia unaohusiana na urejeshi na mkufu kifani unaohusiana na maana iliyo nje ya matini.

Kwa jumla aina moja ya leksimu za mshikamanao huhusiana na aina nyingineyo na kuunda wavu. Nomino moja inaporejelea nyingine katika usemi, huunda mkufu wa kurejelea. Kwa mfano,

**Kielezo 1.4: Ruwaza za kileksia**

*Wanafunzi* hufanya *mitihani* yao kila muhula. *Wanafunzi* hawa wanapotahiniwa, huonyesha umilisi wao kwa jinsi ambavyo wanaishughulikia *mijarabu* husika. Wao hutuzwa kwa *alama* bora. Hizi *alama* ndizo huwawezesha kufuzu na kufanya vyema katika maisha, jambo linalowafanya kuwa waja wema.

Mkufu1: Wanafunzi, alama.

Mkufi 2: Mtihani, mjarabu.

Wavu : Urudiaji na sinonimia.

Wanafunzi walionyesha mifano ifuatayo ya mshikamano wa kileksia katika insha zao:

**Jedwali 2.11: Mshikamano wa Kileksia**

| Sentensi | Vipengele vya kileksia |
|---|---|
| i) Alifaulu na kuitwa *shul*e ya upili maarufu sana. *Huko* alifanya bidii. | Mahali |
| *ii) Bwana Thifa* na familia yake walikuwa miongoni mwa walalasifu ambao hawakubahatika. *Bwana Thifa* a*lifanya* kazi ya kijungujiko. | Urudiaji |
| iii) Ali alimwomba ashirikiane naye katika biashara ya kuuza dawa za kulevya. Juma alimpigia simu na kumwarifu kuwa alikubaliana na *pendekezo lake.* | Nomino za kawaida –Wazo |
| iv) Walijikaza na kupasi kwani walikuwa *nyembe* masomoni. | Hisia kuzaji/ nomino kuzaji. |
| v) Katika harakati za *kufunga* na *kufungua.* | Antonimu |
| vi) Mamake alijawa na *hofu* na *wasiwasi* | Sinonimu |

| | |
|---|---|
| *vii) Mandhari* ilikuwa safi sana na *maua* yaliyokuwa yanametameta yalitoa harufu iliyonukia zaidi. | Hiponimu |
| viii) Kiuno chake kilikuwa cha nyigu, pua lake la upanga, meno yake meupe, na miguu yake ya cherehani. | Uhusiano-leksika |

Mshikamano wa kileksia huonyesha taarifa ya jinsi leksimu zimepangwa katika usemi. Mshikamano wa kileksia ulichanganuliwa kwa kutumia vipengele vifuatavyo; urudiaji (nomino za kawaida, wazo, mahali na hisia kuzaji) mfumo-maana (sinonimu, antonimu, hiponimu) na uhusiano leksika.

Nomino *shule* na kiashiria *huko* vina uhusiano wa kurejeleana. Aidha, nomino *nyembe* ina maana ya kimatlaba inayoashiria werevu. Sinonimu na antonimu husika zimetumika kusisitiza nomino na kitenzi husika na kwa njia hiyo kushikamanisha usemi. Sentensi ya wanafunzi ya ii) katika jedwali 3.10 inaonyesha *bwana Thifa* likiwa limerudiwa. Urudiaji ukitumika vizuri, husisitiza na kuthibitisha ujumbe unaopashwa, hujenga na kuchochea kumbukizi na kuzidisha athari kwa mpokezi wa ujumbe (Brierley,1995 na Leech, 1996). Mhimili uliotumiwa katika kuchanganua leksia hizi ni umilisi wa Sarufi Zalishi. Katika Jedwali 2.11, mifano inayohusiana na mahali, urudiaji, wazo, hisia kuzaji, antonimu, sinonimu, hiponimu na uhusiano-leksika inaonyesha kuwa wanafunzi wana ung'amuzi wa vipengele husika kwa sababu umilisi huhusu ujuzi alio nao

mtumiaji wa lugha. Aidha, matumizi faafu ya vipengele hivyo, yanadhihirisha utendaji wao ambao pia ni mhimili wa Sarufi Zalishi.

Wanafuzi wote walitumia urudiaji wa nomino za kawaida katika kazi yao. Kumi na wanne walitumia sinonimu (22%), tisa walitumia antonimu (8%), kumi na mmoja walitumia hisia kuzaji (9.2%) na thelathini na mmoja walitumia hiponimu (26%). Aidha, waliotumia uhusiano leksia ni wanafunzi thelathini na sita ambayo ni asilimia 30%. Kwa hivyo, mshikamano wa kileksia ulidhihirisha kwamba urudiaji ulitumiwa zaidi, ukifuatwa na vipengele vya mfumo maana na mwisho uhusiano leksika.

Kutokana na maelezo hayo, inajitokeza kwamba chini ya nusu ya wanafunzi walitumia vipengele vya kileksia vya mfumo maana na uhusiano leksia. Kwa hivyo, kwa kutumia mhimili wa utendaji wa Sarufi Zalishi, inaamaanisha kuwa ukuzaji wa baadhi ya vipengele vya kileksia mathalani vipengele vya mfumo maana na vile vya uhusiano leksika havikukuzwa sana.

Uelewa wa maana na mahusiano ya kimaana katika leksia mbalimbali husaidia si tu katika kuleta mshikamano, bali pia katika kupima ujuzi wa mzungumzaji wa lugha. Ujuzi huu husaidia katika kutunga na kuelewa tungo mbalimbali katika lugha husika. Aidha, huleta ujumi katika utunzi kwa jumla mathalani vipengele hivyo vinapochanganywa kwa ufundi, husaidia katika kukosoa zile tungo zilitungwa vibaya na zinazotata.

### 2.5 Mshikamano wa Ubadilishaji

Hii ni hali ya umbo moja kuchukua mahali pa jingine katika nafasi fulani kwenye muundo wa usemi. Kuna aina tatu za ubadilishaji nazo ni ubadilishaji wa nomino au kikundi nomino, ubadilishaji wa kitenzi au kikundi tenzi na ubadilishaji wa kishazi (Halliday na Hasan, 1976). Chunguza sentensi zifuatazo;

*Sentensi 9a (i):* Nimetupa *chakula* kilichooza na kutengeneza *kingine.*

*ii):* Alipendezwa na *msichana mrembo*; nami nikapendezwa na *huyo huyo.*

*b):* Je, ninaweza *kumaliza kazi* hii kwa muda ufaao? Pengine *nitafanya hivyo.*

c(i): *Silabasi iliyopendekezwa na Wizara ya Elimu ni bora kuliko ya awali.*

*d):* Sikubaliani *hivyo.*

Sentensi 9(a) i) na ii) ziinaonyesha ubadilishaji katika nomino na kikundi nomino mtawalia. Sentensi ya b) inaonyesha ubadilishaji katika kitenzi nayo ya c) inaonyesha ubadilishaji katika katika kishazi. Mifano kutoka insha za wanafunzi ni kama ifuatayo:

**Jedwali 2.12: Mshikamano wa Ubadilishaji**

| Ubadilishaji-Aina | Sentensi | Ubadilishaji |
|---|---|---|
| Nomino | Wakati uliwadia ambapo *Bi arusi* aliingia akiwa na wavyele wake kwa mwendo wa aste aste…Bwana arusi alitabasamu akiichukua | 'Bi arusi' na 'mali yake' |

| | | |
|---|---|---|
| | ‘*mali yake’* kutoka kwa wazazi. | |
| Kitenzi | i) “Ndio *nitamchukua* Sela” Joeakim alimjibu. Na wewe Sela *utafanya hivyo* pia?<br>ii) Walitamani ardhi *ipasuke* na kuwameza wangali hai lakini *hilo* halikuwezekana. | nitamchukua, utafanya hivyo.<br>Ipasuke, hilo. |
| Kishazi | i) Alimwelekeza Nasibu kwa madaktari wa ng’ambo na akaahidi *kuwalipia watoto wake gharama yote*. Nasibu alikuwa kwanza ameshindwa kukubali *jambo hilo*.<br>ii) Walirudi nchini baadaye na kufungua shule ya walemavu ambapo *waligharamia kila kitu*. Wanafunzi walifurahishwa na *hicho kitendo*.<br>iii) Wanahabari walitoa habari kuwa *duka kuu la Martgate lilikuwa limeshambuliwa na magaidi*. Mama aliposikia *vile*, akajaribu kumpigia Abdi simu.<br>iv) Alisema kwamba Salasa alikuwa mke wake | ‘Kuwalipia watoto wote gharama yote’ na ‘jambo hilo’.<br>‘Waligharamia kila kitu’ na ‘hicho kitendo’<br>Duka kuu la Margate lilikuwa limeshambuliwa, vile. |

| | | |
|---|---|---|
| | na bado hakuwa amempa talaka….Je huu ni uungwana? | Amempa talaka na huu |

Wanafunzi waliweza kudhihirisha aina zote za ubadilishaji; wa nomino, kitenzi na kishazi. Nomino *bi arusi* katika mfano wa kwanza ina uhusiano wa mshikamano wa ubadilishaji na *mali yake.* Kitenzi *nitamchukua* kina uhusiano wa mshikamano wa ubadilishaji na *utafanya hivyo* na kishazi *duka kuu la Martgate lilikuwa limeshambuliwa* kimewakilishwa na *vile.*

Ubadilishaji ulichukua nafasi ndogo katika kazi ya wanafunzi. Wanafunzi 22 tu ndio walitumia dhana hii. Hii ni asilimia 18.3. Hali hii inajitokeza pia katika utafiti wake Thiga (1997).

Wanafunzi katika kukosa kutumia mshikamano wa ubadilishaji kwa wingi, inamaanisha kuwa utendaji wao wa kipengele hiki u chini. Hili liliafikiwa kwa kutumia mhimili wa utendaji wa Sarufi Zalishi. Utendaji huhusu matumizi ya ujuzi alio nao mtu katika hali halisi. Aidha, mhimili wa umilisi ulitumiwa katika kutambua ubadilishaji husika katika tungo za wanafunzi. Wanafunzi waliweza kutumia ubadilishaji wa nomino, vitenzi na kishazi kwa sababu waliving’amua vingele hivi akilini. Umilisi huhusu ujuzi alio nao mtumiaji wa lugha husika. Kwa hivyo, walitumia ujuzi wa ubadilishaji.

## 2.6 Mshikamano wa Udondoshaji

Hii ni hali ambapo baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kisarufi huachwa bila kuathiri maana. Sehemu iliyodondoshwa inaweza kupatikana kutokana na usemi uliotangulia. Udondoshaji pia ni wa aina tatu; wa nomino, kitenzi na kishazi. Mifano ifuatayo inadhihirisha hayo;

*Sentensi 10 (a):* *Nchi* yangu ni Kenya, – yako ni ipi?

*(b)*: Mwalimu *anasoma* jarida na mwanafunzi – kitabu.

*c (i)*: *Unaenda maktabani?*

*(ii)*: Ndio –

Sentensi 10 (a) inaonyesha udondoshaji wa nomino, (b) wa kitenzi na (c) wa kishazi. Umilisi na utendaji wa dhana hii ya mshikamano wa udondoshaji ulijitokeza ifuatavyo katika insha za wanafunzi, kama ilivyo katika jedwali 2.13.

**Jedwali 2.13: Mshikamano wa Udondoshaji**

| Aina ya udondoshaji | Sentensi | Vipengele vilivyodondoshwa |
|---|---|---|
| Nomino/kikundi nomino | a) Kina baba walitamani kuwa katika kusakata *densi* lakini ilikuwa tu ya kina mama. | Densi |
| | b) Tulipofika pale ambapo njia ilikuwa panda, kundi moja lilifuata njia ya kulia na jingine likafuata ya kushoto. | Njia |

| | | |
|---|---|---|
| | c) Nilimweleza mwandani wangu kuhusu wazo langu na moja kwa moja bila kupoteza muda tukaaanza kutengeneza vilipuzi hata kama vyetu si kama vile vilivyotengenezwa na majasusi. | Vilipuzi |
| Kitenzi/Kikundi tenzi | "Wewe Ng'anga, utamchukua Zuhura Napendo kama bibi yako, *kumpenda*, na *kumtuliza* hadi kifo? Kasisi aliuliza.<br>'Naam' Ng'anga alijibu. | Kumpenda na kumtuliza |
| Kishazi | i) Ilimfanya Nasibu atake kuwaua watoto wake kwani walikuwa mzigo aliokuwa ameshindwa kuubeba. Mgongo wake ulikuwa umeganda na uchovu na hakuwa tayari kuendelea. | Kubeba mtoto mgongoni. |

Wanafunzi walidhihirisha aina zote za udondoshaji; wa nomino, kitenzi na kishazi. Udondoshaji wa nomino katika mfano wa pili '*Tulipofika pale ambapo njia ilikuwa panda, kundi moja lilifuata njia ya kulia na jingine likafuata ya kushoto* nomino *njia* imedondoshwa katika sehemu ya pili. Kuhusiana na kitenzi, mfano 'Wewe Ng'anga, utamchukua Zuhura Napendo kama bibi yako,

*kumpenda*, na *kumtuliza* hadi kifo? Kasisi aliuliza. '*Naam*' Ng'anga alijibu. Ng'ang'a amedondosha *kumtuliza* na *kumpenda*. Amejibu: 'Naam', badala ya 'Naam,nitamchukua Zuhura Napendo kama bibi yangu, kumpenda na kumtuliza hadi kifo. Hatimaye, katika upande wa kishazi, kishazi kubeba mtoto mgongoni kimedondoshwa mwishoni mwa sentensi.

Udondoshaji uliojitokeza katika mifano katika jedwali 3.9 umekuza maudhui mbalimbali kwa kutumia maana ya maana tambuzi ya nadharia ya SAM. Katika upande wa kikundi nomino, maudhui ya vitendwa 'densi' 'njia' na 'vilipuzi' yamekuzwa. Katika upande wa kikundi tenzi, maudhui ya kuchukua, kupenda na kutuliza yamekuzwa. Katika muktadha huu vilevile, kwa kutumia maana husishi ya nadharia ya SAM, wazo la 'kutuliza bibi' linadokeza maudhui ya nafasi ya mwanamke ya kudunishwa na nafasi ya mwanamume (ubabedume) katika jamii.

Aidha, uchanganuzi huu uliafikiwa kwa kutumia mhimili wa umilisi wa Sarufi zalishi. Mwanafunzi ana ung'amuzi wa kile anachodondoa. Umilisi wake unajitokeza anapotumia upatanisho mwafaka wa sarufi katika udondoshaji kwa sababu umilisi huhusu ujuzi wa mhusika wa kutunga na kuelewa tungo za lugha yake.

Wanafunzi kumi na watano pekee ndio walitumia mshikamano wa udondoshaji ambayo ni asilimia 13 ya wanafunzi wote kwa jumla. Hali hii pia inajitokeza katika utafiti wa semi zungumzi miongoni wa wasemi wa Dholuo (Saddimbah 2011).

Wanafunzi katika kukosa kutumia mshikamano wa udondoshaji kwa wingi, inamaanisha kuwa utendaji wao wa kipengele hiki u chini kama ilivyokuwa pia katika mshikamano wa ubadilishaji. Hili liliafikiwa kwa kutumia mhimili wa utendaji wa Sarufi Zalishi. Aidha, ili kutathmini namna udondoshaji umetokea katika matini, uchanganuzi wa maudhui ulifanywa. Maudhui haya yalitathminiwa kwa kutumia mhimili wa maana tambuzi wa SAM.

Hata hivyo, mshikamano huhusiana sana na kiimbo. Uhusiano huu hujikita katika ama upazaji au ushushaji wa mawimbi katika usemi.

### 2.7 Mshikamano na Kiimbo

Kiimbo ni utaratibu wa kupaza na kushusha sauti katika usemaji (Njogu, Mwihaki na Buliba, 2006). Kwa mujibu wa Halliday na Hasan, dhana ya kiimbo inakuwa kipengele cha mshikamano ikiwa kile kinachotajwa ama kwa kupandisha au kushusha sauti kinahusishwa na matini iliyotangulia, vinginevyo, haiwezi kuchukuliwa kama kipengele cha mshikamano. Katika kuleta mshikamano, mikondo miwili ya kiimbo huhusishwa;

i) Mkondo wa kupanda-shuka

ii) Mkondo- shuka

#### 2.7.1 Mkondo wa Panda-Shuka

Mkondo huu wa panda-shuka hutumiwa pamoja na uunganishaji wa kinyume kwa mfano, Halliday na Hasan (1976) katika uk 273 wana mifano ifuatayo;

*Sentensi 11(a)*: Watu walitumia nguo kuingia katika ukumbi wa kuigiza, sasa

*/sasa/* wanavaa chochote.

Hapa, */sasa*/ linatumika kuonyesha kinyume au tofauti kati ya kinachofanywa na kilichokuwa kikifanywa.

*Sentensi (b):* Shida yake ni *mguu. Kichwa* tayari ni kikubwa. Neno '*Kichwa'* linatumika hapa kuonyesha tofauti kati yake na *mguu.*

*Sentensi (c):* *Si vizuri* kuchelewa shuleni. Alisema mwalimu, " *Si vizuri kabisa* kwani husababisha kutofanikiwa kwingi." */si vizuri kabisa*/ hutofatiana na */vizuri/.*

### 2.7.2 Mkondo - Shuka

Mkondo-shuka hutumiwa kusisitiza uunganishaji wa kuongeza. Kwa mfano ;

*Sentensi 12:* Kijana aliingia kitandani akiwa amefurahi. *Asubuhi yake*, alipanga mizigo na kuondoka. Kishazi '*Asubuhi yake*' kinatumika hapa kuonyesha nyongeza ya vitendo vyake. Kishazi hiki kikitumika vinginevyo hakitaleta maana kama ya sentensi ya awali. Kwa mfano, *Asubuhi yake huwa na uchovu mwingi*.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imeangazia kwa kifupi aina mbalimbali za mshikamano na namna vipengele mbalimbali vya mshikamano vilivyokuza uelewa wa maudhui katika insha za wanafunzi. Aidha, uhusiano kati ya mshikamano na kiimbo umeonyeshwa. Mshikamano wa urejeshi uliongoza, ukifuatwa na mshikamano wa

kuunganisha, wa kileksia, ubadilishaji, mshikamano wa udondoshaji na uhusiano kati ya mshikamano na kiimbo ulichukua nafasi ya mwisho. Sura ya tatu itaonyesha namna vipengele hivi vya mshikamano vilivyolemaza uelewa wa maudhui katika insha za wanafunzi.

# SURA YA TATU

# MATUMIZI POTOSHI YA MSHIKAMANO KATIKA INSHA ZA WANAFUNZI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia kwa kifupi namna vipengele vya mshikamano vilivyolemazwa katika insha za wanafunzi wa shule za upili. Kulemazwa au makosa ya mshikamano katika insha hizi yamechanganuliwa kwa kutumia mihimili ya maana matinishi na maana husishi ya Sarufi Amilifu Mfumo ili kutathmini usarufi katika tungo za wanafunzi. Makosa yanayohusiana na mshikamano pekee ndiyo yaliangaziwa na kuainishwa katika makundi mbalimbali. Jedwali la 3.8 limerejelewa katika kuelezea asilimia ya makosa katika makundi hayo.

Vipengele vya mshikamano vinapokosa kutumiwa vizuri, hutatiza uelewa wa maudhui kwa jumla. Sehemu hii itaangalia namna vipengele hivyo vimetumiwa vibaya na kwa hivyo, kusababisha ufifishaji wa mshikamano. Makosa haya yanayohusiana na mshikamano katika insha za wanafunzi yamegawanywa katika matapo mbalimbali kwa kutumia mhimili wa maana matinishi. Mhimili huu umesaidia katika kutathmini usarufi wa vipengele hivi katika insha husika.

**3.1 Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi**

Makosa ya upatanisho wa kisarufi yalijitokeza katika insha za wanafunzi kama ifuatavyo katika Jedwali 3.1.

**Jedwali 3.1: Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi**

| Makosa | Sahihi |
|---|---|
| i) Mwanamume yule alikuwa ametoka benkini kutoa hela ambazo zilikuwa za shule. Ilikuwa shillingi million moja. | Mwanamume yule alikuwa ametoka benki kutoa hela ambazo zilikuwa za shule. Zilikuwa shilingi milioni moja. |
| ii) Changamoto mingi ambazo walizipitia hao hazikusababisha wao kufa moyo. | Changamoto nyingi ambazo walizipitia hazikuwafisha moyo. |
| iii) Shule yetu iliibuka ya tatu na ilikuwa na wanafunzi *tatu* bora katika kidato cha nne. | Shule yetu iliibuka ya tatu na ilikuwa na wanafunzi *watatu* bora katika kidato cha nne. |
| iv) Kutokana na kazi ya binti huyo kuzoea kukaa mno na mwakilishi wa bunge, hata alibidiwa kutembea naye momote aingiapo na aendako. | Kutokana na binti huyo kuzoea mno kukaa na mwakilishi wa bunge, alihitajika kutembea naye momote aingiamo na aendamo.<br>au<br>Kutokana na binti huyo kuzoea mno kukaa na mwakilishi wa bunge, alihitajika kutembea naye kokote aingiako na aendako.<br>au |

| | |
|---|---|
| | Kutokana na binti huyo kuzoea kukaa mno na mwakilishi wa bunge, alihitajika kutembea naye popote aingiapo na aendapo. |
| v) Sherehe hilo lilikuwa na furaha sana. | Sherehe hiyo ilikuwa ya furaha sana. |
| vi) Tulizungumza nao kwa heshima kubwa tukaweza kuzungumzia mambo kadha iliyowakabili. | Tulizungumza nao kwa heshima kubwa kuhusu mambo kadha yaliyowakabili. |

Makosa ya upatanisho wa kisarufi yalijumulisha makosa ya matumizi ya vihusishi visivyofaa, viambishi vya ngeli, wakati na udogo na ukubwa, vivumishi na udondoshaji wa viambishi katika maneno. Mhimili wa maana matinishi wa nadharia ya SAM ulifaa sana hapa katika kupima huu upatanisho wa kisarufi kwani mhimili huu hupima usarufi katika tungo. Makosa 77 ya upatanisho wa kisarufi ambayo ni asilimia 18 kwa jumla ya makosa yote yalifanywa na wanafunzi. Hii ni asilimia 64 ya jumla ya wanafunzi; jambo linaloonyesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi walikuwa na tatizo la kupatanisha sarufi. (Taz. Jedwali 3.8 la makosa mwishoni mwa sura hii).

Upatanisho wa kisarufi husaidia sana katika kuleta mshikamano wa maneno katika sentensi (Mdee, 1986, Kapinga, 1983, Crystal, 1981). Hata hivyo, Kapinga anasisitiza kwamba iwapo nomino ina kiambishi awali kinachotambulisha ngeli,

basi maneno mengine yaliyotawaliwa na nomino hiyo hufuata upatanisho wa kisarufi wa neno hilo. Hili linaungwa mkono na Kihore na  wenzake (2003) wanaposema kuwa upatanisho wa kisarufi ni kule kukubaliana kunakojitokeza baina ya nomino/kiima na kitenzi au kivumishi. Mawazo haya yanasisitiza umuhimu wa upatanisho wa kisarufi katika makala. Hali kuwa wanafunzi zaidi ya nusu walikuwa na tatizo hili kutokana na utafiti, ni jambo linalofaa kushughulikiwa kwa dharura.

## 3.2 Makosa ya Kileksia

Ifuatayo ni mifano ya makosa ya kileksia kutoka insha za wanafunzi.

**Jedwali 3.2: Makosa ya Kileksia**

| Makosa | Sahihi |
|---|---|
| Mamake alijawa na hofu na wasiwasi na baadaye ugonjwa ukampata. Alilazwa hospitalini lakini hakuna ambaye angemlipia *karo*. | Mama alijawa na hofu na wasiwasi. Baadaye, ugonjwa ukampata. Alilazwa hospitalini lakini hakuwa na wa kumlipia *bili*. |
| Kasisi huyo alikuwa akiyasoma *makubaliano* hayo wakirudia baada yake. | Kasisi huyo alikuwa akisoma *kiapo* huku wakirudia baada yake. |
| Usaidizi ulikuwa wa hali ya juu sana kwa kutoa watu kwa *manyumba* zilizobomoka. | Usaidizi ulikuwa wa hali ya juu sana kwa kutoa watu kwenye *nyumba* zilizobomoka. |

| | |
|---|---|
| Polisi waliwakamata tena na *kuwasilimisha* kwenye kituo hicho. | Polisi waliwasalimisha kwenye kituo cha polisi. |
| Ghafla, nilihisi kifaa kizito kimenigonga kichwani ambacho kilinifanya nianguke mchangani *puf!* | Ghafla, nilihisi kifaa kizito kimenigonga kichwani ambacho kilinifanya nianguke mchangani *tifu!* |
| Mzee Mawewa alisema huku akiguguma. | Mzee Mawewa alisema huku akigugumia. |

Makosa ya kileksia yaliyojitokeza katika insha za wanafunzi yalijitokeza kwa namna ifuatavyo; Kuandika msamiati visivyofaa, utohozi usiofaa, msamiati potoshi, kuchanganya ndimi, unyambuaji usiofaa, tabdili na matumizi ya sheng'. Mbali na mifano katika jedwali la makosa ya kileksia, mingineyo ni; *msamiria mwema* badala ya *msamaria mwema, kuvua mimea, alinunua stove, baba mrembo, nilikimbia chap chap, maji kutoka mtoni 'yalipaa' hadi manyumbani, mmoja wao 'aliwika'* baada ya *kuumia, hulkahulka* badala ya *pilkapilka, mahadarati* badala ya *mihadarati, kata kona (sheng') na mayoye* badala ya *mayowe.* Makosa 45 ya kileksia yalichukua asilimia10. Asilimia ya wanafunzi waliofanya makosa ya kileksia ni 38 (Taz. Jedwali la 3.8 la makosa mwishoni mwa sura hii).

Makosa ya kileksia yalilemaza uelewa wa maudhui kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, sentensi i) katika Jedwali 3.2 inapotosha kwa sababu karo ni malipo ya

shuleni na wala si hospitalini. Aidha, neno 'makubaliano' katika sentensi ii) ni neno la kijumla mno wala halijikiti tu katika muktadha wa arusi pekee. Kwa hivyo, kwa kutumia mhimili wa maana tambuzi wa SAM unaohusiana na maudhui, maudhui ya 'bili' na kiapo yamelemazwa. Makosa ya kileksia ya aina hii yanaonyesha tatizo la ung'amuzi wa vipengele hivyo na kwa sababu hii mhimili wa umilisi wa Sarufi Zalishi ulifaa hapa katika kuchanganua makosa hayo ya kileksia.

## 3.3 Makosa ya Viunganishi

Makosa yanayohusiana na viunganishi pia yalijitokeza kwenye insha za wanafunzi kama ilivyo katika Jedwali 3.3.

**Jedwali 3.3: Makosa ya Viunganishi**

| Makosa | Sahihi |
|---|---|
| a) Mwata alipoambiwa, alipata huzuni kwa kuachwa *na pia kwa sababu* hangeweza kuja nyumbani. | Mwata alipoambiwa, alipata huzuni *kwa sababu* asingekuja nyumbani. |
| b) Alikuwa mpenda utajiri *na hivyo*, aliwakandamiza watu na kuwanyanyasa | Alikuwa mpenda utajiri *hivyo*, aliwakandamiza watu. |
| c) Wengi walijawa na maswali na basi kuuuliza kwa nini alimpendelea hivyo. | Wengi walijawa na maswali *na* kuuliza kwa nini alimpendelea hivyo. |

| | |
|---|---|
| d) Baada ya kunielezea yaliyojiri, nilimpeleka hospitalini *na baada yake* kulazwa pale. | Baada ya kunielezea yaliyojiri, nilimpeleka hospitalini. Baadaye, alilazwa pale. |
| e) Nilipojipinduka na kujiekelea blanketi ile pana na iliyokuwa na joto jingi kutokana na baridi shadidi iliyokuwepo ndiposa jogoo wa kwanza aliwika na nikaanza kunuguna lakini nikafika elewa kuwa atafutaye hachoki na akichoka keshapata. | Kutokana na baridi shadidi, nilijipindua na kujiwekelea blanketi la joto jingi. Jogoo wa kwanza alipowika, nilinung'una lakini nikaelewa kuwa atafutaye hachoki, akichoka, keshapata. |

Baadhi ya viunganishi havikukamilika, vingine viliandikwa na kutumiwa vibaya hasa visababishi na vya kinyume. Hili lilisababisha sentensi kuwa na ama maana zaidi ya moja au maana potoshi hasa katika matumizi ya viunganishi viongezi . Aidha, wengine waliandika viunganishi kwa lugha ya Kiingereza huku wengine wakivimilikisha. Kwa mfano, waliendelea kula 'and' kuimba na 'baada yake' Isitoshe, katika mfano wa a), mwanafunzi ametumia viunganishi vitatu kwa pamoja; viongezi viwili 'na na pia' na kisababishi kimoja yaani 'kwa sababu'. Haya ni matumizi mabaya. Mbali na sentensi zilizoorodheshwa katika Jedwali 3.3, sentensi 'Tulifika hotelini ambamo vyakula viliandaliwa na vinywaji' inapotosha kimaana. Sentensi hii inaweza kumaanisha kuwa vyakula viliandaliwa

na vinywaji kwa hivyo, kukosa mantiki kwa sababu vinywaji vitakuwa vimepewa uwezo wa kuandaa vyakula. Uhuishi wa aina hii hukosesha sentensi maana kamili na faafu.

Viunganishi vinapotumika vizuri husaidia kujenga na kuimarisha mshikamano. Pia, hutumiwa kama kitambulishi cha hadhi ya vishazi katika matini (Halliday, 1994). Asilimia ya wanafunzi waliofanya makosa yanayohusiana na viunganishi ni 43. (Taz. Jedwali 3.8).

Viunganishi vinapotumika, nia ya matumizi hayo lazima yabainike wazi; kuonyesha ziada, kulinganua, sababu, wakati na uteuzi. Wanafunzi wanaposoma kwa upana na kufanya mazoezi katika maongezi yao, makosa katika muktadha wa viunganishi hupungua. Kwa mfano, makosa ya kuchanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili ni ishara ya ukosefu wa msamiati katika lugha husika au mazoea ya kuchanganya lugha kiholela, wanafunzi wanapozungumza.

## 3.4 Makosa ya Tafsiri Isiyofaa

Makosa ya tafsiri isiyofaa yalichangiwa na mambo kadha kama ilivyodokezwa katika aya zitakazofuatia. Jedwali 3.4 lifuatalo linaonyesha namna makosa hayo yalivyojitokeza katika insha za wanafunzi.

**Jedwali 3.4: Tafsiri Isiyofaa**

| Makosa | Sahihi |
|---|---|
| i) Ilikuwa ni siku ya Alhamisi | Ilikuwa siku ya Alhamisi nilipokuwa |

| | |
|---|---|
| nilipokuwa nastahili kusafiri nyumbani baada ya likizo ya Agosti kwa sababu linalo mwanzo, lina mwisho. | nastahili kusafiri nyumbani baada ya likizo ya Agosti kwa sababu lililo na mwanzo, lina mwisho. |
| ii) Juma na Salasa walifunga chapta hiyo na kuanzisha mpya. | Juma na Salasa walifunga ukurasa huo na kuanzisha mpya. |
| iii) Juma alimbusu Salasa, kionyeshi cha mapenzi yake. | Juma alimbusu Salasa kama ishara ya mapenzi yake. |
| iv) Alipata mtoto wa kiume aliyeitwa ali baada ya baba, aliyeaga dunia miaka tatu zilizopita. | Alijifungua mtoto wa kiume aliyemwita Ali, jina la marehemu baba aliyeaga dunia miaka mitatu iliyopita. |

Ufasiri ni kazi inayohusiana na lugha na tamaduni mbili tofauti. Nida (1975) anaonyesha kuwa ili tafsiri iwe nzuri inafaa ifuate kanuni za hali ya ujumbe, lengo la tafsiri na la msemaji na aina ya walengwa. Tafsiri yoyote ile inastahili ifae ndiposa Mbaabu (1986) anaunga wazo hili mkono anaposema kwamba tafsiri yaweza kuwa haifai ikiwa semi, methali au matumizi mengine ya lugha moja yatatafsiriwa moja kwa moja hadi lugha nyingine bila uangalifu.

Asilimia 6 ya wanafunzi walitafsiri na kutohoa moja kwa moja kutoka ama lugha ya kwanza au Kiingereza. Kwa mfano, *chapta* badala ya *sura* na *kionyeshi* badala ya *ishara*. Mifano zaidi ni kama vile tulipakiwa (parked), tuliwahisia (we felt for

them), Alifunguka (became open), boeka (get bored), baiwa ( to be bought for) na demu (dam). Kama ilivyojitokeza, tafsiri mbaya ilisababisha baadhi ya wanafunzi kutohoa visivyo. Kwa sababu hii, maana katika baadhi ya sentensi ilipotoka. Utohozi ukitumiwa vizuri hurahisisha matamshi na mawasiliano. Aidha, huipa lugha uamilifu (Maina, 2011). Hata hivyo, kosa hili halikujidhihirisha kama sugu miongoni mwa wanafunzi. Hili limeonyeshwa katika jedwali 3.8 la makosa mwishoni mwa sura hii.

## 3.5 Makosa ya Urudiaji

Makosa ya urudiaji yalilemaza uelewa wa maudhui katika tungo za wanafunzi kama inavyodhihirika katika Jedwali 3.5.

**Jedwali 3.5: Makosa ya Urudiaji**

| Makosa | Sahihi |
|---|---|
| i) Alikuwa mpenda utajiri na hivyo aliwakandamiza watu na kuwanyanyasa | Alikuwa mpenda utajiri hivyo, aliwakandamiza watu.<br>Au<br>Alikuwa mpenda utajiri na/hivyo, aliwanyanyasa watu. |
| ii) Shule zilikuwa na huduma nzuri, manufaa na usaidizi kwa walemavu. | Shule zilikuwa na manufaa kwa walemavu. |
| iii) Madai mengi yalijitokeza kuhusu | Madai yalijitokeza kuhusu mwelekeo |

| | |
|---|---|
| mwelekeo wa Sudi *kama ilivyo kawaida.* | wa Sudi kama kawaida. |
| iv) Jioni tulienda kujiburudisha na *kucheza.* Kaka na mkewe *walicheza.* | Jioni, tulienda kujiburudisha na kucheza pamoja na kaka na mkewe. |
| v) Katika maegesho ya magari, magari mengi yalikuwa. | Magari yalikuwa mengi maegeshoni. |

Asilimia 22 ya wanafunzi ilidhihirisha makosa ya urudiaji. Haya yalihusu urudiaji usiofaa. Kwa mfano, kishazi kinachokamilisha sentensi kutumiwa kama kitangulizi cha sentensi inayofuata na kurudia neno lile lile zaidi ya mara tatu katika sentensi moja. Kama inavyojitokeza katika jedwali 3.5 la makosa ya urudiaji, wanafunzi walifanya makosa ya urudiaji katika misingi miwili mikuu; uradidi wa nomino na uradidi wa vitenzi. Mfano wa uradidi wa nomino ni *usaidizi* na *huduma* ilhali wa kitenzi ni *kucheza* katika sentensi ya iv).

Uradidi unapotumika vizuri husaidia katika kusisitiza dhana fulani. Uradidi ukichanganywa vizuri, huleta ujumi katika matini mbali na kuvutia. Kwa hivyo, uelewa mpana wa kile kinachorudiwa ni muhimu.

### 3.6 Makosa ya Urejeshi

Jedwali 3.6 lifuatalo linaonyesha wazi namna makosa ya urejeshi wa ndani na nje uliojitokeza. Makosa ya urejeshi dokezi hayakujidhihirisha.

**Jedwali 3.6: Makosa ya Urejeshi**

| Sentensi | Sahihi |
|---|---|
| i) Haukupita hata siku moja kwa vile kazi ilianza siku ifuatayo. | Haikupita hata siku moja kwa vile kazi ilianza siku ifuatayo. |
| ii) Nikasema nimueleze ili nijue vyenye nitafanya. | Nikasema nimweleze ili nijue nitakavyofanya. |
| iii) Tulienda kanisani yenye ilikuwa na bonge la mauwa. | Tulienda kanisani mlimokuwa na shada la maua. |
| iv) Kijana huyo alimwita na kumweleza yalikuwa moyoni mwake. | Kijana huyo alimwita na kumweleza yaliyokuwa moyoni mwake. |

Makosa katika muktadha wa urejeshi yalijitokeza kupitia kwa matumizi mabaya ya ‘amba’ na ‘o’ rejeshi na matumizi ya mzizi –enye. Kwa mfano, ‘Tulienda kanisani yenye..’ Wanafunzi 27 walifanya makosa ya aina hii ambayo ni asilimia 23. Aidha, haya yalitokana na kudondoa viambishi vya urejeshi. Hata hivyo, makosa ya urejeshi dokezi hayakudhihirika.

Urejeshi unaofaa huimarisha mriririko wa mawazo katika tungo. Uhaba wa mazoezi mapana hufanya wanafunzi kutumia vibaya mzizi –enye kama ilivyojitokeza. Mazoezi hufanya mhusika kung’amua dhana mbalimbali za mzizi huu ambazo ni kuonyesha umilikaji, hadhi/cheo, kubainisha, kutofautisha, kuonyesha tabia na kuonyesha namna kitu kilivyo.

### 3.7 Makosa ya Viashiria

Viashiria vya karibu, mbali kidogo na mbali mno vilitumiwa vibaya kama ifuatavyo; (Taz. Jedwali 3.7).

**Jedwali 3.7: Jedwali la Makosa ya Viashiria**

| Makosa | Sahihi |
|---|---|
| i) Wakati uliyongojewa ulifika. | Wakati uliongojewa ulifika. |
| ii) Walijawa na furaha ya kibogoyo aliyeota meno lakini hawakujua meno *iyo iyo* ingeng'oka. | Walijawa na furaha ya kibogoyo aliyeota meno lakini hawakujua meno *hayo hayo* yangeng'oka,<br>Au<br>Walijawa na furaha ya kibogoyo lakini hawakujua meno *yayo hayo* yangeng'oka. |
| iv) Kutokana na hali yake, hakupata fursa *hio.* | Kutokana na hali yake, hakupata fursa *hiyo.* |
| v) Licha ya hayo, nilielewa kuwa watoto hao wanapita mtihani na *hio* shule ndiyo bora zaidi nchini. | Licha ya hayo, nilielewa kuwa watoto hao wanapita mtihani na *hiyo* shule ndiyo bora zaidi nchini. |
| vi) Nilijionea fahari sana kuwa mmoja wa wale waliochaguliwa chuoni mwetu kwenda katika ziara hili. | Niliona fahari kuwa mmoja wa wale waliochaguliwa chuoni mwetu kwenda katika ziara *hii.* |

Makosa ya viashiria yalijumlisha asilimia 6 ya jumla ya makosa yote huku shule za wilaya zikiongoza. Shule za kaunti zilidhihirisha makosa machache ya viashiria kuliko shule za kitaifa. Kutokana na hilo, makosa ya viashiria si sababu kuu ya ukosefu wa mshikamano katika insha za wanafunzi kwa jumla.

Makosa machache ya viashiria yalifasiriwa kumaanisha kuwa umilisi na utendaji wa wanafunzi katika matumizi ya viashiria u juu. Uchanganuzi huu uliafikiwa kwa kutumia mihimili ya umilisi na utendaji ya Sarufi Zalishi; kuwa wana ujuzi wa viashiria na wanavitumia kwa njia inayofaa.

### 3.8 Makosa ya Vilinganuzi

Vilinganuzi vilitumika isivyofaa na baadhi ya wanafunzi. Kwa mfano, *uwanja ulijaa kama siafu* badala ya *uwanja ulijaa watu kama siafu* na *Tulifurahia kama kibogoyo aliyeng'oka meno* badala ya *tulifurahia kama kibogoyo aliyeota meno.*

Vilinganuzi vilitumiwa visivyo huku baadhi ya wanafunzi wakitumia maneno kwa vilinganuzi visivyofaa, na kutokamilisha baadhi ya vilinganuzi. Kwa mfano, sentensi 'Tulifurahia kama kibogoyo aliyeng'oka meno' inakosa mantiki kwani tunatarajia kibogoyo afurahie akiota meno. Mifano zaidi kutoka insha za wanafunzi ni; *alilalalala kama sungura, mkutano kaa huo* badala ya *mkutano kama huo*, *alifurahia kama ghaya* na *banana kama ndizi*. Asilimia ya makosa haya ilikuwa 2. Kama katika viashiria, inafasirika kwamba sababu kuu ya ukosefu

wa mshikamano katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne si makosa ya vilinganuzi ila sababu zinginezo kama inavyodhihirishwa katika Jedwali 3.21.

### 3.9 Makosa ya Vimilikishi

Vimilikishi kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 2.1, huzingatia nafsi ya umilikaji; makosa yatatokea ikiwa kuna kutokubaliana kwa kimilikishi na nafsi. Kwa mfano, 'wilaya *wao',* badala ya 'wilaya *yao*', ' kitanda *yangu'* badala ya 'kitanda *changu', '*mwajiri *mwetu'* badala ya 'mwajiri *wetu' na* 'mipango *zao* badala ya 'mipango *yao'.* Usarufi katika muktadha huu uliathiriwa na kwa njia hii mhimili wa mhimili wa maana matinishi wa SAM ulitumiwa. Mhimili huu hutathmini kama tungo zimeandikwa kwa kufuata kanuni za sarufi husika.

Makosa yaliyojitokeza hapa ni ya kuchanganya vimilikishi na kuvitumia visivyo. Makosa haya yalifanywa na wanafunzi 22. Vimilikishi vya nafsi ya pili na tatu vilitatiza wanafunzi. Makosa ya vimilikishi yalichukua asilimia 5 ya jumla ya makosa huku asilimia 18 ya wanafunzi wakiyafanya. Makosa mengi yalishuhudiwa katika shule za kibinafsi na za wilaya.

Uelewa wa nafsi na mizizi ya umilikaji humsaidia mwanafunzi kupunguza makosa yanayohusiana na umilikaji mathalani –angu, -etu, -ako, -enu, -ake na –ao. Aidha husaidia katika kuimarisha urejeshi mwafaka.

### 3.10 Makosa ya Nafsi

Baadhi ya wanafunzi hawakudumisha nafsi iliyodokezwa katika kimalizio cha insha husika. Kimalizio kilikuwa …..*Itakumbukwa kuwa siku muhimu sana maishani mwao*. Nafsi katika kimalizio ni ya tatu wingi. Aidha, wengine walichanganya nafsi, hasa walipotumia vimilikishi. Asilimia 13 ya wanafunzi ilifanya makosa haya huku wengi wakitoka shule za kibinafsi na wilaya.

Udumishaji wa nafsi ni jambo muhimu katika insha za wanafunzi. Udumishaji huu, mbali na kuimarisha mshikamano, huonyesha umakini wa mwanafunzi katika utunzi wake kwa jumla.

### 3.11 Makosa ya Mshikamano katika Sentensi

Makosa katika sentensi yaliulemaza mshikamano na uelewa wa maudhui kwa jumla yalijumlisha makosa ya kisarufi na tahajia. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya; *Nilichukua maji na karai ambapo maji hayo yalikuwa fufutende* badala ya *nilichukua maji fufutende kwa karai*. Aidha, *bila ya kutarajiwa ndege likaamriwa kurudi kwani lilikuwa lina kasoro kiasi* badala ya *Rubani aliamriwa kurudisha ndege kwani lilikuwa na kasoro kiasi*. Isitoshe, *Juma na salasa walipiga densi*. (Sheng'). Badala ya *Juma na Salasa walisakata densi* na *nilipojipinduka na kujiekelea blanketi ile pana na iliyokuwa na joto jingi kutokana na baridi shadidi iliyokuwepo ndiposa jogoo wa kwanza aliwika na nikaanza kunuguna lakini nikafika elewa kuwa atafutaye hachoki na akichoka keshapata* badala ya *kutokana na baridi shadidi, nilijipindua na kujiwekelea blanketi la joto jingi. Jogoo wa*

*kwanza alipowika, nilinung'una lakini nikaelewa kuwa atafutaye hachoki, akichoka, keshapata.*

Baadhi ya sentensi zilielekea kupotoka kwa sababu ya kukosa kuakifishwa au kuakifishwa vibaya hasa matumizi ya kitone kabla ya sentensi kukamilika. Baadhi ya sentensi hazikukamilika na zingine hazikufuata kanuni kikamilifu. Hili lilipelekea sentensi hizo kuwa na zaidi ya maana moja au kupotosha maana kwa jumla. Aidha, zingine zilikosa umantiki. Kwa mfano, 'alipiga densi' badala ya 'kusakata densi' na *nilichukua maji na karai* badala ya *nilichukua maji kwa karai*. Asilimia kubwa zaidi ya wanafunzi ilifanya makosa haya; wanafunzi 83 ambayo ni asilima 69. (Taz. Jedwali 3.8).

**3.12 Makosa ya Udondoshaji**

Kutokana na zoezi walilofanya wanafunzi, (Taz. Kiambatisho ii), ilibainika kwamba wanafunzi 48 walifanya makosa ya udondoshaji. Hii ni asilimia 40 ya wanafunzi wote. Hawa walijibu: *Darasa la wanakidato cha pili ni chafu ilhali cha wanakidato cha tatu ni safi* badala ya *darasa la wanakidato cha pili ni chafu ilhali la wanakidato cha tatu ni safi*.

Nomino iliyokuwa imedondoshwa katika swali la zoezi husika ni nomino 'darasa'. Kwa hivyo, kiambishi 'la' kilifaa katika kuleta mshikamano husika. Kwa kutumia mhimili wa sarufi tambuzi wa SAM, tajriba ya matumizi ya udondoshaji husika u chini. Maudhui yaliyolemazwa katika muktadha huu ni

maudhui yanayohusu 'darasa'. Mbinu mwafaka za kufunzia udondoshaji zinafaa katika shule za upili.

### 3.13 Makosa ya Mshikamano katika Tungo

Makosa haya yalijitokeza katika insha ambayo wanafunzi walipewa kuandika. Insha ilikuwa ya mdokezo iliyowahitaji wanafunzi wamalizie kwa kimalizio walichopewa. Walitarajiwa wabuni kisa kinachoafikiana na kimalizio hicho ili waonyeshe mshikamano kati ya kisa na kimalizio husika {Taz. Kiambatisho i)}.

*Pingu mkononi, askari wakiwa nyuma Hassan na juma walitoka milango ya korti baada ya uamuzi wa mashtaka yap kufanywa, familia zao wakitoa machozi kuona kijana wao wakielekea jela kuanzia kifungo chao cha maisha baada ya kupatwa na kosa ambayo wao wenyewe walijitakia. Mwiba wa kujidunga hauambiwi bole hivi basi Hassan na Juma hawakuwa na budi ila kuubeba mzigo wao. Alakini je? Ni nini kilichotokea hadi kufika kiwango hiki?*

*Ilianza miezi mitano yaliyopita. Hassan mwanafunzi wa uhandisi wa ndege katika chuo kikuu cha Jomo Kenyatta alikuwa akitembea baada ya kutoka darasani, 'Vipi leo kaka?'Juma, rafikiye alimsalimu kwa furaha. 'Sina lolote mimi, sijui wewe?'Hasan alimjibu 'Ah! Basi nina kitu ambacho kitakacho kufurahisha. Nina suluhisho ya shida zote za pesa' Juma alimwambia. Neno pesa lilimkamata Hassan kutoka bahaki ya fikra na kumsikiliza Juma kwa makini. Hapo ndipo Juma alifungua mkoba wake, na ndani yake aliona juma kitu ambacho hakutarajia. 'Aisee! Wafanya nini na bangi wewe? Unajua uwaweza pelekwa*

*kortini na ushitakiwe, mwishowe ujipate gerezani, Hassan alimaka. 'Tulia kaka, situmii dawa hizi bali tutauza nina hakika utanishukuru baadaye' kutoka hapo Juma alialeke zake.*

*Hassan baada ya kufikiria aliona haja ya dawa hizo. na kumpigia Juma kumwarifu kuwa alikubali pendekezo lake. Haukipita hata siku moja kwa vile kazi ilianza siku ifuatayo. Juma na Hassan walizunguka kote Nairobi wakiuza bidhaa zao haramu, na kwa kweli walipata hala si chache. Hakuna asiyeweza kununua dawa hizi, si wazee, si wauni, si wanawake, si wanafunzi. hakina aliyeulizia na kunyimwa na baada ya wiki ya kwanza vijana haowalikuwa njiani kuwa wakwasi*

*Hali hii ya utajiri uliwafanta wote kudadi. Maisha yao Hassan aliacha kuenda chuoni. Ili kuendelea na mahadharati yake kwa vile alishapatapesa, basi kwa nini aendelee na masomo na ashapata chote alichotaka. Naye Juma alikata kabisa kurudi nyumbanin kwa vile hela hizo zilimpa uwezo wa kujitegemea.*

*Lakini wahenga hawakutuchezea shere. za chinikwa chini waliponena 'ujana ni moshi huishia jangwani'. Usiku mmoja, Hassan na Juma walipokuwa katika hulka hulka yao ya kuuza dawa hizo, walimfikia mja mmoja ambaye alikuwa mteja wao wa dhati hivi basi waliamina kuwa kila kitu kingeendelea kama kawaida, wapate pesa zao kisha waende zao. Punde tu walipokuwa wakimpa mizigo yake palitikea askari wawili majitu wa miraba mine, wakizielekeza bunduki zao kwa Hassan na Juma 'Umepatikana na kosa la kuuza dawa za kulevya, una haki ya kubaki kimya na chochote utakachosema kitatumiwa dhidi*

*yako kortini! Walitiwa mbarono na siku iliyofuata walifikishwa kortini na kupatwa na hatia ya kuuza dawa za kulevya na kupewa kifungo cha maisha. Itakumbukwa kuwa siku ya muhimu sana maishani mwao.*

Makosa katika insha hii yamebainishwa kwa kutumia mhimili wa maana tambuzi wa SAM. Mhimili huu huangazia maudhui katika matini. Maudhui haya ndiyo yameonyesha wazi kama mwanafunzi ama amejibu swali au la. Makosa yanayohusiana na insha ya mwanafunzi huyu ni kama yafuatayo;

i) Mwanafunzi amedokeza kuhusu siku saba katika tungo;

a) Siku Juma anampendekezea Hassan kuhusu kuuza dawa za kulevya.

b) Siku Hassan anakubaliana na wazo lake.

c) Siku wanapozunguka Nairobi wakiuza dawa hizo.

d) Kipindi cha kuwa tajiri-Siku nyingi.

e) Siku ya wote kuacha masomo.

f) Siku ya kukamatwa.

g) Siku ya kuhukumiwa.

2). Mwanafunzi amepotoka kimaudhui pia kupitia kwa toni ya uwasilishaji wa kisa. Wawili anaowazungumzia wanatiwa mbaroni kifungo cha maisha na kwao iwe siku muhimu maishani!

Wanafunzi walifanya makosa yafuatayo;

a) Kuhusisha zaidi ya siku moja badala ya siku moja tu katika swali.

b) Kutokuza siku yenyewe kikamilifu

c) Kutoonyesha umuhimu wa siku yenyewe

d) Kuonyesha siku ikiwa ya huzuni badala ya furaha kulingana na swali.

e) Kujitungia kimalizio (kutofuata maagizo)

Baadhi ya vimalizio potoshi katika insha za wanafunzi wengine vilikuwa:

i) Watu walisherehekea walipokuwa wakibusu.

ii) Mola hamsahau mja wake.

Maagizo ni muhimu sana katika kazi yoyote ile. Kulingana na mwongozo wa kudumu wa KNEC wa kusahihisha insha, mwanafunzi akifanya kosa kama hili, huadhibiwa kwa kupewa alama za bakshishi (alama 1-2). Wanafunzi 51 walifanya makosa ya mshikamano wa tungo. Hii ni asilimia 43 ya jumla ya wanafunzi wote. Insha ya mdokezo huwa na sura mbili; mwanafunzi anaweza kuulizwa au aendeleze (kitangulizi) au amalizie (kimalizio).

Mwanafunzi anafaa achunguze maneno yaliyotumiwa na ajibu swali akizingatia maneno hayo muhimu. Maneno haya huwa ndio nguzo muhimu. Toni ya mdokezo inafaa idumishwe pia. Ikiwa toni ni ya huzuni, ikuzwe kuanzia mwanzo hadi mwisho vivyo hivyo katika toni ya furaha. Nafsi vilevile inastahili idumishwe wala mwanafunzi asizichanganye. Hatimaye, mwanafunzi anafaa aonyeshe mtiririko mzuri wa aya ili adumishe uwiano kati ya aya mbalimbali na hatimaye insha mzima. Makosa yaliyoshughulikiwa katika sura hii yameonyeshwa katika jedwali lifuatalo kwa muhtasari.

**Jedwali 3.8: Muhtasari wa Makosa**

| Makosa | Shule 1 | Shule 2 | Shule 3 | Shule 4 | Shule 5 | Shule 6 | Jumla | Asilimia ya makosa | Idadi ya wanafu-nzi | Asilimia ya wanafu- |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | | | | | nzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Sentensi | 12 | 14 | 12 | 17 | 11 | 16 | 83 | 19% | 120 | 69% |
| Upatanisho wa Kisarufi | 12 | 15 | 15 | 12 | 10 | 13 | 77 | 18% | 120 | 64% |
| Viunganishi | 10 | 7 | 9 | 6 | 10 | 10 | 52 | 12% | 120 | 43% |
| Tungo | 8 | 6 | 8 | 12 | 9 | 8 | 51 | 11.8% | 120 | 43% |
| Kileksia | 4 | 5 | 8 | 11 | 7 | 10 | 45 | 10% | 120 | 34% |
| Urejeshi | 4 | 3 | 3 | 6 | 6 | 5 | 27 | 6% | 120 | 23% |
| Urudiaji | 3 | 4 | 4 | 3 | 6 | 6 | 26 | 6% | 120 | 22 |
| Vimilikishi | 2 | 3 | 8 | 2 | 2 | 5 | 22 | 5% | 120 | 18% |
| Viashiria | 3 | 6 | 3 | 1 | 4 | 4 | 21 | 5% | 120 | 18% |
| Nafsi | 2 | 3 | 4 | 3 | 1 | 3 | 15 | 3% | 120 | 13% |
| Tafsiri isiyofaa | 1 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 7 | 2% | 120 | 6% |
| Vilinganuzi | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 4 | 7 | 2% | 120 | 6% |
| Jumla | 63 | 68 | 76 | 75 | 66 | 85 | 433 | 100% | 1440 | 30% |
| Asilimia ya shule | 15% | 18% | 15% | 20% | 17% | 16% | 100% | | | |

Kama inavyojitokeza makosa ya mshikamano katika sentensi na upatanisho wa kisarufi yalichukua asilimia ya juu huku yale yanayohusiana na tafsiri isiyofaa na vilinganuzi yakichukua asilimia chache. Aidha, wanafunzi katika shule ya wilaya walikuwa na makosa mengi zaidi ikilinganishwa na wenzao kutoka shule za kaunti na kitaifa. Shule za kaunti hazikuonyesha makosa ya vilinganuzi. Makosa

ya viunganishi yalikuwa mengi katika shule za kitaifa na za wilaya. Makosa ya urejeshi yalichukua asilimia kubwa katika shule za kaunti.

### 3.14 Hitimisho

Sura hii imeangazia namna vipengele vya mshikamano vilivyolemazwa na hatimaye kulemaza uelewa wa maudhui katika insha za wanafunzi wa shule za upili hasa wa kidato cha nne. Nadharia zilizotumika katika kufanya hivi ni Nadharia za Sarufi Zalishi na Sarufi Amilifu Mfumo. Sura ya nne itashughulikia chanzo cha matatizo ya mshikamano na namna ya kuuboresha.

# SURA YA NNE

# CHANZO CHA MAKOSA YA MSHIKAMANO NA NAMNA YA KUUBORESHA

### 4.0 Utangulizi

Sura hii itashughulikia chanzo cha makosa ya mshikamano na namna ya kuuboresha. Wataalamu wa ufunzaji lugha wanatambua chanzo cha makosa katika lugha kuwa ukosefu wa umilisi wa utendakazi wa vipengele vya sarufi na matumizi ya mitindo isiyofaa ya ufunzaji (Pearson, 1981, Mclaughlin, 1987 na Ipara na Maina, 2008).

Sababu za kuwepo kwa makosa ya mshikamano katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne yaliafikiwa kwa uchunguzi wa insha walizoandika, zoezi la vipengele vya mshikamano, ukaguzi wa madaftari yao ya insha na hojaji zilizojazwa na walimu kumi na wawili wanaofunza kidato cha nne pekee. Hojaji zilichanganuliwa kwa kufuata vigezo vifuatavyo; Mbinu za kufunzia insha, viunganishi na msamiati, changamoto wakati wa kufunza na kusahihisha darasani, kiwango cha wanafunzi, na muda wa kufunza na kusahihisha insha. Ilibainika wazi kuwa kuna sababu nyingi zinazowafanya wanafunzi kufanya makosa ya mshikamano. Katika kufanya hivi, sura hii ilijibu lengo la nne la utafiti huu.

### 4.1 Mbinu za Kufunzia

Hojaji (Kiambatisho 3) zilihitaji walimu waonyeshe mbinu wanazotumia kufunzia insha, msamiati na viunganishi. Aidha, kulikuwa na haja ya kuchunguza mtazamo

wao kuhusiana na umuhimu wa mshikamano katika insha za wanafunzi, chanzo cha makosa katika tungo zao na namna ya kuuboresha . Ufasiri wa maudhui ya maelezo (mhadhara), matumizi ya vielelezo na kamusi na kushirikisha wanafunzi uliafikiwa kwa kutumia mhimili wa SAM wa maana husishi. Mhimili wa maana husishi humilikiwa na watumiaji wa lugha kama nyenzo ya kufasili na kufasiri ujumbe.Yafuatayo yalijitokeza na kufasiriwa ifuatavyo;

### 4.1.1 Mbinu za Kufunzia Insha

Maelezo kuhusu mbinu za kufunzia yalipatikana kutokana na majibu ya hojaji walizojaza walimu. Asilimia 100 ya walimu walitumia mbinu ya maelezo katika kufunzia wanafunzi insha. Waliwafafanulia kwa kina insha husika, kisha kuwaambia waandike yao. Asilimia 33 ya walimu walishirikisha wanafunzi katika ufunzaji mathalani katika kufunza kadi ya mwaliko, insha za mahojiano na dayolojia. Asilimia 83 walidhihirisha matumizi ya vielelezo vilivyoandikwa vitabuni. Mwalimu ama huwasomea vielelezo hivyo mwenyewe, huwaambia waviandike vielelezo hivyo katika vitabu vyao wenyewe au kutolesha nakala na kuwapa wanafunzi. Asilimia 17 ya walimu ilirekebisha makosa darasani. Mwalimu pamoja na wanafunzi hurekebisha makosa ya wanafunzi darasani huku wakitumia insha sampuli tatu; za mwanafunzi wa kiwango cha juu, kati na chini.

Hili linafasirika kuwa baada ya walimu wengi kuwapa wanafunzi kazi, wao huisahihisha na hawachukui muda kurekebisha makosa darasani. Jambo hili ni

hatari kwa sababu wanafunzi hawawezi kugundua makosa waliyofanya ili wasirudie kuyafanya.

Aidha, jambo la kuchagua baadhi ya insha darasani na kuzisahihisha papo hapo huenda lisimfae kila mwanafunzi kwa sababu kuna hatari ya baadhi yao kutosahihishiwa na kwa namna hiyo watakufa moyo. Aidha, hii mbinu haimfai mwalimu kwa sababu hawezi katu kukadiria vizuri kiwango cha wanafunzi wake wote kwa njia mwafaka. Hili lilijitokeza wazi katika utafiti huu. Walimu wote walionyesha wanafunzi wao kuwa wastani katika uandishi wa insha. Hata hivyo, utafiti ulionyesha asilimia 17 ya wanafunzi wao kuwa hafifu.

### 4.1.2 Mbinu za Kufunzia Viunganishi

Kuhusiana na viunganishi, asilimia 83 ya walimu ilitumia tungo zilizo na viunganishi na kuwahusisha wanafunzi katika kuvitambua. Asilimia 17 hushirikisha wanafunzi katika kutunga sentensi kisha wanafunzi hudondoa viunganishi kutokana na sentensi hizo.

Mbinu ya kushirikisha mwanafunzi humsaidia kutosahau kipengele anachofunzwa kwa sababu kadri anavyozidi kushiriki ndivyo uwezo wake wa kuking’amua kipengele husika unavyokua.

### 4.1.3 Mbinu za Kufunzia Msamiati

Walimu wote walitumia kifungu fulani kufunzia msamiati; ufahamu na tungo mbalimbali. Hata hivyo, asilimia 67 ya walimu walitumia kamusi.

Uelewa wa msamiati ni muhimu katika utunzi. Ufahamu wa msamiati mwafaka hukuza uwezo wa mwanafunzi wa kutumia si tu vipengele vya mshikamano, bali pia usemi kwa jumla. Kamusi ni muhimu katika kutambua uhusiano wa maneno na maana.

Kwa mujibu wa Norrish (1983), uteuzi mwafaka wa mbinu ni muhimu kwani husababisha shughuli za ufunzaji na ujifunzaji kwenda sambamba katika somo. Hili husaidia pakubwa katika kupunguza makosa.

### 4.1.4 Mbinu ya Idadi ya Masomo ya Insha na Kusahihisha

Isitoshe, majibu kutokana na hojaji za walimu yalitia mwanga kuhusiana na ruwaza ya ufunzaji na usahihishaji wa somo la insha; ruwaza ya kila wiki, mwezi, muhula na mwaka/ miaka. Kuhusu kufundisha na kusahihisha insha, asilimia 50 ya walimu hufanya hivyo kati ya mara moja na tatu kwa mwezi, asilimia 17 kila wiki na asilimia 33 kati ya mara moja na mbili kwa muhula. Hili linamaanisha kuwa somo la insha halipewi vipindi vya kutosha kulingana na matarajio ya silabasi kuwa somo hilo lifunzwe kila wiki. Kwa kufanya hivi, utendaji wa mwanafunzi huwa chini kuliko umilisi wake kwani hajapewa muda wa kutosha wa kutumia alichong’amua tayari. Kwa njia hii, mhimili wa Sarufi Zalishi wa utendaji na umilisi ulitumiwa katika kuchanganua wazo hili la kuonyesha namna utendaji wa mwanafunzi unaweza kuathiriwa kwa kutopewa mazoezi mapana,

licha ya kuwa mwanafunzi huyo ana umilisi wa jambo husika. Hata hivyo, asilimia 67 walisema wao huwapa wanafunzi mazoezi machache kwa sababu ya upana wa kazi na vipindi vichache vya Kiswahili ikilinganishwa na lugha nyingine kwa mfano, Kiingereza.

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa wanafunzi hupewa mazoezi machache ya insha. Walimu wana mchango mkubwa katika ama kuanguka au kupita kwa wanafunzi katika somo la insha. Wanafaa wajiandae kwa kina. Mogere (2013) aligundua kuwa walimu wanatengeneza maazimio ya kazi yanayohusisha insha lakini hawayafuati. Aidha, hawakuwa na mpangilio wa somo wanapofunza. Nasibi (2003) anasema kuwa ukosefu wa kifaa hiki hufifisha utaratibu mzuri wa ufunzaji.

Utafiti huu pia uligundua kuwa, walimu hawana mpangilio mahususi wa kufunza na kusahihisha insha za wanafunzi. Aidha, hata kama wanalifunza somo la insha, hawalipendi. Mwalimu atawahimizaje wanafunzi wakipende asichokipenda!

Ilibainika kwamba walimu wanaelewa umuhimu wa mshikamano katika tungo lakini juhudi zao ni chache kuufanikisha. Asilimia mia kwa mia walisisitiza kuwa mshikamano ni muhimu mno katika tungo za wanafunzi kwa sababu husaidia katika uelewa wa maudhui yanayozungumziwa na mwanafunzi. Hili linasisitizwa pia na Mutugu (2001). Anasema kuwa mshikamano katika insha hufanya yafuatayo miongoni mwa mengine: huvutia msomaji na kumtia moyo aendelee kusoma, hurahisisha kueleweka kwa ujumbe katika insha, humwongoza

mwandishi asirudie kwani kila wazo huanzishwa, kuelezwa na kukamilishwa na huleta uwiano ambao husaidia kuhusisha vipande tofauti tofauti vya makala kimaana na kimuundo na hivyo, kufanya msomaji aelewe kwa urahisi. Maandishi yenye mshikamano huwa na ujumi, sifa inayoyafanya yawe ya kuvutia.

**4.2 Mbinu Zinazohusu Mwanafunzi**

Sababu zilizotolewa na walimu ambazo hufanya insha za wanafunzi kutokuwa na mshikamano ni; kutoelewa swali vizuri, kutumia msamiati usiofaa, ukosefu wa makini wanapoandika, kujibu kwa haraka, ukosefu wa mazoezi mengi na ukosefu wa maelezo kutoka kwa walimu. Hata hivyo, wengi wa walimu walielekea kusisitiza sababu ya kutoelewa swali vizuri (asilimia 67).

Nusu ya walimu (50%) walitoa changamoto ya wanafunzi kutopenda insha na uandishi kwa jumla katika mazingira ya darasani huku asilimia 16 ikionyesha changamoto ya Sheng'. Wanaposahihisha, asilimia 50 ilionyesha changamoto ya makosa ya sarufi na hijai huku asilimia 33 wakiwa na changamoto ya hati isiyosomeks vizuri na asilimia17 walionyesha changamoto ya wanafunzi kuandika insha fupi.

Wanafunzi wakizoeshwa utunzi, ari ya kuandika insha itaibuliwa na makosa mbalimbali yatapungua. Hati nayo ni muhimu kwa kumpa msomaji hamu ya kutaka na kuendelea kusoma kazi. Mwanafunzi anafaa asirembeshe hati na azingatie sauti za chini na za juu. Aidha, anadhifishe kazi. Kulingana na mwongozo wa kudumu wa kusahihisha insha wa KNEC, insha kamili inafaa iwe

kati ya maneno 375-400. Insha robo (0-174) ina upeo wa alama tano, nusu (175-274) upeo wa alama kumi, robo tatu (275-374) upeo wa alama 15 na hatimaye 375-400 (kamili) husahihishwa kwa alama 20.

### 4.3 Ukaguzi wa Madaftari ya Insha za Wanafunzi

Katika kuchunguza uzoefu wa wanafunzi wa kuandika insha, vitabu vya wanafunzi vilichunguzwa. Katika kufanya hivi, mihimili ya maana tambuzi na maana matinishi ya SAM ilitumiwa. Mhimili wa maana tambuzi huwakilisha uwezo wa msemaji wa kung'amua mambo. Kitengo hiki cha maana hubeba maudhui na ujumbe katika lugha. Mhimili huu ulitumiwa kutathmini maudhui au mambo muhimu katika insha za wanafunzi. Mhimili wa maana matinishi hurejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa mawasiliano ya lugha. Hii humilikiwa na msemaji kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha wa lugha. Mhimili huu ulitumiwa katika kupima usarufi katika insha zao. Usarufi huu ndio ulitumiwa kupima kama mwanafunzi ametuzwa kulingana na utendaji wake katika insha. Yafuatayo yalijitokeza; Mwanafunzi alituzwa alama 20 kwa 20 na alikuwa makosa mengi ya mshikamano na insha ilikuwa na maneno mia moja badala ya maneno mia nne kama inavyopendekezwa na Taasisi ya Usahihishaji wa Mitihani. Baadhi ya shule hufunza somo la insha kuliko zingine. Idadi ya juu ya insha zilizofunzwa ilikuwa 45 na ya chini insha 5.


Aidha, insha chache zilisahihishwa na walimu huku shule moja kwa sita ikiruhusu wanafunzi kuhusika katika kusahihisha insha darasani lakini bila mwongozo wa

kudumu. Baadhi ya insha zilisahihishwa kwa alama 30 huku zingine kwa alama 20. Kwa hivyo, maudhui ya ukosefu wa usawa katika muktadha wa upeo wa usahihishaji yalijitokeza.

Alama anazotiliwa mwanafunzi ni muhimu kwa sababu humfanya mwanafunzi kutathmini ikiwa ameafikiana na azimio lake katika somo husika au la. Aidha, humsaidia katika kuibua mikakati itakayomsaidia awe bora. Utafiti huu uligundua kuwa insha za wanafunzi zilisahihishwa lakini mwanafunzi hakutiliwa alama. Baadhi ya insha zilitiliwa alama potoshi! Kwa mfano, insha moja ilituzwa alama 12 badala ya 9 na nyingine ikatuzwa alama 20 badala ya 5; alama 3 na 15 zaidi mtawalia. Isitoshe, baadhi ya insha hazikuwa na alama yoyote ila mkwaju tu kando kando ya insha, ishara kuwa zimepitiwa. Insha zingine hazikuwahi kupitiwa. Mwisho, baadhi ya walimu walitoleshea wanafunzi nakala za aina mbalimbali za insha kutoka vitabu teule na kuwaambia wabandike nakala hizo katika vitabu vyao.

Chati ifuatayo inaonyesha viwango vya usahihishaji wa vitabu vya insha za wanafunzi.

**Chati 4.1: Chati ya Usahihishaji wa Vitabu**




Asilimia iliyochukua nafasi kubwa ni ile ya insha chache zilizosahihishwa na walimu. Utiaji wa mkwaju kuonyesha kuwa kazi imepitiwa lakini bila alama na insha chache zilizosahihishwa zilichukua asilimia 80. Insha zilizosahihishwa bila kuonyesha alama zilichukua asilimia 60. Pongezi bila alama na alama potoshi zilichukua asilimia 40. Asilimia ya chini ilichukuliwa na hali ya walimu kutoleshea wanafunzi nakala na tofauti kwa upeo wa utuzaji ambayo ni asilimia 20. Hili linamaanisha kuwa baadhi ya walimu wanahitaji kukumbushwa kuhusu mbinu mwafaka za kufunza na kusahihisha insha.

Ukaguzi wa vitabu ulichangia sana katika kutathmini chanzo cha wanafunzi kuandika tungo hafifu.

Maudhui yanayohusiana na chanzo cha ukosefu wa mshikamano kulingana na data ya utafiti ni kama yafuatavyo;

i) Wanafunzi Kutosahihishiwa Kazi

Insha nyingi za wanafunzi hazikuwa zimesahihishwa. Badala yake, alama ya mkwaju ilitiwa kando kando ya kazi kuonyesha kuwa kazi imepitiwa.

ii) Mwelekeo Hasi

Walimu walisitiza kwamba wanafunzi wana mwelekeo hasi katika utunzi kwa jumla. Somo la insha huwa ni kama mzigo kwao. Kwa sababu hii, wanafunzi walikosa kufanya mazoezi ya kutosha. Hata hivyo, utafiti ulibainisha kwamba walimu wana mwelekeo hasi vilevile katika kulifunza na kusahihisha somo la insha.

iii) Kushirikisha Mwanafunzi Isivyofaa

Utafiti uligundua kuwa baadhi ya shule hushirikisha wanafunzi katika usahihishaji wa insha darasani lakini bila mwongozo wa kusahihisha uliokubalika na KNEC. Kwa hivyo, mbinu isiyofaa ilitumika na hatimaye kukosa kuelekeza mwanafunzi ipasavyo kuhusu kiwango chake cha utunzi.

iv) Kuandika Vielelezo kutoka Vitabuni

Vielelezo kutoka vitabu vya insha vilivyoandikwa na waandishi mbalimbali vilipewa wanafunzi ili waviandike katika vitabu vyao vya insha. Mbali na baadhi

ya insha hizi katika vielelezo kukosa kuwa kamili, pia zilimkosesha mwanafunzi nafasi ya kutunga yake. Utafiti huu uligundua kuwa baada ya hawa wanafunzi kuvihamisha vielelezo hivyo katika vitabu vyao, baadhi yao hawakutunga tungo zao kwa kutumia vielelezo hivyo. Walihitajika kuvisoma vielelezo hivyo kwa ajili ya mtihani. Jambo hili huwafanya wanafunzi kuwa wazembe na upevu wa utunzi kwao huathiriwa pakubwa.

v) Kutotiliwa Alama katika Kazi yao

Baadhi ya insha zilisahihishwa lakini hazikukadiriwa kwa alama. Mwanafunzi katika hili, hawezi kujua uwezo wake. Insha zingine zilitiwa alama zinazopotosha mwanafunzi kuhusu kiwango chake. Kwa mfano, mwanafunzi alikuwa ametiliwa alama 15 badala ya alama 5 na mwingine alama 12 badala ya alama 9. Isitoshe, baadhi ya insha zilikuwa na pongezi bila alama. Baada ya mwalimu kusahihisha kazi, wachache walisahihisha makosa darasani. Mwanafunzi anapopongezwa bila alama, pongezi ya aina hii humkosesha mwanafunzi dira mwafaka ya utunzi. Jukumu mojawapo la pongezi ni kumfanya mwanafunzi afahamu anakotoka (umilisi wake) na anaazimia wapi au nini.

vi) Athari ya lugha ya Kwanza

Athari ya lugha ya kwanza iliwafanya wanafunzi wafasiri visivyo na kuyafanya makala kukosa mantiki. Kwa mfano, *chapta* badala ya *sura* na *kionyeshi* badala ya *ishara*. Mifano zaidi ni kama vile tulipakiwa (parked), tuliwahisia (we felt for them), Alifunguka (became open), boeka (get bored), baiwa ( to be bought for) na

demu (dam). Mhimili wa SAM uliotumiwa hapa ni wa maana matinishi. Mhimili huu hurejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa mawasiliano ya lugha. Hii humilikiwa na msemaji kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha wa lugha. Katika kuutumia, ilibainika kuwa fasiri zilizotolewa kama mifano hapo juu hazikuwa sawa kisarufi.

vii) Mbinu za Kufundishia

Asilimia mia kwa mia ya walimu waliojibu maswali katika hojaji walitumia mbinu ya maelezo darasani. Maelezo haya hutumiwa kufafanua aina mbalimbali za insha. Mbinu ya maelezo bila kumhusisha mwanafunzi humpendelea mwalimu kuliko mwanafunzi. Kumhusisha mwanafunzi husaidia katika kutathmini ikiwa mwanafunzi ameng'amua analofunzwa na kiasi cha ung'amuzi huo.

viii) Haraka ya kujibu maswali

Pia, ilibainika kwamba wanafunzi hukosa makini katika kuchunguza mahitaji ya swali na hulijibu kwa haraka. Kasi ya kujibu maswali husababisha wanafunzi kukosa kufuata maagizo katika kujibu. Ukosefu wa kufuata maagizo husababishia mwanafunzi hali ya kujibu swali visivyo au kupotoka kabisa.

ix) Kuchanganya Kazi

Wanafunzi waliyaandika maelezo ya insha pamoja na maelezo ya masomo mengine kama vile, Kemia, Fizikia na Somo la Dini. Hali hii iliwafanya

wanafunzi kutatiza usomaji na udurushaji wa insha zao kwa sababu ya kupoteza muda katika kuzitafuta insha hizo miongoni mwa kazi zingine. Maelezo ya insha yakiandikwa pamoja, mtiririko wa kile anachosoma mwanafunzi hukuzwa mbali na kurahisisha uelewa wake. Anapochanganya kazi, katika harakati ya kutafuta kile anachotaka kusoma, anaweza kuvutwa macho na kile kinachohusiana na somo lingine na kwa njia hii mtiririko wa kile alichokuwa anasoma huathiriwa na hata kusababisha usahaulifu.

x) Kukosa Uhakika

Baadhi ya insha za wanafunzi zilionyesha hali hii. Kwa mfano, mwanafunzi anatumia kiambishi kile kile vizuri na vibaya katika sentensi moja. Kwa mfano 'Ha*u*kupita hata siku moja kwa vile kazi ilianza siku *i*liyofuata'. Hapa mihimili ya umilisi na utendaji wa Sarufi Zalishi ilitumiwa. Mwanafunzi anang'amua kuwa anachorejelea ni siku (umilisi) japo anakosa uhakika kwacho. Kwa hivyo, anaelekea kufanya makosa katika matumizi (utendaji) katika mojawapo ya kirejeshi – *u*.

Uhakika katika utunzi wa insha husaidia katika kukuza maudhui katika muktadha wa mshikamano kwa njia ifuatayo; husaidia katika kutambua wazi kile kinachorejelewa katika usemi. Aidha, husaidia katika kuonyesha kinachotiliwa mkazo, hadhi na kazi ya viunganishi, kilichodondoshwa na vibadala katika usemi.

xi) Matumizi ya sheng'

Maneno ya lugha ya Sheng' yaliyojitokeza katika insha za wanafunzi yalidhihirisha kwamba baadhi ya wanafunzi hawatambui mpaka kati ya maneno hayo na Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, lugha hii ilionekana kuharibu ubora wa insha za wanafunzi. Msingi mwafaka wa Kiswahili hasa wa msamiati ni muhimu katika kumbainishia mipaka mwafaka kati ya Kiswahili na lugha nyinginezo. Bila mpaka wa aina hii, mshikamano hasa wa kileksia huathirika pakubwa. Kwa mfano, matumizi ya sinonimu, homonimu, hiponimu na meronimu yatapotosha kwa ukosefu wa mpaka wa aina hii.

xii) Silabasi Pana

Walimu walisema kuwa wao hukosa muda wa kusahihisha na kurekebisha insha darasani kwa sababu ya vipindi vichache vya somo la Kiswahili. Wanaelekea kuwa na vipengele vingi vya kushughulikiwa lakini kwa muda mchache. Silabasi ikiwa pana na vipindi vichache vitengewe somo la Kiswahili, inamaanisha kuwa baadhi ya vipengele katika somo hilo havitashughulikiwa kwa ukamilifu na kwa ubora unaostahili.

xiii) Mahudhurio Haba ya Wanafunzi

Mahudhurio haba ya wanafunzi yalidhihirika katika shule za kutwa. Wanafunzi walikosa kuenda shuleni kwa sababu au bila sababu yoyote. Wanafunzi waliokosa shuleni mara nyingi, walielekea kufunzwa mara chache kuliko wenzao waliohudhuria mara nyingi. Hali hii iliwafanya wanafunzi kutopata mwelekeo sawia. Kutokana na utafiti, wale waliohudhuria, walifanya mazoezi machache kwa sababu zilizotajwa tayari. Hili lilimaanisha kuwa, wale waliohudhuria vipindi vichache, walikuwa na uwezekano wa kuathirika hata zaidi katika upande wa mazoezi hayo.

### 4.4 Namna ya Kuboresha Mshikamano

Asilimia 83 ya walimu waliojaza hojaji walitoa mapendekezo yafuatayo;

i) Mazoezi Zaidi kupewa wanafunzi ili waweze kuboresha mshikamano katika kazi yao. Aidha, mazoezi mengi yatawasaidia katika kuwa na tajriba pana kuhusu masuala ibuka ambayo huweza kuwaongoza wanapoandika.

ii) Mwanafunzi kuwa na uhakika wa kile anachoshughulikia na kuandika. Hili litasaidia kudumisha uwiano katika kategoria zote za mshikamano.

iii) Haja ya mwanafunzi kufuata maagizo ili asipotoke katika maudhui yake.

iv) Uakifishaji wa kazi ipasavyo ili mshikamano katika kishazi uweze kuimarishwa.

v) Vipindi vya Kiswahili viongezwe ili mazoezi zaidi yafanikishwe na walimu wapate muda wa kulishughulikia somo hilo kwa ukamilifu.

vi) Mtaala upunguzwe kwani ni mpana mno. Hili litasaidia walimu na wanafunzi katika kuboresha vipengele vingi vya sarufi kwani ndivyo mwanafunzi hutumia katika uandishi wake wa insha.

vii) Upatanisho mzuri wa sentensi utiliwe maanani ili maana kusudiwa isipotoshwe.

Aidha, Asilimia 17 ya walimu waliojaza hojaji walipendekeza yafuatayo;

i) Wanafunzi kutathmini maneno makuu katika swali ili yawaongoze wasipotoshe mshikamano katika uandishi husika.

ii) Haja ya wanafunzi kusaidiwa katika kupenda uandishi wa insha na uandishi kwa jumla labda kupitia kwa tuzo.

iii) Wanafunzi waepuke kutumia lugha ya Sheng' katika tungo zao kwa sababu huathiri ubora wa kazi ya uandishi.

iv) Wanafunzi wasome kwa mapana ili waepuke tatizo la tafsiri sisisi na athari ya lugha ya kwanza.

Wanafunzi wanapofanyishwa mazoezi mengi, uzoefu wao wa kuandika huimarika. David (2003) anasisitiza wazo hili lakini anatoa kanuni tatu ambazo zinastahili ziongoze uandishi; mwalimu anafaa ajue sababu za wanafunzi kuandika. Maazimo ya mwanafunzi katika muktadha huu yanastahili yawiane na ya mwalimu. Aidha, mwalimu anafaa ampe mwanafunzi uwanja mpana wa

uandishi. Katika muktadha wa shule za upili, insha za kiuamilifu na zile za kawaida zinaweza kufanyiwa mazoezi. Mwisho, kama Hounsell (2008), anapendekeza mwalimu kuripoti kwa wanafunzi baada ya kusahihisha kazi yao. Hili linamsaidia mwanafunzi kujua makosa yao na kutorudia makosa hayo katika uandishi wa baadaye. Hata hivyo, anaelekeza kuwa walimu wawe makini wanapotuza wanafunzi; walimu wanafaa waandike maneno kwa ukamilifu na asitumie alama ya kiulizi (?) kwa yale yasiyoeleweka kwani huashiria ukali.

Maneno makuu ni muhimu kwani humwongoza mwanafunzi namna atakavyojibu. Maneno haya ndiyo huwa nguzo muhimu katika kumwongoza mwanafunzi katika ufafanuzi wake wa maudhui. Umakini ukikosa katika hili, basi upotoshi na ukosefu wa mshikamano hutokea.

Aidha, kuna baadhi ya maswali ambayo huwa na maswali mawili katika swali moja. Mwanafunzi asiposoma kwa makini, ataelekea kujibu ama sehemu moja pekee ya swali au apotoke kabisa. Kwa mfano, 'Jadili chanzo cha ukosefu wa amani katika nchi zinazoendelea huku ukitoa suluhu.' Katika swali hili, sehemu ya kwanza inamhitaji mwanafunzi atoe chanzo cha ukosefu wa amani huku sehemu ya pili atoe suluhu.

Kutokana na maoni ya walimu, Sheng' huathiri ubora wa kazi kwa kiasi kikubwa maoni ya. Hili linaungwa mkono na Apondi (2013) anaposema kuwa matumizi ya Sheng' yamelaumiwa na walimu wengi katika shule za msingi na zile za upili

kuwa ni sababu mojawapo kuu ya kushuka kwa matokeo ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Sheng' imelaumiwa kwamba, inasababisha wanafunzi kutozingatia mafunzo ya kanuni za sarufi na tahajia au maendelezo. Jambo hili limetokea kwa sababu Sheng' imejitanzua kutoka hali ya kuwa kilugha cha maongezi pekee na sasa kinatumiwa na baadhi ya waandishi wa vitabu. Aidha, vyombo vya habari kama redio, televisheni na magazeti vinaendeleza mawasiliano kwa matumizi ya Sheng'. Kwa hivyo, mwanafunzi asipokuwa makini, anaweza kukosa kutambua mpaka kati ya Sheng' na Kiswahili.

Licha ya lugha ya Sheng' kuchangia kuunda msamiati ambao unatumika katika lugha ya Kiswahili, ina hasara kubwa ya kutumia baadhi ya majina ya Sheng' ambayo yanapotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili. Aidha, lugha ya Sheng' inaweza kuwafanya watu waache kuyatumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhania ni Sheng. Baadhi ya maneno hayo ni kama vile 'manzi' ambalo ni neno la Kiswahili sanifu kumaanisha msichana ila wengi hulitumia kama Sheng'. Pia, 'Ashara' kumaanisha idadi kumi.

Kuhusu mtaala, ni muhimu mwalimu ajitahidi katika kufanikisha utekelezaji wa silabasi husika. Hili linaungwa mkono na Bishop (1985) anayesema kwamba ubora wa silabasi ni utekelezaji wake wala si tu uzuri wa yaliyomo. Hili humtegemea mwalimu kwa kiasi kikubwa (Benaars, Otiende na Boisvert, 1994).

Hata hivyo, walimu hawakuweza kufanya utekelezaji huu kwa sababu ya upana wa silabasi na muda uliotengewa Somo la Kiswahili kwa jumla.

Mazoezi mengi yatasaidia kuimarisha mshikamano miongoni mwa wanafunzi na kuwezesha mwalimu na mwanafunzi mwenyewe kugundua kiwango cha mwanafunzi husika. Katika kufanikisha hili, Lawton (1973) anapendekeza kwamba ili kutathmini viwango mbalimbali vya wanafunzi na uwezo wao wa kuandika, ni sharti mwalimu atumie takisonomia za malengo alizoasisi Bloom (1956); ujuzi, ufahamu, uwekelevu, uchanganuzi, usanisi na tathmini. Kiwango cha ujuzi huhusisha kukumbuka. Mwanafunzi anafaa akumbuke sura ya insha za kiuamilifu kwa sababu huwa za lazima. Kitengo cha ufahamu kitamfaa kufasili swali ili kujua matakwa yake. Uwekelevu husaidia katika kutabiri matokeo kutokana na aliyofunzwa. Uchanganuzi kwa upande mwingine utasaidia kudumisha hatua mbalimbali za insha; utangulizi, mwili na hitimisho kutegemea aina ya insha. Usanisi humsaidia katika kuunda kisa au mawazo yaliyo na mshikamano. Hatimaye, tathmini humsaidia katika kujua kiwango chake. Kwa hivyo, takisonomia hizi zinaweza kutumiwa ama na mwalimu (anapofunza na kuwapa wanafunzi zoezi) au na mwanafunzi mwenyewe kwa usaidizi wa mwalimu.

Kutokana na majibu ya hojaji, mbinu tegemezi mwalimu ndiyo ilitumika sana; mbinu ambayo inampa mwalimu nafasi kubwa. Walimu walitumia maelezo (mhadhara) kuliko kuwahusisha wanafunzi zaidi. Mbinu hii, mbali na kumfanya

mwalimu kuchukua nafasi kubwa katika ufunzaji, humfanya mwanafunzi kumtegemea mwalimu kwa kila kitu. Aidha, makosa ya mshikamano ya mwanafunzi yatahusishwa na mwalimu kwa sababu mara nyingi mwanafunzi ataiga anachosema mwalimu. Ogalo (2010) anapendekeza matumizi ya mbinu tegemezi mwanafunzi (mbinu inayompa mwanafunzi nafasi kubwa) ili imsaidie mwanafunzi kujifunza zaidi na kupenda somo. Mbinu hizi ni kama; vikundi vya mjadala, tafakuri husishi (maswali ya papo hapo), kazi mradi (maswali na majibu kutolewa baadaye), maigizo, maswali na majibu na matumizi ya vifaa. Kwa mfano, mwanafunzi kuandika kielelezo ubaoni.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imeangazia chanzo cha makosa ya mshikamano katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne na namna ya kuuboresha. Ilibainika wazi kwamba mwanafunzi na mwalimu wana mchango mkubwa katika kuboresha mshikamano na matokeo ya insha kwa jumla. Mwanafunzi anastahili awe makini anapofunzwa na anapofanya mtihani. Mwalimu anafaa ashughulikie tofauti za wanafunzi mbalimbali anapofunza, kusahihisha na hatimaye kurekebisha kazi. Ni jukumu la mwalimu na mwanafunzi kuboresha mshikamano awezavyo. Sura ya tano itashughulikia hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti huu kitaaluma na mapendekezo kutokana na utafiti na kwa ajili ya tafiti za baadaye.

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulinuia kubainisha nafasi ya mshikamano katika kukuza maudhui katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne katika kaunti ya Murang'a. Dhamira kuu ilikuwa ni kubainisha chanzo cha makosa au matatizo ya mshikamano na namna ya kuweza kuuboresha. Utafiti ulihusisha mbinu za utafiti za maktabani na vilevile nyanjani. Kabla ya kuenda nyanjani, mtafiti aliandaa sura ya kwanza ya utafiti maktabani kwa kuandika usuli wa utafiti, swala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu za kuchagua mada na misingi ya nadharia katika kuipa kazi mwelekeo. Sura ya pili ilishughulikia maelezo kuhusu vipengele vya mshikamano na namna

vilivyokuzwa katika insha za wanafunzi. Sura ya tatu imeshughulikia namna vipengele vya mshikamano vimelemazwa. Sura ya nne ilishughulikia chanzo cha makosa ya mshikamano na jinsi ya kuuboresha. Hatimaye, sura ya tano imeshughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti kitaaluma na mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye. Katika kufanikisha matokeo, malengo ya utafiti huu yalitiliwa mkazo kama ifuatavyo;

### 5.1.1 Lengo la Kwanza

Lengo la kwanza lilikuwa kutathmini namna vipengele vya mshikamano vilivyokuzwa katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne. Lengo hili limeshughulikiwa katika sura ya pili. Katika kufanya hivi, insha za wanafunzi zilichunguzwa na zoezi kutolewa ili kutathmini umilisi na utendaji wao wa vipengele vya mshikamano vifuatavyo; urejeshi, uunganishaji, ubadilishaji, udondoshaji na leksia.

### 5.1.2 Lengo la Pili

Lengo la pili lilikuwa kubainisha namna vipengele vya mshikamano vilivyolemazwa katika insha za wanafunzi wa kidato cha nne. Hili nalo limeshughulikiwa katika sura ya tatu. Ulemavu huu ulipimwa katika miktadha kama inavyojitokeza katika matokeo ya utafiti huu. Mhimili uliotumiwa katika kufanya hivi ni mhimili wa maana matinishi wa SAM.

### 5.1.3 Lengo la Tatu

Lengo hili lilidhamiria kubaini chanzo cha makosa ya mshikamano. Hili limeshugulikiwa katika sura ya nne. Madaftari ya insha ya wanafunzi yalikaguliwa ili kutathmini mazoea yao ya kutumia vipengele vya mshikamano na uandalizi wao wa uepukaji wa makosa yanayohusiana na mshikamano. Kutokana na ukaguzi wa vitabu vya wanafunzi na hojaji, ilibainika kuwa chanzo cha makosa haya ni mwalimu na mwanafunzi. Walimu walitumia mbinu zisofaa katika ufunzaji na usahihishaji wa insha. Wanafunzi nao hawakupenda somo la insha kwa jumla.

### 5.1.4 Lengo la Nne

Lengo hili lilikuwa kuonyesha namna ya kuboresha mshikamano katika kazi ya wanafunzi. Lengo hili limeshughulikiwa katika sura ya nne. Walimu katika majibu yao ya hojaji walisisitiza umuhimu wa mshikamano katika insha za wanafunzi huku wakipendekekeza namna mshikamano huo unavyoweza kuboreshwa.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yamepatikana kutokana na uchanganuzi wa insha za wanafunzi wa kidato cha nne, zoezi la vipengele vya mshikamano, ukaguzi wa vitabu vya insha za wanafunzi na hojaji zilizojazwa na walimu.

Ili kutathmini ukuzaji wa vipengele vya mshikamano, vipengele hivyo vilichanganuliwa kwa kufuata misingi ifuatayo; urejeshi, uunganishaji

ubadilishaji, udondoshaji na leksia. Nadharia iliyotumiwa ni Sarufi Zalishi, mihimili ya utendaji na umilisi.

Kuhusu urejeshi, ilibainika kwamba mrejeo nje haukutumiwa sana na wanafunzi. Wanafunzi walitumia nafsi ya tatu zaidi kuliko ya pili na ya kwanza huku ya pili ikichukua nafasi ya chini kwa zote (asilimia 32.5). Kwa upande wa viashiria, viashiria vya kati ndivyo vilitumika zaidi. Isitoshe, vilinganuzi vilivyotumika sana ni vya mzizi wa –ingine kubainisha dhana za tofauti na, kando na, mbali na, zaidi ya na baadhi ya.

Mshikamano wa kuunganisha uliweka wazi kutozoea kwa wanafunzi katika kutumia viunganishi vya uteuzi. Ilibainika kutoka insha za wanafunzi kuwa asilimia 100 ilitumia viunganishi vya kuongeza, vya wakati asilimia 72.5, visababishi asilimia 55, vya uteuzi asilimia 20, vinyume asilimia 53.3 na viendelezo asilimia 39.2. (Taz. Chati 2.1). Mshikamano wa ubadilishaji ulichukua asilimia 18 na ule wa udondoshaji asilimia 13 ya jumla ya wanafunzi. Kutokana na zoezi hilo, wanafunzi walionyesha kutozoea kwao katika kutumia mshikamano wa udondoshaji na ubadilishaji. Hiki ni kipengele kinachostahili kutafutiwa suluhisho. Aidha, matumizi ya mshikamano wa kileksia ulionyesha matumizi mengi ya urudiaji zaidi ya vipengele vya mfumo maana na uhusiano-leksika.

Ili kutathmini namna vipengele vya mshikamano vilivyolemazwa, au makosa ya mshikamano katika insha hizi, mhimili wa maana matinishi wa Sarufi Amilifu Mfumo ulitumiwa ili kutathmini usarufi katika tungo za wanafunzi. Makosa

yanayohusiana na mshikamano pekee ndiyo yaliangaziwa na kuainishwa katika makundi mbalimbali; makosa ya upatanisho wa kisarufi, makosa ya kileksia, makosa ya viunganishi, makosa ya tafsiri isiyofaa, makosa ya urudiaji, makosa ya vilinganuzi, makosa ya urejeshi, makosa ya vimilikishi, Makosa ya nafsi, makosa ya udondoshaji, makosa ya sentensi na makosa katika tungo.

Ilibainika kuwa makosa ya upatanisho wa kisarufi na ya sentensi ndiyo yalifanywa sana na wanafunzi zaidi huku yakichukua asilimia 18 na 19 mtawalia ya jumla ya makosa. Makosa ya kileksia yalichukua asilimia 10. Asilimia 43 ya wanafunzi walifanya makosa ya viunganishi.

Makosa ya urejeshi ndani na nje yalijitokeza huku ya mshikamano dokezi yakiwa nadra. Makosa haya yalihusu matumizi mabaya ya virejeshi 'amba' na 'o' pamoja na matumizi ya mzizi –enye (asilimia 27). Hata hivyo, utafiti ulibainisha kuwa makosa ya viashiria na vilinganuzi si vyanzo vikuu vya ukosefu wa mshikamano katika insha za wanafunzi. Asilimia ya makosa ya viashiria ilikuwa 6 na ya vilinganuzi 2. Asilimia ya wanafunzi waliofanya makosa yanayohusiana na viunganishi ni 43.

Aidha, asilimia ya wanafunzi waliofanya makosa ya kileksia ni 38 huku asilimia 22 ikidhihirisha makosa ya urudiaji. Makosa ya vimilikishi yalichukua asilimia 5 ya jumla ya makosa huku asilimia 18 ya wanafunzi wakiyafanya. Makosa mengi yalishuhudiwa katika shule za kibinafsi na za wilaya. Isitoshe, asilimia 13 ya wanafunzi walifanya makosa ya nafsi huku wengi wakitoka shule za kibinafsi na

wilaya. Asilimia 6 walitafsiri na kutohoa moja kwa moja kutoka ama lugha ya kwanza au Kiingereza.

Kutokana na insha waliyoifanya wanafunzi, walithibitisha dai la walimu la wanafunzi kukosa mshikamano kwa sababu ya kutosoma kwa upana ; ndiposa walifanya makosa mengi katika sentensi na upatanisho wa kisarufi kwa jumla. Wengi pia wanakosa kufuata maagizo. Kwa hivyo, wanapofanya kazi, hawatiririshi namna wanavyostahili kufanya.

Pia, sababu zingine ya ukosefu wa mshikamano katika insha za wanafunzi zilibainika kutokana na hojaji walizojaza walimu wanaofunza kidato cha nne na ukaguzi wa madaftari ya insha za wanafunzi.

Hojaji zilichanganuliwa kwa kufuata vigezo vifuatavyo; Mbinu za kufunzia insha, viunganishi na msamiati, changamoto wakati wa kufunza na kusahihisha darasani, kiwango cha wanafunzi, na muda wa kufunza na kusahihisha insha. Sababu za ukosefu wa mshikamano kulingana na majibu ya walimu ni: silabasi pana, matumizi ya Sheng', kuchanganya kazi, kukosa uhakika, haraka ya kujibu swali, wanafunzi kutosahihishiwa kazi, wanafunzi kuwa na mwelekeo hasi, kushirikisha wanafunzi isivyofaa, kutoleshea wanafunzi nakala za insha, athari ya lugha ya kwanza, mbinu ya mwalimu ya kuchukua nafasi kubwa katika ufunzaji na ujifunzaji kuliko mwanafunzi na mahudhurio haba ya wanafunzi.

Kwa jumla, ilibainika kuwa mwalimu pamoja na mwanafunzi wanachangia katika ukosefu wa mshikamano. Mbinu mwafaka inastahili kutumiwa katika ufunzaji na

ujifunzaji ili kuwafanya wanafunzi kuzoea utunzi. Kwa mfano, mbinu ya wanafunzi kujisahihishia kazi bila mwongozo ni suala linalostahili kuangaliwa kwa jicho pevu.

## 5.3 Changamoto Wakati wa Utafiti

Licha ya utafiti huu kufaulu kwa kiasi kikubwa, ulikumbwa na changamoto si haba. Kwanza, matini nyingi zinazohusu mshikamano zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Hili lilipelekea kufanya tafsiri kila mara taarifa fulani ilipohitajika; jambo lililogharimu muda na makini mno kutoka kwa mtafiti. Aidha, baadhi ya walimu walikuwa na vikwazo kabla ya kujaza fomu. Waliomba wanafunzi ama watuzwe au wazungumziwe kitahini kabla ya mtihani wowote. Ili kufanikisha utafiti huu, wanafunzi katika baadhi ya shule walielekezwa namna ya kuandika insha bora na insha ambazo zilikuwa zimeandikwa zikatuzwa, kulingana na mwongozo wa kudumu wa insha wa Taasisi ya Usahihishaji wa Mitihani.

Dhana ya kupoteza wakati ilikuwa changamoto katika shule za kitaifa. Mtafiti anapewa miadi ambayo haitimizwi na washikadau. Hili lilipelekea utafiti kufanywa wakati wa usiku katika baadhi ya shule za kitaifa.

Isitoshe, uchanganuzi wa matini ulihitaji makini, ili kutofautisha dhana ya mshikamano na muwala ambazo zina uhusiano wa karibu.

Baadhi ya shule za wilaya hazikufikika kwa urahisi kwa sababu ya hali ya barabara; ilimgharimu mtafiti pesa nyingi kufika hapo.

## 5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti huu

Somo la Kiswahili likiwa somo la lazima katika mtaala wa elimu, linafaa lichukuliwe kwa uzito unaostahili. Hili pia linafaa hata zaidi ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya.

Ilibainika wazi kuwa sababu kuu ya ukosefu wa mshikamano katika kazi ya wanafunzi ni wanafunzi na walimu. Walimu wanafaa wakumbushwe umuhimu wa somo hili kupitia warsha mbalimbali ili kuwe na njia sawia ya kufunza na kutuza. Jambo hili litasaidia kupunguza au kuondoa kabisa hali ya kwa mfano, walimu wengine kutuza insha kwa upeo tofauti na wengine.

Isitoshe, walimu wanafaa wawadhihirishie wanafunzi uwezo wao mapema ili mwanafunzi aandike akiwa na nia ya kujiboresha katika tungo za baaadaye. Hali ya kuwa mwalimu ametia mkwaju nyuma ya kazi ya mwanafunzi au kumpa pongezi bila alama inapotosha mwanafunzi na hataweza kujiboresha vilivyo.

Walimu wanafaa wadurusu kazi ya mwanafunzi baada ya kuisahihisha. Kwa kufanya hivi, mwanafunzi hatarudia makosa yake katika tungo zake za baadaye. Asilimia 83 ya walimu hawakurudia kazi darasani baada ya kusahihisha.

Umakinifu pia unahitajika katika upande wa mwalimu asije akashughulikia wanafunzi wachache tu darasani. Wazo kuwa baadhi ya walimu husahihisha darasani kutegemea viwango (chini, kati na juu) linastahili liangaliwe kwa umakini mno ili wengine wasipatikane katika hali kuwa kazi yao haijawahi kusahihishwa darasani kwani kuna huo uwezekano. Labda mwalimu anaweza kuwa na rekodi ya kuonyesha yule ambaye kazi yake imesahihishwa na yule bado.

Mashindano kupitia kwa vyombo vya habari yamechangia matokeo mazuri ya Kiswahili lakini kwa walioshiriki tayari; ni muhimu wanafunzi kupitia kwa walimu na washikadau wengine wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mashindano haya katika harakati ya kuibua ari ya kupenda utunzi miongoni mwa wanafunzi. Aidha, ari hii inaweza kuibuliwa na walimu katika kiwango cha shule. Wanafunzi wanaweza kushindana miongoni mwao na mshindi akatuzwa na kwa njia hii, wengi wataenzi utunzi kwa jumla.

Wanafunzi kwa upande mwingine, wanafaa watambue msemo wa ‘kikulacho ki nguoni mwako’ ili wafanye juhudi ya kutojidhuru wenyewe. Wanafunzi wanafaa wamakinike wanaposoma na kujibu swali kwa kuangalia nguzo za swali kimaneno ili wasikose kushikamanisha kazi. Aidha, wajifunze kutumia mitindo

ya lugha inayofaa ili wakuze mshikamano wa kileksia; Sheng' itofautishwe na Kiswahili ili wasije wakachanganya lugha hizi mbili visivyo.

Kadhalika, wanafunzi wanaweza kujifunza kujirekebisha wenyewe. Linalotatiza, wampelekee mwalimu kwa mwongozo zaidi. Katika kufanya hivi, uelewa wao wa vipengele mbalimbali huimarika. Hata hivyo, hili halitafaa wanafunzi wa viwango vyote.

Silabasi ya Kiswahili kwa jumla ni pana mno, jambo lililopelekea baadhi ya walimu kukosa muda wa kuwasahihishia wanafunzi insha zao. Matokeo ni kuwa wanafunzi hurudia makosa yale yale kila wakati; jambo ambalo huwachosha wanafunzi na kuwanyima ari ya kuandika. Ikiwa kuna baadhi ya vipengele vilivyozidi kiwango chao, vinafaa viondolewe. Kwa mfano, kipengele cha utafiti katika somo la Fasihi Simulizi.

### 5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Wataalamu wengine wanaweza kuangazia mshikamano wa kileksia na waonyeshe mpaka wazi kati ya nomino za kawaida na zile nomino katika tapo la uhusiano-leksika. Aidha, ruwaza za kileksia zinaweza kuangaziwa.

Kwa ambavyo utafiti huu ulihusu wanafunzi wa kidato cha nne pekee, utafiti unaotofautisha viwango vya chini na vya juu ni muhimu.

Aidha, chanzo cha ukosefu wa mazoea ya kutumia mshikamano wa udondoshaji na mrejeo nje ni suala linalofaa kuchunguzwa.

Suala la uhusiano kati ya muwala na mshikamano katika matini husika linaweza kuangaziwa na watafiti.

### 5.6 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti huu kitaaluma na mapendekezo kutokana na utafiti na kwa ajili ya tafiti za baadaye. Ni matumaini kuwa utafiti huu utawafaa walengwa; wanafunzi, walimu, watahini na watafiti wengineo.

## MAREJELEO

Allen, E.P. and Vallette, R.M. (1972). *Classroom Techniques: Foreign Language and English as a Second Language.* New York: Harcourt Brace Jovaniovich Inc.

Apondi, A. (2013, Septemba). Mustakabali wa Sheng’ ni Upi? *Taifa Leo*.

Beaugrande, R. and Dressler, W. (1981). *Introduction to Text Lingistics*. New York: Longman Group Limited.

Bennars, G. Otiende, J. na Bosvert, R. (1994). *Theory and Practice of Education*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Berzlánovich, I. Egg, M. & Redeker, G. (2008). Coherence Structure and Lexical Cohesion in Expository and Persuasive Texts. . *In A. Benz, P. Kühnlein & M. Stede (Ed,). Proceedings of the Workshop Constraints in Discourse III* (pp. 19-26). Potsdam, Germany, July 30 -August 1, 2008.

Bishop. G. (1985). *Curriculum Development: A textbook for Students*. London: Macmillan Education Ltd.

Brierley, S. (1995). *The Advertising Handbook*. London: Routledge.

Brown, G. and Yule, G. (1983). *Discourse Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bloom, B.S. (1956). *Taxonomy of Educational Objectives: The Classification of Educational Goals.* New York: Longman.

Candlin, E. (1952). *An English Course for Professional Students*. London: University of London Limited.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge Mass: MIT Press.

Chomsky, N. (1995). *Minimalist Programme*. Cambridge: MIT Press.

Crystal, D. (1981). *Direction in Applied Linguistics.* London: London Academic Press.

Crystal, D. (1988). *Rediscover Grammar.* UK: Longman.

David, N. (2003). *Practical English Language Teaching*. Mcgraw Hill Companies: USA.

Digolo, O.O. (1986). *Creative Arts Education*. Nairobi: Kenyatta University and University of London Institute of Education.

Edelsky, C. (1986). *Writing in a Bilingual Programme*. Norwood New Jersey: Abex Publishing Cooporation.

Fitzgerald, J. and Spiegel, D. (1981). *Textual Cohesion and Coherence in Childrens' Writing*. Research in the Teaching of English 20 (3).

Habwe, J. (1999). "Discourse Analysis of Political Speeches." Tasnifu ya Uzamifu ya chuo kikuu cha Nairobi.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M. A. and Hasan, R. (1976). *Cohesion in English*. New York: Longman Group Limited.

Halliday, M. (1984). *An Introduction to Functional grammar*. 2nd Ed. London: Edward Arnold.

Halliday, M. (1994). *An Introduction to Functional Grammar 3rd Ed*. London: Edward Arnold.

Halliday, M. (1997). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Arnold.

Halliday, M. and Mathiessen, C. (1999). *Construing Experience through Meaning.* London: Cassell.

Halliday, M. and Mathiessen, C. (2004). *An Introduction to Functional Grammar* (3rd Ed.). London: Arnold.

Hann, W. (1984). *Learning to Read and Write*. Gulford Surrey: Biddles L.T. D.

Hounsell, C. (2008). *Guidance and Feedfack*. Sydney: University of Western Sydney.

Hedge, T. (1988). *Writing*. Oxford: Oxford University Press.

Hope, J. and Write, L. (1996). *Stylitics*. London: Routledge.

Hymes, D. (1965). *Communicative Competence of Low Income Children: Assumptions and Programmes.* Report of Language Development Study Group: Ford Foundation.

Ipara, I. O. na Maina, G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford.

Jafarpur, A. (1991). Cohesiveness as a Basis of Evaluating Compositions. *In System,* Vol. 19, No. 4 pp.459-456. Great Britain: Pegamon Press.

Kapinga, M. C (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Karanja, (1993). “A Discourse Analysis of KBC TV Broadcast Discussion Programmes” Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kariuki, G. J. (2012). Makosa ya Kisintaksia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili za Wanafunzi wa Shule za Upili. M.A Thesis: Kenyatta University.

Kempson, R. (1977). *Semantic Theory.* London: Cambridge University Press.

Kihore, M. Y, Massamba, D.P. na Msanjila, Y.P. (2000). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Dares-salaam: TUKI.

Kinneavy, J. L. and Warriner, J. E. (1993). *Elements of Writing*. USA: Holt, Riinehart and Winson.

Kitsao, J. (1995). *Mbinu za Uandishi.* Nairobi: Oxford Publishing Press.

Kroll, B. (1990). *Second Language Writing*. Cambridge: Cambridge University Press.

Kuczaji, A. S.(1984).( Ed.). *Discourse Development Progress in Cognitive Development Research.* New York: Springer Verlag.

Labov, W. (1972). *Discourse Markers.* Cambridge: Cambridge University Press.

Lawton, D. (1973). *Social Change, Education Theory and Curriculum Planning.* London: University of London Press.

Leech, G. (1996). *English in Advertising: A Linguistic Study of Advertising in Great Britain.* London; Longman.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics.* Cambridge: The University Press.

Maina, R.W. (2011). “Mbinu za Mawasiliano katika Matangazo ya Runinga Nchini Kenya.” Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. haijachapishwa.

Matei, K. A. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili* Nairobi: Phoenix Publishers.

Martin, J. R. (1992). *English Text: System and Strucrure.* Amsterdam: Benjamins

Mathiessen, C. (2013). *Introduction to Functional Grammar*. New York Routledge.

Mbaabu, I. (1986). *Ukubalifu wa Msamiati kutoka Kenya*. Nairobi: Kenyatta University College.

Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longman.

Mclaughlin, B. (1987). *Theories of Second Language Acquisition Research and its Implication for Classroom*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili: Muundo na Matumizi yake*. Nairobi: Nairobi Intercontinental Publishers.

Mogambi, H. (2007). *Golden Tips Kiswahili*. Nairobi: Autolitho Ltd.

Mogere, G. N. (2013). "Teachers' Instuctional Strategies in Insha and their Influence on Class Seven Pupils Performance in Garrisa." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Morris, J. & Hirst, G. (2004). Non-Classical Lexical Semantic Relations. *In D. Moldovan & R. Girju (Eds.), Proceedings of the Workshop on Computational Lexical Semantics* (pp. 46-51). Boston, MA, USA, May 6, 2004.

Mutugu, B. N. (2001). "Makosa ya Kileksia katika Insha na Chanzo Chake ; Uchunguzi wa Shule Tano za Upili Wilayani Kiambu." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nasibi, W. M. (2003). *Instructional Methods: Teaching Across the Curriculum.* Nairobi: Nehema Publishers.

Norrish, J. (1983). *Language Leaners and Their Errors*. London: Macmillan.

Nida, E. (1975). *Language Structure and Translation.* Stanford: Calif Stanford University Press.

Njogu, K. Mwihaki, A. na Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Njoroge, M.C. (2006). "Linguistic Variation in Spoken English as Used by Teachers in Kenyan Primary Schools." Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyamasyo, E. A. (1994). An Analysis of Spelling Errors in the Written English of Kenyan Pre- University Students. *In Language Culture and Curriculum* Vol. 7:1 1994. Great Britain.

Nyarige, P.K. (2002). "Thematic Organization and the use of Reference Cohesion in Written Composition." Tasifu ya M.A ya chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ogalo, M. (2010). "Factors Affecting Integration of the Four Basic Languages Skills in Secondary Schools in Gatundu Division, Kenya." Tasnifu ya M.A ya chuo Kikuu cha Kenyatta.

Okwara, M.O. (1989). "Factors Related to Achievement in English Composition among Secondary School Students." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kukuu cha Kenyatta.

Ombati, J. M. (2009). "A Comparision of Descriptive English Compositions of Visually Sighted Students in Kenyan Schools." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ombuna, O.V. (2014). "Valenisi ya Kitenzi katika Kishazi cha Kiswahili." Tasnifu ya chuo Kikuu cha Kenyatta.

Onguko, S.A (1999). A Comparative Study of Cohesion in Academic and Newspaper Text. M.A Thesis: Kenyatta University.

Onyango, J.O. (2006). “Verb Tonology in Olunyala.” Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Orodho, A. J. (2004). *Elements of Educational and Social Science Research Methods.* Nairobi: Masola Publishers.

Palmer, F. S. (1981). *Semantics.* London: Cambridge University Press.

Pearson, H. (1981). *The Teaching of Language Skills: Listening, Talking, Reading and Writing.* Nairobi: Oxford University Press.

Radford, A. (1997). *Syntax. A Minimalist*: *Introduction*. Cambridge : Cambridge University Press.

Redeker, G. (2000). *Coherence and Structure in Text and Discourse*. Amsterdam: Benjamins.

Redeker, G. (2000). Coherence and Structural Text and Discourse Parsing. *In Strube, M. and Sidner, C. (Eds.), Proceedings of the 5th Sigdial Workshop on Discourse and Dialogue.* (pp 108-117). Cambridge. MA USA April 30- May 1, 2004.

Saddimbah, C. R. (2011). “Cohesive Devices in Dholuo Sermons: A Textual Analysis.” Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Scinto, F.M. (1986). *Written Language and Psychological Development*. INC. Orland, Florida: Academic Press.

Sichangi, G. M. (2008). “Uarifu katika Taarifa za Habari.” Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Tanen, D. (1993). *Framing in Discourse.* New York: Oxford University Press.

Tanned, A.L. and Hamilton, A. (2001). *Project Management Towards Best*. New York: Oxford University Press.

Tanskanen, S.K. (2006). *Collaborating Towards Discourse: Lexical Cohesion in English Discourse.* Amsterdam: Benjamins.

Thiga, C.N. (1997). "Cohesion and Compactness in Compositions Written by Kenyan Urban Primary School Children." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Thompson, S. (1994). Aspects of Cohesion in Monologue. *In Applied Linguistics* 15 (1), 58-75.

TUKI (2004). *Kamusi Saniifu ya Kiswahili. (Toleo la pili).* Dar es Salaam: TUKI.

Ullman, S. (1972). *An Introduction to Science of Meaning.* Basil Blackwell: Oxford.

Vygotsky, L. S. (1986). *Mind in Society*. USA: MIT Press.

Waihiga, G. na Wamiltila, K.W. (2004). *Chemichemi za Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Were, E. A (1996). "The First Language Influence on Kiswahili Composition Writing: The Case of Babukusu Students from Kadunyi Division, Bungoma District." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wiersma, W. (1986). *Research Methods in Education*: *An Introduction*. Boston: Allyn and Bacon.

Yde, A. and Spoelders, O. (1985). Cohesion. An Exploratory Study with Beginning Writers. *Psycholinguistics 6.*

Yousif, E. (1995). "Cohesion in Spoken English Discourse of Arabs." Tasnifu ya M.A ya Chuo Kikuu cha Oklahoma.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho (i): Insha kwa Wanafunzi**

**Maagizo**: Andika insha itakayokamilikia kwa maneno..Itakumbukwa kuwa siku ya muhimu maishani mwao.

WAYNE OMONDI P13
2466
4 KASKAZINI

Andika insha itakayomalizika kwa, Itakumbukwa kuwa siku ya muhimu sana katika maisha yao.

HARAMU HUHALALISHWA

"Uuwii! Aisee! Njooni muwaone washerati Jibaba azima kama hili ~~linamchoza~~ linajaribu kunibia mke!" Ali alisikika akisema. Muda si muda tulialikaa nyumbani mwako kwani hata wasuahili walamba mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo.

Mkewe Ali alikuwa amekumbatiwa na mzee Mawewa wakijamiana. Mzee Mawewa alikuwa na umri mkubwa kiasi cha kwamba Ali na mkewe wangemwita baba. Aibu iliyoje! La! Dunia ina waku na virabu. Wanakijiji walijaa hadi ya kujaa. Walikuwa wamekasirika si haba kwani hii ilikuwa mazoea ya mzee Mawewa. Ebi kwa sababu alikuwa bwanyenye kijika. Kwa muda mrefu, mtindo ulikuwa ule wa akikalia kiyenda mbii lakini wakati huu wanakijiji walikuwa wameamua kumsaidia Ali kupigania haki za 'wanyonge'

Wanakijiji walibeba silaha si haba, si mikuki, si mishale, si virungu sikwambii, wale waliokuwa wamebeba maji moto ya kuwachoma wawili hawa. Umoja ni nguvu! Mzee Mawewa alijaribu kumshawishi Ali kwa kumpa kibitu kikubwa cha pesa lakini wapi, Alikambulia patupatu!! Waama, siku ya nyani kufa, miti yote huteleza. Punde si punde, wawili hao ambao bado walikuwa uchi wa mnyama waliamrishwa watoke

Kibandani vivyo hivyo. Woga uliwaingia. Nyoyo zikadunda. Walitamani ardhi ipasuke wa na kuwameza wangali hai lakini hilo halikuwezekana.

Mzee Mawewa alitangulia kutoka kibandani kwa mwendo wa kinyonga, huku akitetemeka mithili ya kifaranga aliyenyeshewa. "Tuambie unachofanya nyumbani mwangu na mke wangu," Ali alimwamrisha huku akimkodolea macho makali. "Ni...ni... mk...e ...wa...ko... aliyeni...ita hapa. Alitaka nimsa...idie kati...ka biashara. Sina ubaya mi...mi." Mzee Mawewa alisema huku akigugumia.

"Mpumbavu wewe!! Biashara katika kibanda yangu!" Haba haunа aibu wewe. ~~"Mtu mmoja mwenye msafi tangu~~ Ali aliskika akisema. "Mimi nina ~~siri~~ Pendekezo. Kama kunaye mtu hata mmoja hapa ambaye hajawahi kuwa na uhusiano wa nje ya ndoa awe wa kwanza kunipiga vita," Mzee Mawewa alisema. Lo! Kila mtu alimwangalia mwenzake, kuangusha virungu na silaha na kisha kuondoka. Wawili hawa walikuwa wamepona aibu chupuchupu. Aisee! Haba haramu uhalalishwa. Wawili hawa walijifunza mengi na kuwa wenye maadili kutoka siku hiyo. Itakumbukwa kuwa siku ya muhimu sana katika maisha yao.

P9

2292 4 NORTH

~~Andika insha itakayomalizikia itakumbukwa siku ya muhimu~~

Andika insha itakayomalizikia itakumbukwa kuwa siku muhimu katika maisha yao.

Milango ya kanisa ilifunguliwa, mlangoni Bi harusi alisimama huku akiwa amevaa rinda jeupe pepepe. Kando yake alisimama mwanaume mwenye miraba minne. Machozi ya furaha yalinitiririka kumwona dada yangu Sela akifunga pingu za maisha. Hadhira iliyowasili ilikuwa kubwa, si watoto si wazee si akina baba si akina mama wote walikusanyika hapo.

Mwanaume aliyempeleka Bi harusi katika Bwana wake alikuwa ni mjomba wetu aliyekuwa katika jeshi. Sote tuliwaangalia kwa furaha kwani mwenye macho haambiwi tazama. Kasisi alimpokea Bi harusi na kisha sherehe ikaanza. "Bwana Joakim Mwatela unamchukua Bi Sela Maende kama bibi yako kwa shida na kwa furaha, kwa magonjwa na kwa afya heri leo mpaka mtakapo aga dunia." Kasisi alisema. "Ndio" nitamchukua Sela." Joakim alimjibu "Na wewe Sela utafanya hivyo pia." Kasisi alimuuliza Sela huku akimkodolea macho. "Naam namchukua." Sela alijibu kwa amri.

"Nawaunganisha kama Bibi na Bwana na iwapo kuna aliye na pingamizi aitoa sahi ama aiweke mpaka milele." Kasisi alisema. Hadhira yote ilikuwa tuli kama maji ya mtungi. Hakuna aliyeitoa pingamizi yoyote kweli hakuna mtu katika hadhira ambaye hakupendezwa na wapenzi hawa wawili.

Punde si punde ibada ilipoisha Bwana na Bi Mwatela walitembea asteaste huku wakielekea katika hoteli kuu ya Ole serani. Huko wange shsherekea

mwanzo wa maisha yao mapya kama Bibi na Bwana. Vyakula vilikuwa vimeandaliwa na wapishi hodari kwani chakula hiki kilikuwa ni cha hadhira muhimu. Huku ni watu sabini tu waliokuwa wamealikwa kwani hoteli hiyo haikuwa hoteli ya kawaida. Nilipomtazama Sela mawazo yalinijia kichwani kwani niliyapata mawazo ya utotoni wetu. Sela alikuwa ameiota siku hii tangu utotoni. Tulipitia mateso chungu nzima lakini kama wahenga wanavyosema yaliyopita si ndwele na tunafaa kuganga yaliyopo.

Sherehe ilikuwa bora zaidi kwani kila mtu alijivinjari. Wengi wataikumbuka sherehe hii kwani kila mtu aliachwa na furaha. Siku hiyo itakumbukwa kuwa siku ya muhimu katika maisha yao.

- Nafsi – 3, 1, 2
- Vimilikishi – GKe
- Leksis – Colloc
- Vuunganish, ongeza, ulelezi
- Mwendelezo
- Visishi – Kati, ikawa
- lex – amisi, bw. amisi, chakula, wapishi, colloc (hadhira)
- Ubadilishaji.

(Mshikamano upo)

P6.

Kwesi Essuman 2246 4NORTH

Anza Insha itakayo kamilika ... Itakuwa siku ya majuto sana kwa maisha yao.

Pingu mkononi, askari wakiwa fwata nyuma, Hassan na Juma walitoka mlango ya korti baada ya wambizi wa mashtaka yao katingwa. Familia zao wakitoa machozi kuona vijana wao walichaguliwa jela kuanzia kifungo chao cha maisha baada ya kupatwa na kosa ambayo wao wenyewe walijitakia. Mwiba wa kujidunga hauambiwi pole hivi basi Hassan na Juma hawakuwa na budi ila kuh kubeba mzigo wao. Lakini je? Ni nini kilichotokea hadi kufika kiwango hiki?

Ilikuwa miezi mitano yaliyopita. Hassan mwanafunzi wa uhandisi wa ndege katika chuo kikuu cha Jomo Kenyatta alikuwa akitembea baada ya kutoka darasani. "Vipi ya leo kaka?" Juma, rafikiye alimsalimu kwa furaha. "Siwezi lalafa mimi, siyo wewe?" Hassan alimjibu "Ah! Basi nina kitu ambacho kitakacho kufurahisha, nina suluhisho ya shida zetu zote za pesa," Hasse Juma alimwambia. Neno pesa ulimkamata Hassan kutoka bahari ya fikra na kumsikiliza Juma kwa makini. Hapa Hapo ndipo Juma alifungua mkoba wake, na ndani yake aliona Juma kitu ambacho hakutarajia "Aisee! Wataka nini na bangi wewe? Unajua wakuze polisi kortini na wahalifu, mbishola kupata gerezani," Hassan alimjibu "Tulia kaka, sitaki dawa hizi bali tutakaze nao uchakika kwamba utanishukuru baadaye" kutoka hapo Juma aliacha zake.

Hassan baada ya kufikiria aliona haja ya dawa hizo na kumpigia Juma kumwambia kuwa alikubali pendekezo lake. Hakukupita hata siku moja kwa hile kazi ilianza siku ifuatayo. Juma na Hassan walizunguka kote Nairobi wakiuza bidhaa zao haramu, na kwa kweli walipata kila si chache wateja. Hakuna asiyeweza kununua dawa hizi. Sijawahi, si wanawake, si wazee, si wanafunzi hakuna aliyewahi na kungojea na baada ya wiki ya kwanza vijana hao walikuwa kujani kwa wakwasi wa wakwasi

Hali hii ya wageni wengi ililetelea watu kubadili maisha ya Hassan alianza kunza chuoni ili kuendeleza mahaduri yake kwa vile alishapata pesa, bali kuna na gereji na magari ya ashapata chake alichotaka Naye Juma a [illegible] alikata kama kufadhili nyumba kwa vile hali hii iliimpa ameri wa kujitegemea.

Lakini wachenge hawakutachiwa shule za chini kwa chini walipokuwa Ugeni wa ngeni Kauli jengwani Usiku mmoja Hassan na Juma walipokuwa katika hulka yao ya kazi duka hio, walimtikia mja mmoja ambaye alikuwa mteja wao wa dhati kwa bei wale walimwambia kuba kile kitu kingeanzalia Kasoro kama kuuawa, walipata pesa za kiste wendi zao. Punde tu walipokuwa wakimpa mizigo yake polisi waliwakuli, mojawapo wa mirabe minne, wakizialikiwa bunduki zao kwa Hassan na Juma. Umepatikana na kosi la kuuza dawa za kulevya, wa haki ya kibohi kimya na chochote utakachosema kitatumiwa dhidi yako kortini! Walibwa mbenor na siku iliyofuata walifikishwa kortini na kupatikana na hatia ya kuuza dawa za kulevya na kupewa kifungo cha maisha. Itakumbukwa kuwa siku muhimu sana kwa maisha yao.

Mwejo dokezi
lek - (Jela, kifungo, kesi) collo
jumla - kesi, mseto
- Nafsi - 3, 1
Vimilikishi - 50
- Ubadilishaji
- lek (wazo)
- umaliza
- vieleleze
- vitagaruzi - ongeza, wakati
- viashiria - kaniuh, kari

Potasi
vyeo
dawa za
kulevya
sikio 5

Hali hii ya wasiwasi iliendelea wakati huo. Mawazo ya Hassan alikuwa kwenda chooni ili kuondoa mahitaji yake kwa vile alishtuka pia, bali kiatu na gauni na kitabu na alishika chake alichotaka Naye Juma ~~[illegible]~~ alikata kauli kuendelea nyumbani kwa vile hali hiyo ~~[illegible]~~ ilimpa nafasi ya kujitegemea.

Lakini walimwengu hawakukutachelewa sana. Je chini kwa chini walipoona Ujenzi wa nyumba hiyo jengwa! Usiku mmoja Hassan na Juma walipokuwa katika hali yao ya kawaida hiyo, walishtukia mjumbe mmoja ambaye alikuwa mteja wao wa [sikuzote] hivi basi wali waliona kuwa kila kitu kingeendelea kama kawaida, wakipeleka pesa zao kwa wenzi zao. Punde tu walipokuwa wakimpa mizigo yake polisi walikuwa wameshawafunga minyororo, wakizielekea bunduki zao kwa Hassan na Juma. Umefika na kazi ya kuwa dawa za kulevya, na hiki ni kitabu kinyume na shughuli zinazopigwa marufuku na ... kitatumika dhidi yako kortini! Walibaki mbele na siku iliyofuata walifikishwa kortini na kupatikana na hatia ya kuuza dawa za kulevya na kupewa kifungo cha maisha. Itakumbukwa kuwa siku muhimu sana kwa maisha yao.

Mwijeo dokezi
lek – (Jela, kifungo, COHOE) Jumla – kesi, … abiria …
kesi

– Nafsi – 3, 1
Vimilikishi – 50
– Ubadilishaji
– lek (wizo)
– unadilifu
– vendeleo
– viunganishi – Orgasm, wakati
– vipashi – kanuni, kani

Potasi

vyeo
dawa za
kulevya
ubaradhi siku
mahumu kwa

Siku 3
① …
② …
③ …
④ …

## Kiambatisho (ii): Zoezi kwa Wanafunzi

Ngugi Alphonce

06/10

**Kiambatisho (ii): Zoezi kwa wanafunzi**

Kidato ...Cha one...

**Maagizo :** Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo uliyopewa

i) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viunganishi mwafaka;

a) Mama anasoma. Baba anasoma

Mama na baba wanasoma 1

b) Nilikula jana. Sikushiba.

Nilikula jana ila sikushiba 1

c) John ni mrefu. Moraa ni mrefu zaidi

Moraa ni mrefu kuliko John 0

2. Geuza sentensi zifuatazo kwa "o" rejeshi.

a) Mtoto ambaye alipita mtihani ametuzwa.

Mtoto aliyepita mtihani ametuzwa 1

b) Mwalimu ambaye anafunza kila siku ni bora.

Mwalimu anayefunza kila siku ni bora 1

3. Andika visawe vya maneno haya:

31

a) Mwanafunzi ...... Mkafunzi ...... 0

b) Shule ...... Shuli ...... 1

c) Mtoto ...... Mwana ...... 1

4. Sahihisha kwa kuondoa urudiaji usiofaa;

a) Kalamu ya John ni ndefu. Kalamu ya Jane ni fupi.

...... Kalamu ya John na Jane ni fupi ...... 0

b) Darasa la wanakidato cha pili ni chafu. Darasa la wanakidato cha tatu ni safi.

...... Darasa la wanakidato cha pili ni chafu ilhali cha tatu ni safi ...... 0

02

## Kiambatisho (iii): Hojaji kwa Walimu

Mugoiri

**Kiambatisho ( iii): Hojaji kwa walimu**

Mwalimu,

Ahsante sana kwa kukubali kushiriki katika utafiti huu. Tafadhali tia alama ya (√) katika jibu ulilolichagua au toa maoni yako. Majibu ya utafiti huu hayatatumiwa kupima ufunzaji wako bali ni katika kuboresha matokeo ya mtihani wa karatasi 102/1(Insha) kwa jumla. Karibu.

Eleza kwa ufupi mbinu unazotumia kufundisha masomo yafuatayo;

i) Insha – wanafunzi kuandika insha kisha na baadaye kupitia pamoja nao.
– Kutumia mifano halisi k.v kadi za mwaliko, shajara za vitabu.
– Wanafunzi kushiriki katika kutoa mifano k.v katika ufundishaji wa
– insha za mazungumzo – kutoa mazungumzo mbalimbali ambayo wanayoyasikia kwenye redio na redio.

iii) Viunganishi

– Kuigiza baadhi yake mf. Lakini, na
– wanafunzi kutunga sentensi kwa kuvitumia viunganishi
– Matumizi ya michoro yenye viunganishi katika sentensi.

iv) Msamiati

- Kutoa mifano mahususi - uigizaji wa maana za maneno - mf vitisho
- Kupitia makosa katika kamusi (jalada magumu) kisha kuyatumia sentensi

2. Unawezaje kukadiria kiwango cha wanafunzi wako? Chagua kwa kutumia alama ya mkwaju kwa a, b, c, d na e.

a) Komavu ✓ kwa

b) wastani ✓

c) Hafifu

d) Kisichoridhisha

e) Dhaifu.

Eleza sababu za jawabu lako.

Wanafunzi wengi hawafanyi mazoezi ya insha na hungoja tu wakati mwalimu atawapa zoezi.

3.a) Je, kwa maoni yako mshikamano una una umuhimu wowote katika insha za wanafunzi?

huwasaidia kupitisha ujumbe

Ndio, kwa mfano [illegible] mada za [illegible] wajadili [illegible] Kubadilisha [illegible].

unavutiwa kwa ufasaha

b) Ikiwa jibu lako ni ndio katika 4 (a), kwa maoni yako ni nini husababisha ukosefu wa mshikamano katika insha za wanafunzi?

-Ukosefu wa umakini wanapoandika.
-Tafsiri mbaya ya maswali
- Papara ya kujibu maswali

c) Hali hiyo inaweza kuboreshwaje?

-Kuwaelekeza darasani kuelewa maswali ipasavyo.
-Kuwapa mazoezi zaidi ukiwa na lengo maalum la kushughulikia hali hii.

4. Andika changamoto unazokabiliana nazo unaposhughulikia somo la insha;

i) Darasani

-Wanafunzi kutopenda insha.
-Wanafunzi kutoweza kupanga mawazo yao ili kuwasilisha insha na mambo ya kila siku.

ii) Unaposahihisha insha za wanafunzi

- Idadi ya wanafunzi ni kubwa.
- Athari za lugha mama na Sheng.
- Wanafunzi kuandika insha fupi.

5. Chagua mojawapo; Mimi hufundisha na kusahihisha insha:

a) Kila wiki ✓

b) Kati ya mara moja na tatu kwa mwezi

c) Kati ya mara moja na mbili kwa muhula

d) Kati ya mara moja na mbili kwa mwaka

e) Zaidi ya mwaka mmoja

f) vingine

Eleza Insha hizo hupitiwa darasani kwa pamoja

## Kiambatisho (iv): Kibali cha Utafiti



THIS IS TO CERTIFY THAT:
MS. MARGARET MORAA OGATO
of KENYATTA UNIVERSITY, 179-10205
Maragua,has been permitted to conduct
research in Muranga County


on the topic: NAFASI YA MSHIKAMANO KATIKA KUKUZA MAUDHUI KATIKA INSHA ZA WANAFUNZI WA KIDATO CHA NNE KATIKA KAUNTI YA MURANGA

for the period ending:
17th January,2018

Permit No : NACOSTI/P/17/72446/15183
Date Of Issue : 18th January,2017
Fee Recieved :ksh1000

Applicant's
Signature

Director General
National Commission for Science,
Technology & Innovation



CONDITIONS

1. You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit.
2. Government Officer will not be interviewed without prior appointment.
3. No questionnaire will be used unless it has been approved.
4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.
5. You are required to submit at least two(2) hard copies and one (1) soft copy of your final report.
6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice

REPUBLIC OF KENYA

National Commission for Science, Technology and Innovation

RESEACH CLEARANCE PERMIT

Serial No. 12488

CONDITIONS: see back page

**Kiambatisho (v): Mwongozo wa KNEC wa Kusahihisha Insha**

VIWANGO MBALIMBALI KWA MUHTASARI

| KIWANGO | NGAZI | MAKI |
|---|---|---|
| A | A+ | 19-20 |
| | A | 18 |
| | A- | 16-17 |
| B | B+ | 14-15 |
| | B | 13 |
| | B- | 11-12 |
| C | C+ | 09-10 |
| | C | 08 |
| | C- | 06-07 |
| D | D+ | 04-05 |
| | D | 03 |
| | D- | 01-02 |

4